# Nipashe

Jumamosi Januari 7, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581183

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital   nipasheTZ   nipasheTZ   nipasheTZ   0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT
TZS. 1,063,605,974
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




**Katibu** Mkuu aiwakia MSD kwa utendaji mbovu vituoni

UKURASA 3




UKURASA 13

# Wastaafu wawasilisha hoja 13 kwa serikali

• **Limo** dai nyongeza ya mafao, malipo ya maziko... *Endelea Uk. 2*



Waziri Mkuu,Kassim Majaliwa akikagua maendeleo ya ujenzi katika Hospitali ya wilaya ya Namtumbo akiwa katika ziara ya mkoa wa Ruvuma jana. Waziri Mkuu Majaliwa alitembelea hospitalini hapo Oktoba mwaka jana na kuagiza kasoro zilizokuwepo ikiwemo milango 10 iondolewe na kuwekwa mingine yenye viwango ifikapo Januari 4 mwaka huu. **PICHA: OWM**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### DK. SLAA AIBUKA NA UTATA WA LUGHA KWENYE MAJUKWAA

ALIYEKUWA Balozi wa Tanzania nchini Sweden, Dk.Wilbroad Slaa ameibuka na kudai kuwa upo utata katika tamko la serikali kuhusu matumizi ya lugha kwenye mikutano ya hadhara, akisisitiza unapaswa kuondolewa...

UKURASA WA 4

### MAJALIWA ARIDHISHWA MABORESHO HOSPITALI YA WILAYA NAMTUMBO

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amesema ameridhishwa na maboresho yaliyofanyika kwenye Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa Oktoba 18 mwaka jana alipozuru hospitalini huko...

## CHADEMA waibuka na mikakati kuendesha mikutano ya kisiasa

UK. 2



## Waziri amtumbua meneja RUWASA

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA YAENDA DUBAI UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar Dk.Hussein Ali Mwinyi na mkewe Mariam Mwinyi,(kushoto) wakimsikiliza mwanafunzi wa darasa la Saba wa Shule ya Msingi Salum Turky, Abdul Aziz Suleiman alipowakaribisha katika chumba cha Maktaba mara baada ya kuifungua rasmi jana. Wengine ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Lela Muhamed Mussa (kulia) na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Khamis Abdulla Said ikiwa ni sehemu ya sherehe za shamra shamra za maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# Wastaafu waibuka na hoja 13 kwa serikali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UMOJA wa Wastaafu Tanzania (REAT) umewasilisha hoja 13 serikalini, likiwamo pendekezo la kuongezwa kima cha chini cha pensheni ya kila mwezi kutoka Sh. 100,125.40 ya mwaka 2015 hadi Sh. 259,000.

Rais wa REAT, Dauda Bilikesi alibainisha hayo jana jijini hapa alipotoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu hoja zilizowasilishwa na umoja huo serikalini.

"Hoja zilizowasailishwa serikalini kwa Mheshimiwa Dk. Dorothy Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na zikapokewa kwa niaba ya Makamu wa Rais ni hizi zifuatazo:

"Tumeiomba serikali na taasisi zake na Bunge zitambue kuwa wastaafu wote nchini kwa sasa wana umoja wao ulisajiliwa kisheria, hivyo kabla ya kufanya uamuzi unaohusu wastaafu, watoe fursa ya kupokea maoni ya wastaafu kupitia REAT.

"Tayari tumemwandikia barua Spika wa Bunge kumjulisha kuwapo REAT, ili mhimili huo muhimu wa kutunga sheria utambue kuwapo kwetu na kutushirikisha katika masuala mbalimbali ikiwamo kujadili miswada ya sheria inayohusu hifadhi ya jamii na masuala mengine ya nchi.

"Pia tuna pendekezo la kuongeza kima cha chini cha pensheni kutoka Sh. 100,125.40 ya mwaka 2015 hadi Sh. 259,000 kwa kutumia kigezo cha kima cha chini cha pensheni kuwa ni theluthi mbili ya kima cha chini cha mshahara wa sekta husika.

"Kiwango hicho kilichopendekezwa na REAT, kitakuwa ni sawa na theluthi mbili ya kima cha chini cha mashahara serikalini.

"Pamoja na hayo, REAT inatambua kuwa kama sheria iliyoanzisha Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) iliyoanzishwa 2018 ingekuwa inazingatiwa, Rais alipotangaza nyongeza ya mshahara kwa asilimia 23.5 kima cha chini cha pensheni nacho kilitakiwa kitangazwe na waziri mwenye dhamana ya mifuko ya hifadhi za jamii na kilipaswa kuwa Sh. 155,610".

Hoja nyingine iliyopendekezwa na REAT, ni wastaafu waliostaafu kabla ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) waingizwe kwenye mfuko huo kwa kulipiwa na serikali au kwa kuwapa unafuu wa kulipa kiasi kidogo kila mwaka ili wapate huduma ya matibabu.

"Wizara ya Afya iimarishe utaratibu wa matibabu ya wazee wanaotibiwa kwa kutumia vitambulisho vya bima ya afya hasa pale ambapo hakuna dawa hospitalini na pale ambapo hospitalini haina kipimo kinachotakiwa kumpima mgonjwa na kutakiwa kwenda kupimwa sehemu nyingine," alisema.

Vilevile, alisema waastaafu wote waliopunjwa pensheni, waliopandishwa madaraja bila ya kurekebishiwa mishahara yao, waliokuwa wamezuiwa kulipwa pensheni mpaka mwajiri alipe tozo, waliohitimisha utumishi wao hawajarejeshwa nyumbani, wapate stahiki zao kwa mujibu wa sheria.

"Pendekezo lingine ni wastaafu kuwa na uwakilishi kwenye Bodi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na wastaafu kuzikwa na mifuko wanapofariki dunia, ili kulinda heshima yao," alifafanua.

Vilevile, alisema watoto wa wastaafu wenye ulemavu wasiojiweza, waendelee kupokea pensheni mpaka wafe kama ilivyo kwa watoto wa wanachama wa mifuko wanaofariki dunia kabla ya kustaafu.

"Tumewasilisha serikalini pia pendekezo la kuwatumia wastaafu kutoa mafunzo kwa wafanyakazi waliko kazini juu ya maadili ya kazi na maandalizi ya kustaafu," alisema

# CHADEMA waja na mikakati mikutano ya hadhara 2023

**Na Maulid Mmbaga**

KAMATI Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) imeagiza viongozi wa ngazi zote za chama hicho kuendelea na maandalizi ya kuanza kwa mikutano ya hadhara.

Chama hicho kimetangaza kuwa kinatarajia kufanya uzinduzi rasmi wa kitaifa wa mikutano hiyo Januari 21 mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, hatua hiyo imefikiwa baada ya Kamati Kuu kukutana na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kujadili taarifa ya mwenendo wa mazungumzo ya maridhiano.

Mrema alisema kamati hiyo imeridhishwa na mwenendo wa mazungumzo hayo na hatua ambazo zimechukuliwa mpaka sasa na kuitaka timu ya mazungumzo iendelee na mchakato huo wa maridhiano, huku hatua za kuandaa mikutano ya hadhara zikiendelea.

"Kamati Kuu imetangaza kuwa uzinduzi rasmi wa mikutano ya hadhara kitaifa utafanyika Januari 21 mwaka huu na utafuatiwa na uzinduzi wa mikutano ya hadhara kila makao makuu ya kanda na baadaye ngazi nyingine za chama zitaendelea na mikutano kwenye ngazi zao," alisema Mrema.

**CUF KUMEKUCHA**

Wakati CHADEMA wakitangaza hayo, Chama cha Wananchi (CUF) kimesema kuanzia sasa kitafanya mfululizo mikutano ya hadhara kwenye mikoa mbalimbali, huku kikiwataka viongozi wake ngazi ya shina, kata, wilaya na mikoa yote nchini kuanza maandalizi, uzinduzi rasmi wa mikutano hiyo ukitarajiwa kufanyika leo Magomeni mkoani Dar es Salaam.

Hatua hiyo imekuja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan Januari tatu mwaka huu kuondoa zuio la kufanyika kwa mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa, katazo ambalo lilidumu kwa takribani miaka saba.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Naibu Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguri wa CUF, Yusuph Mbungiro, alitoa rai kwa wananchi kuendelea kukiunga mkono chama hicho, huku akimpongeza Rais Samia kwa kuwa msikivu na kuona umuhimu wa kufuata sheria na katiba ya nchi katika kujenga misingi bora ya demokrasia nchini. "Vyama vya siasa takribani miaka sita tumekuwa hatufanyi mikutano ya hadhara, baada ya zuio lililokuwa limewekwa na Rais aliyetangulia lakini sasa limeondolewa.

"Ninatoa wito kwa wanachama wa CUF, tuko kwenye kipindi cha uchaguzi wa ndani ya chama ulioanza Mei 2022 na utamalizika Oktoba mwaka huu, hivyo wanachama waendelee kujenga hamasa.

"Hamasa iendelee kujengwa ili kuwahamasisha watanzania kuendelea kukiunga mkono chama chetu, tunaamini kwa kipindi hiki watanzania wataona vyama vya siasa vikienda kwenye mikutano ya hadhara, vikinadi sera, vikiikosoa serikali kwa nia njema ya kulijenga taifa letu," alisema Mbungiro.

Pia alisema vyama vya siasa ni mhimili muhimu katika demokrasia ya nchi na ujenzi wa maendeleo ya taifa.

Kutokana na katazo la mikutano ya hadhara kuondolewa, alitoa wito kwa Jeshi la Polisi nchini kuwa sikivu na lifuate sheria na kuacha kuwa watu wa kutabiri na kupanga mikakati ya kuzuia vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara.

"Tunashauri na kuwaomba vyombo vya usalama, mambo ya kiintelejensia ambayo mara nyingi yamekuwa yakitumika kama njia ya kuzuia baadhi ya mikutano ya hadhara, kwamba unaambiwa mkutano huu hautaweza kufanyika kwa sababu za kiintelejensia, sasa hizo sababu za kiintelejensia tunahitaji zitumike kuifanya mikutano ifanyike na siyo kuizuia," alisema Mbungiro.

Aliahidi kuwa watafanya mikutano ya hadhara ambayo itakuwa na tija kwa taifa, akisisitiza kuwa hawataifanya kwa ajili ya kukashfu watanzania wala viongozi wa serikali au wa vyama vingine.

"Mikutano yetu itakuwa ni ya kunadi sera za chama chetu, kukosoa pale serikali inapokuwa imekosea na kusimamia ujenzi wa demokrasia ndani ya taifa letu, hayo ndiyo mambo ya msingi tunayotarajia kuyafanya kwa kipindi hiki," alisema Mbungiro.

# Katibu Mkuu aiwakia MSD utendaji mbovu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, ameeleza kuchukizwa na utendaji kazi mbovu wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kushindwa kufikisha dawa muhimu katika vituo mbalimbali vya afya na kusababisha madeni.

Kutokana na hali hiyo, ameipa MSD miezi miwili kuhakikikisha inamaliza tatizo hilo nchini.

Prof. Makubi alitoa agizo hilo juzi jijini hapa wakati akizungumza na wadau na viongozi mbalimbali wa afya juu ya uboreshaji wa huduma ya afya kwa wananchi sambamba na utekelezaji wa bima ya afya kwa wote unaotarajiwa kuanza Julai 2023.

MSD, alisema imesababisha hali ya upatikanaji wa dawa muhimu kuwa mgumu hasa katika vituo vya serikali na kuwalazimu kufuata dawa nje ya vituo ilihali tayari vimelipia gharama kubwa za kuagiza dawa kwao lakini bado idara hiyo haipeleki dawa katika vituo kwa wakati.

Alisema serikali imetengeneza miundombinu na majengo ili kuboresha huduma za afya lakini si lolote kama maeneo ya kutolea huduma hizo hayana dawa kwa ajili ya wagonjwa na hawako tayari kuendelea kuwavumilia wakishindwa kupeleka dawa hizo ndani ya muda alioutoa.

"Haiwezekani mnadaiwa fedha nyingi hadi katika vituo vidogo vya afya kwa kuendelea kuwacheleweshea dawa za muhimu ambazo zinaweza kupatikana hata katika sehemu tofauti nchini bila kuzifuata Dodoma. Nawapeni miezi miwili pelekeni dawa mkishindwa wapeni tenda wanaoweza kufanya usambazaji kwa wakati" alisema Prof. Makubi.

Katika hatua nyingine, Profesa Makubi alikemea vituo vikubwa vya kutolea huduma za afya ambavyo vinafanya utapeli wa gharama halisi za matibabu kupitia Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa (NHIF) huku ikitishia kufungia vituo hivyo.

Alisema serikali itavifungia vituo vinavyofanya utapeli wa gharama za matibabu vilivyoingia katika mkataba na NHIF vihakikishe vinafuata miongozo na mkataba waliotia saini.

Prof. Makubi alisisitiza kuwa serikali haitasita kuvifungia vituo vyote vya kutolea huduma ambavyo vitafanya utapeli kuhusu gharama halisi zilizotumia mgonjwa.

Aidha, aliwataka watoa huduma kuendelea kutoa huduma katika ubora stahiki na kuacha tabia za kuendekeza matusi kwa wagonjwa ilihali ndio waajiri halisi wa watoa huduma hao.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alisema serikali mkoani Mwanza imeanza mpango kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya rufani ya mkoa ndani ya halmashauri za Ilemela, Misungwi, Magu au Nyamagana.

Mwakilishi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) , Monica Julius, aliwataka wasimamizi wa utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya hospitali mbalimbali na vituo vya afya kuhakikisha wanakamilisha miradi hiyo kwa wakati ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi.



Baadhi ya wenyeviti wa vitongoji vya mji mdogo wa Mirerani Wilayani Simanjiro Mkoani Manyara, wakikagua korongo la kuzuia maji ya mto Nduruma na bwawa la Kidawash yanayosababisha mafuriko juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Jafo ambana DED fedha ujenzi kituo

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk.Selemani Jafo, amemwagiza Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Peter Ngusa, kupeleka fedha za kumaliza ujenzi wa Kituo cha Afya Kiluvya.

Dk. Jafo, ambaye ni Mbunge wa Kisarawe alitoa maagizo hayo jana alipofika kukagua maendeleo ya kituo hicho wakati wa ziara yake ya siku moja kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema kituo hicho kilikuwa hitaji la wananchi kwa muda mrefu ambao walikuwa wakitembea umbali wa kilomita tano kufuata huduma za afya katika Zahanati ya Makurunge.

"Maagizo yangu kwako Kaimu Mkurugenzi hapa fedha ziletwe. Kamati imesema inahitaji Sh. milioni 40 kukamilisha lakini tuanze kuwaletea Sh. milioni 25 jengo likamilike na huduma zianze kutolewa, wananchi waondokane na hii shida ya kutembea umbali mrefu," alisema.

Katika ziara hiyo, Dk. Jafo alizindua daraja la Mto Bululu na Makurunge ambayo yalikuwa kikwazo hususani kipindi cha mvua na maeneo hayo yalikuwa hayapitiki.

Madaraja hayo ambayo yamegharimu Sh. milioni yalikuwa hayapitiki kipindi cha mvua na wakati mwingine wanafunzi walikuwa wakikwama kwenda shule.

Waziri huyo alisema kata hiyo itaendelea kusimamiwa kwa karibu kutokana na kuwa eneo la mjini, hivyo kuhitaji miundombinu ya barabara kila sehemu na huduma za jamii kusogezwa karibu na jamii kuondoa msongamano kwenye vituo vilivyopo.

# Waziri Aweso amtumbua meneja RUWASA

**Na Christina Haule,** KILOSA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amemwondoa katika nafasi yake Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA) Wilaya ya Kilosa, Mhandisi Joshi Chum, na kuagiza kupangiwa kazi nyingine.

Sambamba na kuondolewa kwa meneja huyo kutokana na utendaji kazi wake kwenye miradi ya maji kutoridhisha, Aweso pia ametangaza kuifuta Jumuiya ya Watumiaji Maji Ruaha.

Aweso alitoa agizo hilo juzi akiwa Ruaha, Mji mdogo wa Mikumi Wilaya ya Kilosa wakati akiendelea na ziara ya siku tisa kukagua miradi ya maji mkoani Morogoro.

Waziri alichukua uamuzi huo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi, Diwani na Mbunge wa Mikumi, Dennis Londo, juu ya kero ya kudumu ya maji kwenye kata hiyo ambayo licha ya serikali kupeleka fedha za utatuzi, ujenzi umechelewa kuanza bila sababu maalum.

Alisema Wizara ina nia njema na watendaji wake huku ikiwa na nafasi nyingi, hivyo mhandisi huyo ni vyema akarudi wizarani na mtu mwingine mwenye uwezo wa kufanya kazi na kusimamia miradi apelekwe wilayani Kilosa.

"Kwa dhati ya moyo kabisa pamoja na kazi nzuri anayoifanya mhandisi huyu, kwa Ruaha naomba atupishe. Wizara ya maji ina nafasi nyingi za kufanya kazi, tutakupa nafasi nyingine lakini Kilosa tutamleta mtu ambaye atawasaidia Ruaha," Alisema.

Pia Waziri Aweso alisema kabla ya kuwa Waziri alikuwa naibu waziri katika wizara hiyo na alifanya ziara kwenye mkoa wa Morogoro na jimbo la Mikumi lakini kilichomsikitisha, wataalamu wake hawakuwahi kumpeleka Ruaha hata mara moja.

Aliwataka wahandisi wa maji nchini kuhakikisha wanampeleka kwenye changamoto za maji pindi anapofanya ziara kwenye maeneo yao ya kukagua miradi ya maji ili kuzitatua.

"Nionyeshe masikitiko yangu na nitume salamu kwa wahandisi wote nchini. Waziri wa Maji anapokuja kukagua miradi, mpelekeni kwenye changamoto, ndugu zangu wana Ruaha leo sijaja kuuza sura nimekuja kufanya kazi.

Elezeni kero zenu wala hamna sababu ya kumwogopa mtu ambaye anakwamisha maendeleo yenu," alisisitiza.

Aweso alisema wakati mwingine wananchi wanakosa kupiga hatua za maendeleo kwa sababu ya kuwabeba watu kwa kuwaonea huruma na kuwakumbatia wanaowarudisha nyuma, lakini bila Mbunge Londo asingefika Ruaha.

Kuhusu jumuiya za watumiaji maji nchini, Waziri alisema ameivunja Jumuiya ya Ruaha ili iwe jumuiya ya mfano kwa jumuiya zingine nchini kwa sababu ya uwapo wa baadhi ya jumuiya nyingi hewa na zinazowanufaisha viongozi badala ya kutekeleza majukumu yaliyowapeleka.

Aliagiza mamlaka za maji kuanza kuzifanyia uchunguzi wa kina jumuiya zote nchini kwa sababu ya kuwapo kwa watumishi wanaokula fedha za umma na ikibainika yuko anayekula fedha hizo, hatasita kumchukulia hatua.

Aweso alisema katika kukabiliana na changamoto zinazojitokeza kwa wananchi wa Ruaha juu ya masuala ya maji, ni vyema wakaanzisha Mamlaka ya Maji Ruaha watakayoitumia kutatua changamoto zao kwa karibu na mkurugenzi atakayekuwapo.

Mbunge Londo alisema pamoja na juhudi za serikali katika kuhakikisha jimbo hilo linapata maji, imetenga Sh. Bilioni moja kwa ajili ya uchimbaji visima vikubwa na kufunga pampu za mabomba ya maji katika maeneo yenye uhitaji zaidi kwenye jimbo hilo.

Aliyataja maeneo kutakapofungwa pampu za mambomba ya maji ni pamoja na kata ya Ruaha, Kidodi, Luhembe, Masanze, Kizunguzi, Mabwelebwele na Mhenda.



Mjumbe wa mkutano mkuu wa CCM Taifa, kupitia Wilaya ya Simanjiro Mkoani Manyara, Lenganasa Soipey akizungumza na jamii ya wafugaji wa Kata ya Naisinyai juu ya kutouza ardhi yao juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Dk. Slaa aibuka na utata wa lugha kwenye majukwaa

**Na Enock Charles**

ALIYEKUWA Balozi wa Tanzania nchini Sweden, Dk.Wilbroad Slaa ameibuka na kudai kuwa upo utata katika tamko la serikali kuhusu matumizi ya lugha kwenye mikutano ya hadhara, akisisitiza unapaswa kuondolewa.

Dk. Slaa aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), pia kuwania urais kupitia chama hicho, alitoa kauli hiyo wakati wa mjadala na moja ya vituo vya televisheni za mtandaoni.

Alisema kuwa iwapo tamko hilo litaachwa kama lilivyo, litaleta mvutano mkubwa kati ya polisi na vyama vya siasa kutokana na tafsiri tofauti zitakazopatikana kwa taasisi hizo.

"Hivi lugha ya staha maana yake nini? Lugha nzuri au lugha ya kutokutukanana maana yake nini? Katika siasa nani anaweza kusimama na kutuambia huyu katukana na huyu hajatukana?

"Tanzania ni nchi ya sheria. Je, katika sheria zetu ni nani mwenye haki ya kutafsiri huyu katukana mwenzake au huyu kaongea lugha mbaya?" Dk. Slaa alihoji.

Kwa mujibu wa Dk. Slaa, tamko hilo ni kama agizo kwa polisi kutafsiri kwa namna wanavyoona inafaa lugha za wanasiasa kuona matusi ama la, jambo ambalo alidai litasababisha mgogoro kati ya polisi na vyama vya siasa na hivyo kuharibu maana ya kuruhusiwa kwa mikutano ya vyama vya siasa.

"Kuwapo mikutano ya hadhara kumetafsiriwa na sheria. Kwanini Rais leo aingize maneno ambayo yanaweza kesho kuleta utata mapema kabisa?

"Tumekuwa tunafanya mikutano ya hadhara na nimezunguka nchi hii ninaijua, polisi anapanda jukwaani anakufuata pale umetukana au ulichokisema siyo lugha ya staha, lugha ya staha ni ipi? dictionary (kamusi) ya lugha ya staha iko wapi?" Dk. Slaa alihoji zaidi.

Kwa takribani miaka saba kumekuwa na zuio la mikutano ya kisiasa nchini. Mwanzoni mwa wiki hii, serikali iliruhusu mikutano hiyo na tayari vyama mbalimbali vya siasa vimetangaza kuanza kuifanya nchi nzima.

# Majaliwa aridhishwa maboresho Hospitali ya Wilaya Namtumbo

**Na Mwandishi Maalum,**
NAMTUMBO

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amesema ameridhishwa na maboresho yaliyofanyika kwenye Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa Oktoba 18 mwaka jana alipozuru hospitalini huko.

Akiwa kwenye hospitali hiyo siku hiyo, Majaliwa alieleza kutoridhishwa na milango iliyowekwa na kuagiza iondolewe na iwekwe mingine yenye viwango na jana alikagua maendeleo ya utekelezaji wa maagizo yake na aliridhishwa na kazi iliyofanyika.

Kufuatia utekelezaji huo, Waziri Mkuu alisema ameridhishwa na utekelezaji wa maelekezo hayo ambapo hadi sasa jumla ya milango 67 kati ya 84 imeondolewa na kuwekwa mipya yenye ubora.

"Leo (jana) nimeona milango bora kabisa, kwa nini tulikubali kuweka milango mibovu wakati mizuri ipo? Hii haikubaliki kwa sababu tunapoteza fedha za serikali zinazotokana na kodi ya wananchi. Ni lazima kila mtumishi wa umma atimize wajibu wake," aliagiza.

Alisema serikali imedhamiria kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ya afya ili kusogeza huduma muhimu za kijamii karibu na wananchi. Waziri Mkuu pia aliwataka wakuu wa idara katika halmashauri zote nchini wasimamie kikamilifu utekelezaji wa shughuli zote za maendeleo kwenye maeneo yao ili kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa miradi zinatumika ipasavyo.

"Haipendezi kuona viongozi wakuu waje na kubaini 'madudu' katika miradi wakati watendaji mpo. Kila mtumishi awajibike ipasavyo katika eneo lake ili kuhakikisha lengo la serikali la kuwaletea maendeleo wananchi linatimia," aliagiza.

Mradi wa ujenzi wa hospitali hiyo unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 7.5 na hadi sasa hospitali hiyo imepokea Sh. bilioni 4.2 kutoka serikali kuu ambapo majengo 20 yameshajengwa, majengo 13 yamekamilika, saba yako katika hatua za ukamilishaji. Hospitali itakapokamilika inatarajiwa kutoa huduma kwa zaidi ya watu 200,000.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange alisema serikali itaendelea kuiboresha sekta ya afya ikiwamo kununua magari mawili kwa halmashauri zote 184 nchini -- moja la wagonjwa na lingine kwa ajili ya usimamizi wa huduma za afya.

Akizungumza kuhusu ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Namtumbo, Dk. Dugange alisema watahakikisha wanasimamia maagizo yote yaliyotolewa na Waziri Mkuu ili kuhakikisha shule hiyo inakamilika kwa wakati na inaanza kudahili wanafunzi

Awali Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Christopher Wabarumi aliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha huduma za afya kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwamo wilaya hiyo ambayo inaendelea na ujenzi wa majengo ya 22 ya hospitali ya wilaya.

Wakati huo, Waziri Mkuu Majaliwa jana aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Dk. Samia Suluhu Hassan wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma.

Mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili kwa gharama ya Sh. bilioni nne kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP), awamu ya kwanza ilianza Aprili mwaka jana na inatarajiwa kukamilika Januari 30 mwaka huu, ikighaharimu Sh. bilioni tatu.

Shule hiyo itakapokamilila itapokea wanafunzi 1,080 ambapo awamu ya kwanza itapokea wanafunzi 600.

Awamu ya kwanza ya mradi huo imehusisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwamo mabweni matano, bwalo, vyumba 12 vya madarasa, jengo la utawala, nyumba ya mwalimu, mfumo wa maji safi na maji taka, vyoo matundu 16, uzio, kichomea taka, chumba cha jenereta na njia za kutembelea.

Awamu ya pili ambayo ujenzi wake unatarajiwa kuanza ndani ya mwaka huu kwa gharama ya Sh. bilioni moja, itahusisha ujenzi wa madarasa 10 yenye ofisi za walimu tatu, chumba cha ICT, maktaba, nyumba nne za walimu na mabweni manne.

Majaliwa alisema serikali imeamua kuwekeza kwenye elimu ya mtoto wa kike kwa kujenga shule za wasichana nchi nzima ili kumpunguzia changamoto zilizokuwa zikimkabili.

Waziri Mkuu aliwataka makandarasi wanaojenga shule hiyo kuhakikisha wanakamilisha ujenzi huo kwa muda uliopangwa ili waanze kupokea wanafunzi.

Shule ya Sekondari Dk. Samia Suluhu Hassan inatarajiwa kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano Julai mwaka huu.

# Kampuni yadai zuio dhidi yake huduma uwanja wa ndege batili

**Na Grace Gurisha**

KAMPUNI ya Transworld Aviation ya Zanzibar imedai katazo lililotolewa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) la kuwazuia kutoa huduma kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Aman Abeid Karume (Terminal 3) ni batili kwa kuwa limekiuka makubaliano ya mkataba wao.

Mkurugenzi wa Sheria na Uwekezaji wa kampuni hiyo ya Falme za Kiarabu aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kutokana na zuio hilo lililotolewa na ZAA Septemba 14 mwaka jana.

Madeleka alidai ZAA iliwapa taarifa kuwa hawapaswi kuendelea kutoa huduma zao kwenye uwanja huo eneo la Terminal 3 kuanzia Desemba Mosi mwaka jana bila kuwaeleza sababu ya mamlaka kufanya hivyo.

"Zuio hili kwenu ni katazo haramu ambalo linakiuka makubaliano na masharti yaliyopo kwenye mkataba huo ambao ni baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Transworld ambao unazungumzia uwanja wote na kuhusu terminal.

"Kampuni hii ni ya kimataifa, inayo sifa ya kufanya kazi kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Aman Abeid Karume na baadhi ya kampuni tunazofanya ni Fly Dubai, Eurowings ya Ujerumani, Air France na KLM ya Uholanzi," alisema Madeleka.

Alisema kuwa walitarajia kupewa taarifa ili wakae chini wazungumze kama mkataba unavyozungumza, lakini kama wanataka kuvunja mkataba baina yao, basi wafuate utaratibu ili wawalipe wanachostahili.

Alidai kampuni hiyo imewekeza takribani dola za Marekani milioni nne katika utoaji wa huduma kwenye kiwanja hicho na pia wamekuwa wakipata faida ambayo inaongezeka kila mwaka kutoka Sh. bilioni 1.7 kwa mwaka 2016 hadi kufikia Sh. bilioni 3.4 Novemba 2020.

Hata hivyo, akizungumzia suala hilo kwa njia ya simu, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa ZAA, Self Abdallah Juma, alisema malalamiko hayo hayana ukweli wowote.

## HABARI KITAIFA

# Raia Iran nchini waadhimisha miaka mitatu mauaji ya Jenerali Soleimani

**Na Kulwa Mzee**

RAIA wa Iran nchini wamefanya kumbukizi ya mwaka wa tatu ya mauaji ya aliyekuwa Kamanda wa Kikosi cha Quds cha Jeshi la Walinzi wa Mapinduzi ya Kiislamu, Jenerali Qasem Soleimani yaliyofanywa na Marekani mwaka 2020.

Hafla hiyo ilifanyika jana kwenye ofisi za Kituo cha Utamaduni cha Irani na kuongozwa na Mkurugenzi wa Kituo hicho, Morteza Pirani.

Mkurugenzi huyo alikumbusha kuwa ilikuwa asubuhi ya Januari 3, 2020 wakati habari za kuuawa kwa mmoja kati ya makamanda wakuu wa mapambano dhidi ya ugaidi ilipotangazwa.

"Jenerali Qasem Soleimani aliuawa karibu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Baghdad, Iraq pamoja na baadhi ya wasaidizi wake, akiwamo Abu Mahdi al-Mohandes, Naibu Mkuu wa Harakati ya Wananchi wa Iraq ya al Hashdu al Shaabi.

"Mtazamo wa maadui ulikuwa kwamba kwa kumuua Jenerali Qasem Soleimani, itawezekana kusimamisha kasi ya kuendelea kupata nguvu kambi ya muqawama ndani ya nchi na katika ngazi ya eneo la Asia Magharibi.

"Kuuaa Kamanda Soleimani hakukusimamisha au kudhoofisha mapambano dhidi ya ubeberu na uzayuni, kinyume chake, siku mbili tu baada ya jinai hiyo, Bunge la Iraq liliidhinisha mpango wa kuwafukuza wanajeshi wa Marekani nchini humo na Januari 24 mamilioni ya Wairaqi walifanya maandamano ambayo yalikuwa hayajawahi kushuhudiwa nchini humo dhidi ya Marekani," alisema.

Aliongeza kuwa mapigano kati ya makundi ya muqawama na Jeshi la Marekani yaliongezeka na kuwa jambo la kila siku Iraq na Serikali ya Marekani ililazimika kuanza duru mpya ya mazungumzo na Serikali ya Baghdad kuhusu hali ya wanajeshi wake miezi mitano tu baada ya kuuawa shahidi Jenerali Soleimani, mazungumzo yaliyobadilisha kuwapo Jeshi la Merekani Iraqi kutoka hali 'vita' na kuwa na sifa ya 'ushauri'.

"Hata hivyo, kama Marekani ilikubali kushindwa Afghanistan na kuwaondoa wanajeshi wake kwa madhila nchini humo, hivi karibuni pia italazimika kuwaondoa wanajeshi wake wote Iraq," alisema.

Aliongeza kuwa hali hii inaashiria kwamba baada ya mauaji ya kigaidi ya Kamanda Soleimani, Asia Magharibi inaelekea kutoka kwenye ramani iliyokuwa imechorwa na Marekani.

# Minada ya madini ya vito mbioni kuanza

**Na Mwandishi Wetu,** KARATU

WAZIRI wa Madini, Dk. Doto Biteko amesema serikali iko mbioni kuanzisha upya minada ya madini ya vito ili kuleta wanunuzi wakubwa, wafanyabiashara na wachimbaji wa madini nchini.

Alibainisha hayo juzi wakati akizindua duka la utalii wa madini la Kampuni ya Tanzanite Experience eneo la Manyara Kibaoni wilayani Karatu mkoani Arusha.

Alisema kuwa kupitia mnada huo, Kampuni ya Tanzanite Experience kupitia duka la utalii wa madini itapata madini mengi kwa ajili ya kuendeleza kituo hicho na maeneo mengine anayoyafanyia kazi.

Dk. Biteko alisema kuwa kupitia kituo hicho kilichoKo kwenye ukanda wenye maeneo ya hifadhi, imekuwa ni sehemu kubwa ya kivutio cha utalii kwa wageni kutoka ndani na nje ya nchi.

"Madini ya tanzanite yamekuwa yakinunuliwa nchini kwa kiasi kikubwa na watalii wanaokuja kutembelea hifadhi zetu na kupitia wao madini haya yanaendelea kutangazwa duniani," alisema Dk. Biteko.

Aliongeza kuwa, Wizara ya Madini inapongeza uwekezaji huo ambao umefanywa kwa asilimia 100 na watanzania wakiunga juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan wakati akitangaza vivutio mbalimbali vilivyopo nchini kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour, ambapo utalii na madini ya Tanzanite ulikuwa miongoni wa vivutio hivyo.

Katika hatua nyingine, Dk. Biteko alisema wizara inahamasisha uwekezaji wa namna hiyo ambao unaunga mkono moja kwa moja jitihada zinazofanywa na serikali za kutangaza madini ya Tanzanite duniani hususan kwenye eneo la shughuli za uongezaji thamani.

"Duka hili linatarajia kuuza bidhaa mbalimbali za madini ya tanzanite ambazo kwa miaka mingi zimekuwa zikitengenezwa na kuuzwa nje ya nchi. Hii ni hatua kubwa ambayo nchi yetu inaendelea kuchukua katika kuhakikisha madini haya yanazalishwa hapa nchini," aliongeza Dk. Biteko.

Waziri huyo alitoa wito kwa watu wote ambao wana nia ya kuwekeza kwenye uchongaji na ukataji wa madini, kuwekeza kwenye uongezaji thamani wa madini ili madini hayo yawapatie ajira na kodi kubwa serikalini.

Mkurugenzi wa Tanzanite Experience, Hassinne Sajani alisema duka hilo limekuwa kivutio kikubwa kwa watanzania na watalii kutoka nje ya nchi ambao wananunua bidhaa za madini zilizopo.

Alibainisha kuwa kampuni hiyo imeajiri wafanyakazi 80 na zaidi ya asilimia 80 ni wakazi wa maeneo ya Manyara Kibaoni.

Aliahidi kuendelea kutangaza madini ya Tanzanite ambayo ni zawadi kwa Watanzania ili madini hayo yapande thamani duniani.

Meneja wa Tanzanite Experience, Junaid Khan alisema zaidi ya wageni 6,000 wamefika kutembelea Kampuni ya Tanzanite Experience.

Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Dadi Kolimba alisema biashara ya madini imefunguka wilayani hapa na kuongeza mapato na kueleza kuwa ameipongeza kampuni hiyo kwa kutoa ajira zaidi ya 80 kwa watanzania katika nafasi mbalimbali.


## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, t**unatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAIN | REGINA CHARLES KAJOLE | NYUMBA | ATHUMAN RAJABU JONGO | KILUNGULE-MBAGALA | 23/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | JAFARI ATHUMAN JARIBU | NYUMBA | RABIA SELEMANI NANKOKO | TABATA KIMANGA | 24/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | GODFREY LAURENT MMASI | NYUMBA | FATMA IBRAHIM MNALLY | CHARAMBE MBAGALA | 23/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | OMARY HUSSEIN MHANDO | NYUMBA | OMARY HUSSEIN MHANDO | MBONDOLE -MSONGOLA | 23/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ATHUMANI MBWANA KAWESA | NYUMBA YENEYE LESENI YA MAKAZI | ATHUMANI MBWANA KAWESA | TABATA-MSIMBAZI | 24/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | SEIF HAMAD NASSORO | NYUMBA YENEYE LESENI YA MAKAZI | SEIF HAMAD NASSORO | MBAGALA-KILUNGULE | 23/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ATUPELE LABAN MWAIJIBE | NYUMBA | DR.ATUPELE LABAN MWAIJIBE | KIPUNGUNI KIPAWA | 23/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | RAJABU IBRAHIM MBAMBWA | NYUMBA | RAJABU IBRAHIM MBAMBWA | KIJITONYAMA | 25/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | ZUHURA ISSA GARAHENGA | NYUMBA | AUGUSTINO JOHN SIMBA | PUGU KINYAMWEZI | 23/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | SAIDI AKILIMALI KALILWA | NYUMBA | SAIDI AKILIMALI KALILWA | MWASONGA KIGAMBONI | 13/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA ( MARUDIO) |
| MAIN | CHEX ENGINEERING LTD | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 110 KITALU '15' NA HATI NAMBA 69065 | CHEDIEL GASPER NSHANA | BUNJU-KINONDONI | 12/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA ( MARUDIO) |
| BUGURUNI | MHINA JOSEPH KWELLA | NYUMBA | MHINA JOSEPH KWELLA | PUGU STATION | 25/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | MATHAYO GABRIEL MJEMA | NYUMBA | MATHAYO GABRIEL MJEMA | TEGETA MIVUMONI | 24/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | NJOLE NZALA MWASILE | GARI MITSUBISHI ROSA T557 DUV | GETRUDA BORANI MWAMLIMA | MBEYA | 23/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | MPOKI BROWN MWAIPASI | NYUMBA (2) | MPOKI BROWN MWAIPASI | 1.GONGOLAMBOTO 2. KILUVYA | 24/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | ZAITUNI OMARY JUMA | NYUMBA | ZAITUNI OMARY JUMA | KIVULE MATEMBELE YA PILI | 23/01/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | NYUMBA | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | TANDALE | 24/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | MARY JOHN DEUS | NYUMBA | MARY JOHN DEUS | KIMARA TEMBONI | 25/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | MBAWALA ACADEMY | NYUMBA | RAMADHANI JUMANNE MBAWALA | CHAMAZI MSUFINI | 26/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | NYUMBA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | MBAGALA MWANAMTOTI | 27/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 24/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0715868000/0713237650/0762260787/0719974916**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

17219002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga nusu fainali Afrika isakwe kwa vitendo

**ZIKIWA** zimebakia siku nane ili kumalizika kwa dirisha dogo la usajili, timu za Simba na Yanga ambazo zinatarajia kushiriki hatua ya makundi ya mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), zinatakiwa kujiandaa na hatua hiyo muhimu.

Simba yenyewe itapeperusha bendera ya Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Yanga yenyewe itachuana kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Ili timu ifanye vizuri, inatakiwa kuhakikisha inarekebisha mapungufu yake na kuboresha kikosi baada ya kufanya tathmini iliyotokana na ripoti ya mechi zilizotangulia na michuano hiyo ya CAF au zile za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo kwa sasa imesimama kwa muda kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayofanyika huko Zanzibar.

Wekundu wa Msimbazi ambao msimu uliopita walitolewa kwenye hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho, wanatakiwa kujipanga zaidi ili kupata matokeo mazuri zaidi mwaka huu na kuacha kutinga nusu fainali au fainali kwa 'maneno'.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wao ndio walikuwa na muda mrefu hawajatinga hatua hiyo ya makundi, lakini hicho si kigezo cha wao kutosonga mbele kwenye michuano ya mwaka huu, kila timu inatakiwa kujiweka tayari na imara kukabiliana na ushindani uliopo katika hatua hiyo. Tunafahamu wawakilishi wetu watakutana na timu kutoka mataifa mengine ambayo yanashiriki ligi mbalimbali, hivyo wachezaji na makocha wanatakiwa kuanza kuzifanyia kazi changamoto walizokuwa nazo kwa vitendo na kipenga kitakapolia, basi kila kitu kiwe tayari.

Ni fahari kwa Watanzania hasa wadau wa soka kuona wawakilishi wao wanafika mbali katika mashindano hayo na kuacha kuwa wasindikizaji, na hii itakamilika pale ambapo maandalizi yatafanyika vyema na matunda yake yataonekana. Makocha na viongozi wa klabu hizo hawatakiwi kufanya maandalizi 'midomoni' na badala yake kuanza mapema kuwachunguza wapinzani wao na kuacha kusubiria ikibaki wiki moja au mbili ndio zinaanza kusaka video za wapinzani.

Mpira wa miguu wa sasa umebadilika, wawakilishi wetu kwa kushirikiana na mabosi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wanatakiwa kuanza kuandaa mazingira rafiki ili muda wa mechi utakapofika, kila timu itakuwa imejiweka tayari kukabiliana na ushindani kutoka kwa wapinzani wao.

Imezoeleka kuona timu zikiangalia hali ya hewa au kujiandaa kubeba vyakula na kwenda navyo ugenini, lakini wakasahau kufanya maandalizi ya safari ambayo kwa wakati fulani tumeshuhudia wachezaji makocha na wachezaji wakilalamikia uchovu uliotokana na kutumia muda mrefu angani au safarini.

Suala la kuepuka uchovu litamalizika endapo tu viongozi watakuwa wametafuta ndege maalumu za kukodi ili kufika mapema kituoni na kurejea nyumbani kumsubiri mpinzani au kupata muda mzuri wa kupumzika kuelekea mechi inayofuata ya Ligi Kuu Tanzania Bara au mashindano ya Kombe la FA. Hapa ndio suala la klabu kupata mwekezaji imara au wadhamini watakaofanikiwa mipango yote kufanyika kama ilivyotarajiwa, basi Tanzania nayo itaingia kwenye rekodi ya timu zake kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Afrika au taji la Kombe la Shirikisho Afrika kwa mara ya kwanza.

Kitu kingine muhimu ni kwa klabu kuwaandalia wachezaji wao mafunzo maalumu yatakayosimamiwa na wakufunzi wa waamuzi kwa ajili ya kuwakumbusha na kuwaelimisha mabadiliko ya kanuni, na kwa kufanya hivi kutawapa nyota wao ufahamu na kujiepusha kuonyesha kadi ambazo zinaepukika.

Kingine ni wachezaji kufahamu kujituma ni jukumu lao na wasiburi kupewa ahadi za bonasi kwa sababu kufanya vyema pia kutawasaidia nyota hao husika kujitangaza kwa timu za mataifa ya Ulaya ambao hutuma mawakala wake kufuatilia mashindano haya hasa kuanzia hatua ya makundi hadi fainali. Kama ambavyo Kocha mpya wa Simba, Robert Oliveira maarufu Robertinho, alivyosema hakuna kinachoshindikana kwa timu hiyo kufika nusu fainali au fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, endapo wachezaji watajituma na kuipa thamani ya nembo ya klabu wanayoitumikia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

### Hongera waamuzi Zanzibar, wateuliwe kuchezesha Bara

**MASHINDANO** ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea visiwani, Zanzibar yamekuwa ya kusisimua kutokana na mashabiki wa Tanzania wamekuwa wakiliongelea zaidi soka kuliko waamuzi.

Pia mashabiki wamekuwa wakizungumzia klabu za Zanzibar kama KMKM, KVZ na Mlandege, kwa namna zilivyowashangaza wadau wa mchezo huo kutokana na soka safi wanalocheza.

Mashabiki hasa wa upande wa Tanzania Bara hawakutarajia kushuhudia upinzani mkubwa ambao timu za Zanzibar zimekuwa zikiutoa tofauti na miaka ya nyuma zilipokuwa zikitolewa katika hatua za awali. Kuna wanaojiuliza kama ni soka la Zanzibar limekua au timu za Bara zimeshuka viwango. Lakini inavyoonekana ni soka la Zanzibar limekua, huku timu za Bara zilizokwenda Zanzibar zikiwa zimekariri zitacheza dhidi ya vibonde. Kinachotokea huko kila mtu anaona.

Bingwa mtetezi wa mashindano hayo, Simba tayari ameondolewa mapema baada ya kufungwa na Mlandege bao 1-0. Nilichopenda ni kuona mashabiki wa soka sasa wanazizungumzia timu na wachezaji wao.

Wanazungumzia mapungufu ya vikosi na wachezaji wao na wala si upande wa waamuzi. Huku kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, mashabiki muda mwingi huwazungumzia waamuzi badala ya soka lenyewe. Ni kwa sababu waamuzi wa Bara wanatia shaka kwenye uchezeshaji wao. Mpaka unashindwa kuelewa, hawajui kutafsiri sheria, waoga au wanafanya makusudi. Na kama ni makusudi, wanafanya hivyo kwa sababu ya mapenzi au rushwa?

Nimeangalia mpaka mechi za makundi zote za Kombe la Mapinduzi zimeisha sijaona kasoro kwenye uchezeshaji wa mechi kwa waamuzi wa Zanzibar.

Wamekuwa makini mno. Wanachezesha kwa mamlaka, hawana woga, hawaonekani hata chembe kama wanambeba mtu. Wanaruhusu soka la kutumia nguvu lakini si kucheza rafu. Hawana makosa mengi ya kibinadamu kama ya wenzao wa Bara. Na hata kama likitokea basi linakuwa la kawaida sana ambalo haliathiri matokeo ya mechi yenyewe.

Huku Bara mwamuzi akifanya kosa la kibinadamu, basi linafanyika katika tukio lenye kuchangia uamuzi wa mechi, anaweza kutoa penalti ambayo siyo au kushindwa kutoa penalti kwenye sehemu ambayo ilipaswa na mengine mengi kiasi cha kutia shaka.

Mimi nadhani imefika wakati sasa kwa sababu Tanzania ni moja, waamuzi kutoka Zanzibar wapewe nafasi ya kuchezesha baadhi ya mechi za Ligi Kuu Bara kama ilivyokuwa zamani.

Zamani miaka ya 1980 hadi 1990, waamuzi wa Zanzibar wakiwamo Hafidh Ally, Juma Ally David na wengineo walikuwa maarufu sana Bara kwa kuchezesha mechi nyingi za Ligi Kuu.

Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Bodi ya Ligi na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) zikae na kuangalia namna ya kukuza ushirikiano ikiwa ni pamoja na kubadilisha waamuzi, wa Bara waende kuchezesha Ligi ya Zanzibar na wa Zanzibar wachezeshe Bara kwa baadhi ya mechi za ligi zote mbili.

Hata kama hakuna kanuni hiyo, nadhani kwa msimu ujao urudishwe kanuni ya zamani ya kuwaruhusu waamuzi wa Zanzibar kuvuka maji na kuchezesha baadhi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, vilevile wenzao nao kwenda visiwani huko.

Kubadilishana kwa maofisa hao kunaweza kupata hata ukweli wa kuhusu baadhi ya waamuzi wa Bara wanaovurunda kubaini kana wana matatizo ya kutafsiri sheria au huwa wanafanya makusudi. Tukiona baadhi ya waamuzi wa Bara wanafanya madudu yale yale kwenye Ligi ya Zanzibar tutajua kweli wengi wao hawajui kutafsiri, lakini tukiona wanachezesha vyema sasa tutajua kumbe walikuwa wanafanya makusudi, labda kwa sababu zao wanazozijua na hapo hata TFF na Kamati ya Waamuzi watajua nini cha kufanya.

Binafsi nimefurahishwa sana na uchezeshaji wa waamuzi wa Zanzibar, kiasi inaonekana pamoja na kuzalisha vipaji vingi vya wachezaji wanaoonekana katika michuano hiyo inayoendelea, lakini pia hilo linakwenda sambamba na kuzalisha waamuzi ambao kama wataendelea hivyo watakuja kuipa sifa kubwa Tanzania.

Tumekuwa tukiwaona mashabiki wa soka kama ni watu wa kulalamikia waamuzi tu, lakini kwa hili linalotokea katika michuano ya Kombe la Mapinduzi ni wazi kwa sasa wengi wao wanajua soka, hata mwamuzi anapoboronga wanafahamu, ndiyo maana hadi sasa hatujasikia mashabiki waliwalalamikia waamuzi wa Zanzibar ambao kwenye mechi ya Azam FC dhidi ya Jamhuri walitoa penalti mbili katika mechi moja kitu ambacho ni aghalabu kwa marefa wa Bara ambao wakitoa moja, hawawezi kutoa tena nyingine hata kama ilistahili kutolewa.

# RC ataka sheria kuwabana wasiotunza miti

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameyaagiza mabaraza ya madiwani katika halmashauri zote mkoani hapa kutunga sheria ndogo zitakazowabana watu watakaoshindwa kutunza miti itakayopandwa kuanzia mwaka huu.

Akizungumza jana na viongozi wa taasisi mbalimbali na watumishi, alisema mkoa wa Singida umejiwekea lengo la kupanda miti milioni tatu kila mwaka, hivyo ili kuilinda isiharibike hakuna budi kuwa na sheria ndogo kwa kila halmashauri.

"Katika kulinda miti tutakayopanda ili iweze kukua, wenyeviti wa halmashauri ni vyema wakatumia mabaraza yao kutunga sheria ndogo ili ambaye atapandiwa miti isipokuwa tuweke adhabu za kutoza fedha au adhabu yoyote kadri madiwani watakavyokubaliana kwenye halmashauri yao," alisema.

Serukamba alisema zamani miti ilikuwa inapandwa lakini haikui kutokana na huharibiwa kwa sababu haikuwa na mwenyewe lakini kutungwa kwa sheria hizo, kutawafanya watu kufanya jitihada za kuilinda isiharibiwe na kuhakikisha inakua.

Alisema Januari 7, mwaka huu, Mkoa wa Singida utazindua rasmi upandaji miti katika eneo la viwanja vya Bombadia, Manispaa ya Singida na kila familia itapewa miti mitatu kwa ajili ya kuipanda katika mazingira ya nyumba.

"Kila atakayepewa miti aitunze hadi ikue, serikali, watu binafsi, taasisi dini tushirikiane kufanikisha jambo hili tusingependa kutumia mgambo wakati jambo hili tunaweza kulifanya kwa hiari," alisema.

Aidha, Serukamba alisema kutatungwa sheria ndogo kwa ajili ya kusimamia usafi wa mazingira kwenye miji kwani ni jambo jema watu kuishi katika mji ambao ni msafi.

"Viongozi wa dini tusaidiane kuelimisha watu wetu, hili halihitaji bajeti wala kulipa chochote, tutakuelezea miti uipande na uhakikishe inakua," alisema.

Serukamba alisema leo watu wanalalamika mvua kutonyesha kwa kiwango kinachotakiwa lakini haya yote yametokana na uharibifu wa mazingira na watu kukata miti ovyo.



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (wa pili kushoto) alipotembelea eneo la Mradi wa Maji wa Mugango-Kiabakari-Butiama. Kutoka kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Khalfan Haule akifuatiwa na Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo. **PICHA: MOHAMED SAIF**

# Tathmini yafanywa vyanzo mapato halmashauri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Sera na Mipango Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), John Cheyo, amesema serikali imeanza kufanya tathmini ya vyanzo vya mapato kwenye halmashauri zote nchini.

Amesema lengo la tathmini hiyo ni kubaini fursa zilizopo na kuweka mikakati ya kukusanya kitaalamu ili kuongeza mapato.

Cheyo aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha tathmini ya mapato kwa halmashauri za mkoa wa Dodoma kinachoendelea jijini hapo.

Alisema kwa kipindi kirefu, halmashauri nyingi zinakusanya mapato kwa mazoea ndiyo maana wameona wafanye tathmini hiyo mapema kwa pamoja kuangalia fursa zilizoko katika kila eneo na kuweka bajeti ambayo ni halisia kutokana na takwimu za vyanzo vya mapato.

"Ili mkurugenzi wa halmshauri awe bora anatakiwa awe na sifa ya ukusanyaji mapato na ili aweze kufanya matumizi anatakiwa kukusanya kwanza, hivyo tunajipanga katika eneo hili ili huko mbeleni tuweze kuongeza mapato maradufu kwenye halmashauri zetu nchini," alisema.

Pia alisema ukusanyaji wa mapato unategemea takwimu sahihi, hivyo kwa tathmini hiyo, watapitia chanzo kwa chanzo na kukijadili kwa kina ili kujiridhisha kuwa wametafakari vya kutosha na kiwango cha ukusanyaji kilichowekwa ni halisi na kinaakisi takwimu zilizopo.

"Kuna mazoea yaliyojengeka katika kuandaa bajeti hasa kwenye mapato ya ndani ya halmashauri, unaweza kuta imepanga kukusanya Sh. milioni 100 kutoka chanzo cha leseni za biashara lakini ukichunguza kwa kina hawana takwimu sahihi za wafanyabiashara waliopo katika halmashauri zao.

"Huenda wamekaridia wale wa mjini tu au wale wakubwa lakini wafanya biashara wapo wengi na kiwango walichoweka kinaweza kuongezeka endapo kitafanyiwa tathmini ya kina.

"Kupitia tathmini hii, tunataka kuongeza bajeti ya makusanyo ya ndani ya halmashauri zetu kwenye bajeti inayokuja ya 2023/24 ili halmashauri ziweze kutekeleza miradi ya maendeleo na shughuli zingine zote za halmashauri husika bila vikwazo vya fedha," alisema

Meneja wa Mamalaka ya Mapato Tanzania (TRA) Halmashauri za Wilaya za Chemba na Kondoa, Mohammed Kapera, alisema tathmini hiyo itatoa fursa ya kuendelea kuongeza idadi ya walipa kodi.

Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu Mkoa wa Dodoma, Charles Mduma, alisema tathmini hiyo itasaidia halmashauri za mkoa wa Dodoma kupanga na kupata makisio halisi ya bajeti kwa mwaka 2023/24.

Alisema halmashauri hupanga makisio ya ukusanyaji ambayo si halisi na kusababisha kuomba kuongezewa vifungu vya bajeti hali ambayo inadhihirisha kuwa tathmini ya vyanzo vya mapato haikufanyika kikamilifu.

# Serikali kununua mahindi ya wakulima

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, ametangaza kuwa kuanzia Mei, mwaka huu, serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), itaanza kununua mahindi ya wakulima wa mkoa wa Rukwa kwa bei ya Sh. 500 kwa kilo moja.

Akizungumza na wadau wa kilimo wakati wa majumuisho ya ziara yake ya siku mbili mkoani hapa jana, alisema serikali itanunua mahindi kwa bei hiyo na kama kuna mfanyabiashara atakwenda kununua, naye atapaswa kuanzia bei hiyo na zaidi ili kulipa thamani zao hilo.

Bashe alisema miaka mingine serikali imekuwa ikianza kununua mahindi Agosti lakini msimu wa mavuno mwaka huu itaanza kununua mapema zaidi kwa kuwa imejenga maghala ya kisasa na mashine za kusafisha na kuyakausha mahindi badala ya kuyasubiri yakaukie shambani.

Alisema baadhi ya maeneo ya mkoani Rukwa, mahindi yananza kukomaa na kukauka Aprili, hivyo NFRA itayanunua na kuyakausha kisha kuyahifadhi kwenye maghala yao ili kumsaidia mkulima apate fedha haraka kwa ajili ya matumizi mengine ya maendeleo yake.

Waziri Bashe alisema pamoja na serikali kununua mahindi hayo, pia itaendelea kutoa vibali vya kuuza mahindi nje ya nchi ili mradi tu mkulima na mfanyabiashara wana uhakika wa soko zuri na afuate taratibu za serikali. Pia alisema serikali itaendelea kutafuta masomo ya uhakika ya mazao ya wakulima.

"Serikali yenu inapenda kuona mkulima ananufaika na mazao anayolima ndiyo maana imeweka ruzuku kwenye mbolea. Pia inawawezesha maofisa ugani ili wawape elimu, inawatafutia masoko lengo ni kuona maisha ya mkulima yanakuwa mazuri. Niwahakikishie kupitia kilimo safari hii maisha yenu yatabadilika,' alisema.

Mmoja wa wakulima aliyehudhuria kikao hicho, Mussa Pius, alisema kutokana na mikakati iliyowekwa na serikali na kumpata Waziri wa Kilimo anayeonekana ana nia ya kuendeleza kilimo kiwe cha kisasa, wanaamini watazifikia ndoto zao za kuwa na maisha bora kupitia kilimo.

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga, aliwataka wakulima kuzitumia mvua zinazoendelea mkoani hapa kuzalisha mazao mbalimbali ili mkoa uwe na chakula cha kutosha na mikoa mingine inufaike na kilimo kinachofanyika Rukwa.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akizungumza na viongozi wa Jiji la Dar es Salaam wakati wa kujadiliana juu ya mpango kabambe wa uendelezaji jiji hilo, jana katika ukumbi wa Jengo la Makao Makuu ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). **PICHA: WANMM.**

# Wizara yaonya watendaji dhidi ya ujenzi holela

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula amezitaka halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam kuandaa mipango ya kina na kutoa vibali vya ujenzi kulingana na Mpango Kabambe wa Jiji la Dar es Salaam 2016/2036.

Pia amewataka wananchi kutokufanya ujenzi wowote bila kuwa na kibali cha ujenzi.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa kikao kazi cha kujadili utelekezaji wa mpango huo pamoja na mkakati wa kukwamua mchakato wa urasimishaji makazi.

Waziri Mabula alizitaka taasisi ambazo ni watumiaji wa mpango huo ambazo ni Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA) na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kuhakikisha mipango yao ya kila mwaka pamoja na mambo mengine, inazingatia mpango huo ili kuuwezesha kutekelezwa kikamilifu kabla ya mwaka 2036.

Alitaja baadhi ya miradi iliyopendekezwa kuwa ni ujenzi wa viwanda maeneo ya Pugu, Pembamnazi, Kisarawe II na Kimbiji.

Mingine ni ujenzi wa barabara ya mzunguko kwenye Manispaa za Ilala na Ubungo; uboreshaji na uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi; uhifadhi wa maeneo ya kihistoria katikati ya jiji na mradi wa maji safi kwenye eneo la Kimbiji.

Mingine ni ujenzi wa dampo la kisasa kwenye maeneo ya Kisopwa na Lingato na ujenzi wa viwanda vidogo katika baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa urasimishaji.

"Ujenzi wa barabara za magari yaendayo kasi (BRT) katika awamu sita, ambapo awamu ya kwanza Kivukoni hadi Kimara na Magomeni - Morocco umekamilika, hatua ya pili ya ujenzi Mjini Kati hadi Mbagala bado unaendelea," alitaja.

Waziri Mabula alisema utekelezaji wa miradi unganishi iliyobainishwa katika mpango kabambe utabadilisha taswira ya Jiji la Dar es Salaam na kuboresha utoaji wa huduma kwa wakazi wa Jiji.

"Ninapenda kuelekeza Mamlaka zote zinazowajibika kutekeleza miradi hiyo, kutenga bajeti za utekelezaji wa miradi hiyo katika taasisi zao.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, ninaomba usimamie mpango huu ili fedha za serikali zilizotumika ziwe na tija katika utekelezaji wa miradi husika.

"Moja ya changamoto iliyopo ni kukosekana kwa uratibu mzuri na wa pamoja miongoni wa sekta mbalimbali zilizobainishwa kutekeleza miradi hii," alielekeza.

Waziri huyo pia aliagiza iundwe timu ya wataalamu itakayosimamia utekelezaji wa mpango huo na wajumbe wake watoke katika taasisi zote zinazowajibika kutekeleza miradi mbalimbali iliyobainishwa katika mpango.

Kuhusu urasimishaji makazi nchini, Waziri Mabula alisema sasa umefanyika kwenye mitaa 1,961 katika halmashauri 164 za mikoa yote 26.

"Katika mitaa hiyo, jumla ya viwanja 2,338,926 vimebuniwa kupitia michoro ya mipangomiji 7,051. Suala la upimaji nalo limefanyika kwa kiasi kikubwa ambapo jumla ya viwanja 1,170,639 vimepimwa na kuidhinishwa ambavyo ni sawa na asilimia 50.4 ya viwanja vyote vilivyopangwa," alifafanua.

Waziri huyo alisema viwanja 1,482,846 ambavyo ni sawa na asilimia 49.6, viko katika upimaji wa awali.

Kwa upande wa umilikishaji kupitia urasimishaji, Waziri Mabula alisema jumla ya ankara za umilikishaji 475,915 sawa na asilimia 20 zimetolewa kwa ajili ya wananchi kupata hati miliki ambapo hati miliki 177,330 sawa na asilimia nane zimeandaliwa na kukamilika katika viwanja vya miradi ya urasimishaji makazi nchini kote.

Alisema hadi mwezi Novemba 2022, wizara imebaini Sh. bilioni 70.288 zimekusanywa kama michango ya wananchi kwa ajili ya kugharamia miradi ya urasimishaji katika halmashauri mbalimbali huku Sh. bilioni 68.92 zikiwa zimetumika kufanya malipo ya kandarasi mbalimbali katika miradi husika.

"Katika tathmini iliyofanywa na wizara kwa nchi nzima, kati ya Julai hadi Novemba 2022, hadi sasa imebainika kuwapo kwa jumla ya mitaa 3,397 katika halmashauri 184 za mikoa yote 26 Tanzania Bara. Kati yake, mitaa 1,961 sawa na asilimia 57.7 imerasimishwa au inarasimishwa.

"Mitaa 1,436 sawa na asilimia 42.3 imebainika kuwa haina miradi ya urasimishaji yoyote inayotekelezwa. Katika jitihada za kukabiliana na tatizo la ongezeko la makazi yasiyopangwa nchini, wizara kupitia Programu ya Kuboresha Miliki za Ardhi inatarajia kurasimisha mitaa 559 kutoka halmashauri 34 za mikoa 15," alisema.

Waziri Mabula alisema kwa Mkoa wa Dar es Salaam, jumla ya mitaa 272 ya halmashauri tano mkoani humo inatekeleza miradi ya urasimishaji kutokana na kuwa na tatizo kubwa la makazi yasiyopangwa.

"Takribani asilimia 24 ya kazi zote za urasimishaji nchini zinafanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hadi sasa jumla ya viwanja 554,738 vimepangwa na kurasimishwa kupitia michoro 2,084 ya urasimishaji," alibainisha.

# Walia kero ya tembo tishio kwa maisha

**Na Christina Haule,**
MVOMERO

WAKAZI wa Kijiji cha Lubungo kata ya Mlali, Mvomero mkoani Morogoro wamesema pamoja na Serikali kuwapelekea huduma ya mradi wa maji wenye thamani Sh. milioni 400 , wameiomba serikali kusimamia suala la kuwaondoa tembo wanaozagaa kwenye eneo lao na kuharibu mazao, hivyo kuhatarisha uhai wao.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Kasoko Tokoyeti, amesema walikuwa wanakabiliwa na shida ya maji na kuyafuata maeneo ya mbali kwa baiskeli na wakati mwingine hulazimika kunywa maji ya madimbwi hasa nyakati za mvua kutokana na kushindwa kwenda kuchota maji kwenye chanzo kwa sababu ya uwapo wa tembo.

"Tunafurahi kupata maji. Ilikuwa shida yetu na tembo waliozidi yatatusaidiaje? Hatuwezi hata kulima mimi leo usiku nimepambana nao tembo nyumbani kwangu. Wamekula maembe, wamemaliza mazao yetu yote," alisema mwananchi jana.

Tokoyeti alisema wakazi wa kata hiyo hulima mahindi, mihogo, miwa na ndizi na hawana shida ya chakula muda wote lakini miaka mitatu mfululizo hawajalima baada ya tembo kula na kuharibu mazao yao, hivyo kukabiliwa na njaa.

Alisema adha ya tembo imekuwa ikiwalazimu wazazi kuwasindikiza watoto shuleni asubuhi kwa kuhofia kukutana na makundi ya tembo na kupata madhara.

Mbunge wa Mvomero, Jonas Van-Zeeland, alisema anafahamu changamoto ya tembo ambayo alishaiwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana bungeni jambo ambalo bado halijapatiwa ufumbuzi na kuendelea kuwatesa wananchi wa kata hiyo ambao hawawezi kujishughulisha na shughuli za kiuchumi kwa kuhofia tembo.

"Miezi kadhaa iliyopita usiku, nilipigiwa simu na mheshimiwa diwani. Nilikuja saa 4:00 usiku, nikakuta mtu amekanyagwa tumboni huwezi kumwangalia mara mbili. Sasa viongozi waliopewa dhamana wanafanya nini?

"Mimi mbunge, kazi yangu ni kusema, sina dola, sina chochote na ningekuwa na dola ningeweza kuwahamisha tembo. Watu wa TAWA (Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania) wawatoe wanyama wao," alisema.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara na wakazi wa kijiji hicho jana, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema ataziwasilisha salamu hizo kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, ambaye atafika na kutoa kauli kuhusu suala hilo.

Alisema wananchi wanapaswa kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa sababu wananchi wengi wananufaika na miradi ya maji iliyokwisha na inayoendelea kujengwa katika mikoa mbalimbali nchini na kuacha kutumia muda wao mwingi kutafuta maji na kuelekeza nguvu kwenye mambo ya uzalishaji.

"Sasa kinamama badala ya kupoteza muda mwingi kutafuta maji, mtautumia muda wenu katika shughuli za kukuza uchumi na baadaye kutulia na waume zenu majumbani mkipanga maisha. Maisha yatakuwa raha kabisa," alisema.

Aidha, alimpongeza Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mvomero, Sospeter Lutonjo, kwa kutekeleza majukumu yake vyema na kuwa mhandisi wa mfano sababu Wizara ya Maji ilikuwa ya kero na lawama na kwamba watu wanapewa pesa wakienda kukagua mradi haupo.

Mhandisi Lutonja alisema kukamilika kwa miradi mipya yenye thamani ya Sh. bilioni tisa inayojengwa kutawezesha kuongezeka upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Mvomero kwa asilimia 78 ifikapo Juni, mwaka huu.

Mhandisi Lutonjo alisema mpango wa RUWASA ni kufikia asilimia 85 ya utoaji wa hudumaa ifikapo Desemba, 2025 na hiyo ni kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 25.

Alisema mpango wa utekelezaji wa miradi kwa miaka mitatu ijayo 2023 hadi 2025 itawezesha kufikia vijiji 43 ambavyo vitakuwa vimebaki bila kuwa na huduma ya maji na kwamba miradi mbalimbali itaendelea kutekelezwa ili kufikia lengo la mwaka 2025.

# Madiwani, maofisa wanolewa utendaji

**Na Steven William,** MUHEZA

CHUO cha Serikali za Mitaa Hombolo, kimetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa uongozi madiwani, wakuu wa idara na vitengo wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga.

Mafunzo hayo yalianza kutolewa jana na yatafanyika kwa siku mbili katika ukumbi wa Korogwe Executive ulioko wilayani Korogwe mkoani Tanga. Mgeni rasmi katika mafunzo hayo, ni Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Basila Mwanukuzi.

Akifungua mafunzo hayo, mkuu huyo wa wilaya, amewataka viongozi hao kuzingatia mafunzo hayo kwa kuwa yatawasaidia kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia kanuni, sheria na taratibu za uongozi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina, alitumia fursa hiyo kushukuru kwa kupatiwa mafunzo hayo na madiwani wenzake na aliahidi kwenda kuyafanyia kazi.

Alisema madiwani wa halmashauri hiyo wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kusimamia miradi ya maendeleo hivyo ameishukuru serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha nyingi za miradi wilayani humo.

Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Desderia Haule, alisema mafunzo waliyopatiwa yatawajengea uwezo mkubwa katika uongozi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Muheza, Emigidius Kasunzu, alisema mafunzo waliyopata madiwani na wakuu wa idara wa halmashauri hiyo yatawajengea uwezo kuzingatia sheria,kanuni na utaratibu wa utumishi wa Umma.

# Shirika lazikomboa familia 514 kiuchumi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SHIRIKA lisilo la kiserikali la SOS Children Village, linalofanya shughuli zake katika Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru kupitia mradi wa uimarishaji familia ulioanza kutekelezwa mwaka 2007 kwa kata 11, limeziwezesha familia 514 kuimarika kiuchumi na kuimarisha ulinzi na usalama wa mtoto.

Mradi huo ulifikia tamati Desemba, mwaka jana, huku familia 346 zikiwa zinajitegemea kiuchumi kwa asilimia 86.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya kuhitimisha mradi huo iliyofanyika katika viwanja vya shirika hilo, kata ya Oltrumet, Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Arusha, Daniel Ngasikiwe, alisema kuna kila sababu ya kulipongeza shirika hilo kupitia mradi huo kwa kuwa umegusa maisha ya Watanzania wengi hasa waliokuwa na hali duni kiuchumi.

"Tunatambua dhahiri kuwa endapo hakutakuwa na uchumi imara ndani ya familia, vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake na watoto vitashamiri, hivyo SOS kupitia mradi huu, wamefanya jambo kubwa la kipekee kwa kuwa familia hizi zinajitegemea kiuchumi na tunaamini zitaenda kusaidia familia zingine ambazo hazikubahatika kuwapo kwenye mradi huu," alisema.

Mratibu wa Mradi wa SOS Children Village, Kaiza Sakafu, alisema wamekuwa wakifanya kazi na jamii za familia na watoto wenye umri wa kuanzia miaka sifuri mpaka 17 pamoja na vijana.

Alisema lengo la mradi huo ni kuwezesha familia na jamii kutoa ulinzi na usalama pamoja na kuwahudumia watoto kuhakikisha wanaishi katika mazingira mazuri na salama.

"Haikuwa kazi rahisi tunaamini kile ambacho tumesaidia watakithamini na kukitunza ili kuzisaidia familia zingine zinazowazunguka," aliongeza.

Hata hivyo, alitoa wito kwa wadau kuendelea kutoa ushirikiano ili miradi mingine kama hiyo iweze kufika kwa wananchi wengine zaidi kwa ajili ya kuleta mafanikio.

Wanufaika wa mradi huo, walishukuru shirika hilo na wadau walioshirikiana kwa kuwa mradi umekuwa na manufaa makubwa kwa kuwasaidia kujitegemea kiuchumi kwa kiasi kikubwa na kutoa malezi bora kwa familia.

"Kabla ya kukutana na shirika hili, nilikuwa mama wa nyumbani sikuweza kujikimu kwa kitu chochote. Lakini baada ya kujiunga na mradi huu mwaka 2020 sasa ninaweza kujikimu kimaisha pamoja na familia yangu. Kwa sasa ninajua kushona nguo za mitindo mbalimbali na tuna kikundi cha kinamama," alisema Zulfa Athuman kutoka kata ya Oloirien.



Mkurugenzi Mkuu wa TEMDO, Mhandisi ,Profesa Fredrick Kahimba akitoa maelezo ya namna taasisi yake inavyofanya kazi kwa Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Profesa Preksedis Ndomba pamoja na watu aliofuatana nao wakati walipotembelea taasisi hiyo kuona namna wanavyofanya kazi pamoja na kutia saini makubaliano ya taasisi hizo kufanya kazi kwa pamoja. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Viongozi wa dini wataka watoto wa kiume kuinuliwa kama wa kike

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

VIONGOZI wa dini Mkoa wa Arusha, wameishauri serikali kuwageukia na kuwatazama kwa karibu watoto wa kiume ambao wanaonekana kama wametengwa na kubaguliwa na jamii kwa kuwa hawapewi kipaumbele ikilinganishwa na watoto wa kike.

Akisoma tamko la viongozi hao jana mkoani humo, kwa niaba ya viongozi wenzake, Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mount Kilimanjaro, ambaye pia ni mwenyekiti wa viongozi hao, Dk. Stanley Hotay, alisema sasa hivi masuala ya watoto wa kiume hayazungumziwi sana kama ilivyokuwa kwa watoto kike.

"Hali hii imeleta athari hasi kwa watoto wa kiume ambao hata wanapokuwa shuleni hawana ujasiri wa kutosha ,hata wa kujieleza. Watoto wa kiume na wa kike wote watendewe haki sawa mbele ya jamii na taifa," alisema.

Alisema kila mtu akisimama na kuelekeza nguvu kubwa kama inavyoelekezwa kwa watoto wa kike, watoto wote watalindwa na hakuna atakayeachwa nyuma na mwisho wa siku taifa litakuwa na kizazi imara.


Dk. Hotay alisema viongozi hao wanapenda kusisitiza kwa serikali kuangalia umuhimu wa kuwapo kwa maadili kuanzia ngazi ya familia ili kuwalinda watoto wote ambao ni sawa bila kubagua jinsia moja na kupendelea jinsia nyingine.

Aidha, alisema utamaduni wa magharibi usiruhusiwe katika taifa la Tanzania, ikiwamo masuala ya ushoga na usagaji kwa kuwa hauna afya kwa nchi na kizazi cha sasa na kijacho.

Pia alihimiza kuendeleza juhudi za kuzuia na kupambana na rushwa na madawa ya kulevya ambayo yamekuwa yakisababisha athari kubwa kwa watu hasa vijana.

"Kwa upande wa mitaala ya elimu isifanyiwe mabadaliko ya mara kwa mara na ikitokea inafanyiwa basi wadau wote wahusishwe.

Tunatoa wito kwa watoa huduma wawe na utu na uzalendo pasipo kumwongezea maumivu mwananchi," alisema.





# Afungwa jela maisha kwa kunajisi mtoto

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela mkazi wa Kijiji cha Minjingu, Richard Gara(42) baada ya kupatikana na kosa la kumnajisi mtoto wa miaka 11 (jina linahifadhiwa).

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario, baada ya kumaliza kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili (upande wa mashtaka na upande wa mshtakiwa).

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kimario alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo Julai 2, mwaka jana, katika Kijiji cha Minjingu wilayani Babati.

Kimario alisema tukio hilo lilitokea baada ya mshtakiwa huyo kufika nyumbani kwa mtoto huyo na akaomba gunia la kwenda kupakia mkaa porini. Mshtakiwa, kwa mujibu wa Hakimu Kimaro, alikiuka Sheria ya Kanuni ya Adhabu kifungu cha 130(1)(2)(e) na 131(1), Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

"Ushahidi uliotolewa na binti aliyenajisiwa, ulidai kuwa mshtakiwa alimkuta mtoto huyo akiwa na kaka yake wanachunga ng'ombe na kumuomba aende kumsaidia kubeba mkaa," alisema Kimario.

Aidha, alisema shahidi huyo ambaye ndiyo mwathirika alidai mahakamani kuwa baada ya kufika kwenye mkaa alimnyonga kwa mikono na kumvua nguo kisha mbakaji huyo alishusha nguo yake ya ndani na kumfanyia kitendo hicho.

Hakimu alisema amemtia hatiani mshtakiwa baada ya kusikiliza mashahidi wanane wa upande wa mashtaka na vielelezo vinne vilivyofikishwa mahakamani hapo.

Vilevile alisema upande wa mshtakiwa alijitetea mwenyewe na hakuwa na shahidi mwingine.

Kadhalika, alisema hoja nyingine iliyomtia hatiani imetokana na ushahidi wa daktari aliyempima mtoto huyo na kuithibitishia mahakama hiyo kuwa mtoto alikuwa na maumivu makali, hivyo alimpatia dawa za kutuliza maumivu na dawa za kuzuia maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Alisema hoja nyingine ilikuwa ya mshtakiwa mwenyewe kwenye maelezo yake aliyoyatoa kituo cha Polisi muda mfupi baada ya tukio hilo alidai binti huyo alimwomba kwenda kumsaidia kubeba mkaa na wakiwa njiani alimwomba kuwa mpenzi wake ndipo aliamua kumwingizia uume wake.

Hakimu alisema kutokana na maelezo ya mshtakiwa huyo yameongeza nguvu kwa upande wa mashtaka na ushahidi kuthibitisha tukio kutendeka pasipo kuacha shaka.

Alisema shahidi wa tatu wa mashtaka ambaye ni kaka wa mtoto huyo, alikiri kuwa siku hiyo alikuwa na mdogo wake wakichunga ng'ombe Ziwa Manyara na mbakaji alikwenda kuomba msaada.

Kabla ya hukumu hiyo, Wakili wa Serikali, Grace Mgaya, alidai kwamba kwa kuwa mshtakiwa hana kumbukumbu za uhalifu mahakama itoe adhabu kali ili iwe fundisho wa jamii.

Mshtakiwa alipopewa nafasi ya kujitetea mahakamani,alidai kwamba ana watoto watatu na mama yake amezeeka na wanamtegemea hivyo anaomba apunguziwe adhabu.



Waziri wa Madini, Dk Doto Biteko akiwa ndani ya duka la utalii wa madini la kampuni ya Tanzanite Experience katika eneo la Manyara Kibaoni wilaya ya Karatu Mkoani Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msako kila nyumba wasiopeleka watoto shuleni

**Na Hamida Kamchalla,**
TANGA

MKUU wa Wilaya ya Tanga, Hashimu Mgandilwa, amesema Januari 9, mwaka huu, wataanza msako wa nyumba kwa nyumba kuwabaini wazazi ambao hawajawaandikisha watoto shuleni kuanzia ngazi ya awali na darasa la kwanza na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Mgandilwa aliyasema hayo jana alipokuwa akikagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Saruji na kusisitiza kuwa watoto ambao wanastahili kwenda shuleni waandikishwe na wale wanaotakiwa kuendelea na shule kwa ngazi ya shule ya msingi na sekondari waripotiwe shuleni mapema iwezekanavyo.

"Tunakagua ukamilishwaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa, lakini pia tutaangalia mchakato wa uandikishaji wa wanafunzi wanaotakiwa kuanza shule. Rais Samia Suluhu Hassan ametoa wigo wa elimu bure kwa hiyo mtoto yeyote mwenye umri wa kuwa shule anastahili kuwapo, kwa sekondari tumejitahidi kidogo kwa asilimia 65 ila kwa msingi bado tuna asilimia 50 hapa siyo nzuri sana.

"Niwatake wananchi wenye watoto wanaostahili kwenda shule wawapeleke kwa kuwa tunatarajia kuanza msako wa nyumba kwa nyumba na hatutaki kuwakamata kwa kutokuwapeleka shule wanao," alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, Spora Liana, alisema mchakato wa uandikishaji watoto bado unaendelea ingawa matarajio waliyojiwekea hawajayafikia.

"Tulikuwa na matarajio ya kuandikisha watoto wa shule za awali 6,417 lakini mpaka sasa hivi tumeandikisha wanafunzi 3,303 ambao ni sawa na asilimia 51 na kwa shule za msingi ilikuwa ni wanafunzi 9,397 mpaka sasa tumeandikisha wanafunzi 6097 sawa na asilimia 65, lengo letu ni kufikia asilimia 100.

"Lakini kwa shule za sekondari lengo lilikuwa ni wanafunzi 7997 shule zikifunguliwa tutajua idadi kamili ya wanafunzi watakao ripoti siku ya kufungua na tutaendelea kuwahamasisha wale ambao bado kupitia mikutano ya Mkuu wa Wilaya,' alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe, alisema shule zikifunguliwa atakuwa makini kufuatilia mahudhurio ya wanafunzi na atakayebainika kuwa mtoro mzazi au mlezi wake atachukiliwa hatua.

"Kuna ile desturi ya kusema mtoto kahamishiwa sehemu shule nyingine na ukifuatilia shule inayodaiwa amehamishiwa haukuti, kuanzia Januari 9, mwaka huu, nataka kuwaona wanafunzi darasani kwa kuwa hatutaelewana," alisema Mchembe.

Hata hivyo, alisema amepata taarifa kuwa wako baadhi ya wazazi na walezi waliowatafutia watoto kazi za ndani baada ya kuhitimu mitihani ya darasa la saba hivyo amewataka kuwarudisha haraka iwezekanavyo ili waende wakaripoti katika shule zao.

# Wananchi wapata mwanga kilimo umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WANANCHI wa kata za milimani katika jimbo la Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro, wanatarajia kunufaika na kilimo baada ya Mbunge wa Jimbo hilo, Prof. Patrick Ndakidemi, kutoa Sh. milioni 74 kwa ajili ya ukarabati wa mifereji ya asili.

Akizungumza jana katika kikao cha kawaida cha Kamati ya Maendeleo Mfuko wa Jimbo, Prof. Ndakidemi aliishukuru serikali kwa kumpatia Sh. 74,081,500 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika eneo hilo ikiwa ni fedha za mfuko wa jimbo.

Alisema kupitia fedha hizo, wamekubaliana na wajumbe zitumike kukarabati mifereji ya asili ili kuhakikisha wananchi ambao shughuli zao ni kilimo wanapata maji ya uhakika na kujinufaisha kupitia kilimo hicho.

"Fedha hizi zimekuja kwa wakati sahihi kwa kuwa kila kata itajipatia saruji mifuko 210 pamoja na Sh. milioni moja kwa mgawanyo ambao utakuwa Sh. Milioni 4.5 kwa kila kata kwa ajili ya kununua mchanga kukarabati mifereji yote ya asili kwa kuwa tunauhakika maji yakiwafikia wakulima watajikwamua kiuchumi," alisema Prof. Ndakidemi.

Alisema katika kata za Arusha Chini hawana mifereji ya asili fedha zake zitaelekezwa kwenye ujenzi wa ofisi ya Kijiji cha Chemchem huku kata ya Mabogini fedha zake zitapelekwa katika zahanati ya Mvuleni.

Mbunge huyo alisema mwaka wa fedha 2020/21, jimbo hilo lilipokea Sh. 49,767,000 lakini kutokana na Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka jana, imesababisha kuwapo na ongezeko la fedha hadi kufikia Sh. 74,081,500.

Hata hivyo, alitumia fursa hiyo kuwaomba watendaji wa serikali kusimamia vyema fedha hizo, ziweze kutumika kama zilivyokusudiwa na kuleta matokeo chanya.

Diwani wa Uru Mashariki, Samweli Materu, aliishukuru serikali kwa kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo kwa kuongeza fedha za maendeleo ambazo zimetokana na matokeo ya sensa na aliwataka Madiwani wa kata kuhakikisha wanasimamia fedha hizo.



## 'Anwani za makazi iwe ajenda yetu ya kudumu'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKURUGENZI Msaidizi wa Utawala wa Mawasiliano Wizara ya Habari, Mawasilinao na Tekonolijia ya Habari amezitaka wizara, taasisi za serikali na jamii kuhakikisha suala anwani za makazi linakuwa ajenda ya kudumu ili kufanikisha azma ya serikali kuifikia Tanzania ya kidijitali.

Suleiman Mvunye alitoa rai hiyo jana jijini hapo kwenye kikao kazi cha wataalamu wa wizara na taasisi za serikali kuhusu kujenga uelewa na kujadili namna bora ya kutekeleza maagizo ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu mfumo wa anwani za makazi nchini.

Alisema suala la anwani za makazi linapaswa kueleweka kuwa taarifa ya msingi katika kutoa na kupokea huduma na bidhaa.

Alisema utekelezaji wa mfumo huo wa anwani za makazi unapaswa kutekelezwa kwa wakati ili kutambua wananchi wanaowahudumia na kuchochoea maendeleo.

"Sisi kama wizara, ni wasimamizi kwa niaba ya serikali, hivyo ni jukumu la kila mmoja wetu kufanya kazi kwa uadilifu kuhakikisha kazi hii inafanikiwa kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuondoa changamoto zote zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wake, hatua ambayo itaimarisha usalama na utambuzi wa watu," alisema.

Aliongeza kuwa baada ya kikao hicho, wizara inatarajia utekelezaji wa kina kuanza mara moja kwa kuzingatia uendelezaji wa mfumo wa anwani za makazi ambao unazingatia uhifadhi na kutunzwa na watu wote. "Kwa kufanya hivyo tutafanikiwa, sisi sote lazima tuungane kuhifadhi miundombinu yote hasa ikizingatiwa kuwa serikali imetumia gharama kubwa ya Sh. bilioni 28 katika kutekeleza mfumo huu unaohitajika kuwa endelevu kwa vizazi vijavyo, hivyo kila wizara inapaswa kuwa mbele kuwezesha mfumo huu kwa kushirikiana na kuhamasisha wananchi," alisisitiza.

Akitoa maelekezo kuhusu utekelezaji wa maelekezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mratibu wa Anwani za Makazi Kitaifa, Jampyon Mbugi alisema taasisi zote zinapaswa kuhakikisha taarifa ya anwani za makazi inakuwa taarifa ya msingi wakati wa kutoa na kupokea huduma kwa kujumuisha mifumo ya kielekroniki.

# Upinzani walipa angalizo Jeshi la Polisi rukhsa mikutano siasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADA ya Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza kuondoa zuio la muda mrefu la mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa nchini, viongozi wa vyama vya siasa Mkoa wa Dodoma wamelitaka Jeshi la Polisi kutokuwa kikwazo kwao.

Viongozi wa vyama vya siasa mkoani hapa walitoa rai hiyo jana jijini wakati wa kikao cha pamoja na mkuu wa mkoa huo kilicholenga kujadili utekelezaji wa uamuzi huo wa serikali.

Kamishna wa chama cha NCCR Mageuzi Mkoa wa Dodoma, Meshack Masinga alisema kuwa licha ya serikali kuondoa zuio hilo lililodumu kwa takribani miaka saba, wanalitaka jeshi hilo kuweka usawa kwa vyama vyote nchini.

"Moja ya changamoto ambayo sisi vyama vya upinzani tumekuwa tukikabiliana nayo ni Jeshi la Polisi kushindwa kuweka usawa katika vyama vya siasa na kupendelea chama kilichopo madarakani, hivyo tunaomba agizo hili la Rais lifanyiwe kazi kwa vyama vyote kuwepewa uwanja sawa wa kisiasa," alisema.

Kamishna huyo alisema vyama vya upinzani ni kioo cha chama kilicho madarakani kutokana na kukosoa pale penye maslahi mapana ya taifa.

"Sisi ni wapinzani siyo maadui wa nchi, tunaomba tupewe uwanja sawa wa kisiasa kwa kuwa CCM haijapangiwa kutawala nchi hii maisha, kuna nchi wapinzani wameingia madarakani baada ya miaka 200, hivyo hata sisi ipo siku tutaingia na ninyi CCM mtakuwa chama pinzani," alisisitiza.

Alisema moja ya kero wanazokabiliana nazo ni Jeshi la Polisi kuwasumbua katika mikutano yao hata pale wanapokuwa na vibali. "Mheshimiwa RPC (Kamanda wa Polisi Mkoa), vijana wako wana tabia ya kututisha kwenye mikutano, unakuta mkutano unaendelea wao wanazunguka badala ya kutoa ulinzi," alisema Masinga.

Alibainisha kuwa NCCR Mageuzi haitakuwa tayari kumfumbia macho mtu yeyote ambaye atavunja sheria ya vyama vya siasa nchini.

Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Martin Otieno alisema jeshi hilo halitakuwa kikwazo kwa chama chochote, bali litatoa ushirikiano kwa kila chama bila kujali ukubwa wake. "Tutatoa ushirikiano, vibali na ulinzi kwa chama chochote ambacho kitahitaji kufanya mkutano wake wa hadhara, kinachotakiwa ni kufuata na kuzingatia sheria za nchi," alisisitiza.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa, Donard Mejeti alisema chama hicho mkoani hapa kitahakikisha kinafanya siasa za kistarabu.

"Kama mlivyosema, ninyi kweli ni kioo chetu, sisi tunajisifia tu lakini ninyi ndiyo mnaweza kutukosoa, hivyo ninawahakikishieni kuwa CCM Mkoa wa Dodoma tutafanya siasa za kistarabu," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule aliwaagiza viongozi wote ambao wapo chini yake kuhakikisha wanazingatia na kuyatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na Rais Samia.



Daraja la soko kuu la Majengo, Jijini Dodoma linalounganisha upande moja na mwingine ndani ya soko hilo limekuwa likitumiwa vibaya na baadhi ya wafanyabiashara kwa kufunga njia hiyo na kusababisha wateja kuzunguka kwa kutumia njia ya nje ya soko hilo kama walivyokutwa jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yashtuka kuhitimu la VII bila kujua kusoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imewataka viongozi wanaosimamia elimu katika Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa, kujitathmini na kufuatilia mwenendo wa watoto wanaomaliza elimu ya msingi ili kuhakikisha wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dk. Charles Msonde aliagiza hayo juzi wakati wa kikao kazi cha Maofisa Elimu wa Mikoa, Wilaya, Taaluma na Watu Wazima kilichofanyika jijini hapa.

Alisema kuwa kutokana na baadhi ya viongozi kusahau majukumu yao kwa kutowafuatilia walimu sehemu zao za kazi na kushindwa kufanya kazi kwa waledi, wanasababisha kutokuwapo ufanisi katika kazi.

Dk. Msonde alisema matokeo yake kusababisha kutopatikana kwa elimu bora na watoto kumaliza elimu ya msingi bila kujua kusoma, kuhesabu na kuandika.

Aliwataka viongozi hao kutokubali kukabidhiwa watoto kuanzia darasa la awali kutoka kwa wazazi/walezi na kisha mtoto huyo amalize darasa la saba akiwa hajui KKK.

"Hilo halitakubalika! Baadhi ya watu waharibu mipango na malengo ya serikali, haiwezekani mtoto anamaliza darasa la saba hawezi kusoma, kuhesabu na kuandika. Ingelikuwa ni mtoto wako kama mzazi utajisikiaje? Kama kiongozi uliyepewa dhamana ikitokea hivyo, maanake jitathmini hutoshi," alionya.

Dk. Msonde aliwataka maofisa elimu hao kutojikweza kwa uongozi na madaraka kwa kuwa si lengo la serikali, bali lengo ni kwenda kushirikiana na walimu kwa kuwafuatilia na kujua kero kwa pamoja na kuzipatia ufumbuzi na siyo kuwakatisha tamaa walimu.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kujenga na kuboresha elimu nchini pamoja na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Alisema kuwa kutokana na hali hiyo, mwezi huu watoto wengi wataingia shuleni na kwamba fedha zilizotolewa za ujenzi wa madarasa 8,000 zimetumika vizuri, yakiwa yamekamilika kwa asilimia 96.

"Tuna walimu wazuri wakihamasishwa kwa kupewa motisha, ari na hamasa ya kufanya kazi, tutakuwa na taifa bora kwa sababu wataalamu wetu wengi wanatokana na walimu," alisisitiza Dk. Msonde.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama aliwataka viongozi hao kusimamia misingi ya utumishi wa walimu katika kuwafuatilia maadili na utekelezaji wa majukumu yao ikiwamo suala la ufuatiliaji wa utoro wa walimu.

"Utoro huo unazorotesha elimu na kama walimu watakuwa vizuri kwa kutekeleza kwa ufanisi, waledi na ubunifu tutakuwa na watu wenye elimu bora nchini," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Vicent Kayombo alitoa rai kwa viongozi hao kwenda kuyasimamia na kuyatekeleza maelekezo waliyopangiwa na viongozi hao kwa kuwa wameaminiwa na ni jukumu lao kuleta mabadiliko ya elimu kwa maslahi ya taifa.





# Serikali: Tumejizatiti kupeleka umeme vijijini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imewataka wadau wa sekta ya elimu kujiweka tayari kwa matumizi ya mitaala mipya ya masomo ya msingi na maandalizi inayotarajiwa kuanza kutumika mwakani.

Waziri wake, Lela Muhamed Mussa alitoa kauli hiyo jana wizarani kwake Mazizini Zanzibar alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu matumizi ya mitaala mipya ya elimu baada ya kufanyika marekebisho makubwa.

Alisema mitaala mipya ya elimu inayotarajiwa kutumika mwakani, imezingatia mahitaji ya elimu kwa wanafunzi kwenye mazingira tofauti, elimu ya vitendo ikipewa kipaumbele zaidi.

Alisema marekebisho hayo yamefanyika baada ya kujitokeza changamoto mbalimbali ikiwamo ufaulu usioridhisha kwa wanafunzi katika mitihani ya taifa ya kidatu ya nne.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inapenda kuwajulisha wadau wake katika sekta ya elimu ikiwamo shule binafsi kwamba mitaala mipya ya elimu inatarajiwa kutumika mwakani ambayo inakwenda na mahitaji ya elimu yaliyopo sasa kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kuwa na ufaulu mzuri," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Mwakheri Adam Ameir alisema mahitaji ya mitaala mipya ya elimu yamezingatia mahitaji ya elimu mjumuisho pamoja na upatikanaji wa vifaa vyake ikiwamo kuwapo shule zenye mahitaji hayo.

"Tumejipanga kuhakikisha tunaingia katika soko la ajira kwa mafanikio makubwa, mabadiliko ya mitaala ya elimu yamelenga kuimarisha elimu mjumuisho pamoja na kuwapo shule zenye mahitaji hayo," alisema.

# Rais mstaafu ataka Mapinduzi Zanzibar yalindwe na yaenziwe

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume amesema Mapinduzi ya Zanzibar yana mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi, hivyo ni vyema yakalindwa na kuenziwa.

Dk. Karume alitoa kauli hiyo juzi wakati akifungua Tamasha la Tisa la Biashara kwenye viwanja vya Maisara mjini Zanzibarm, akiwataka vijana kusimamia misingi ya mapinduzi hayo kwa maendeleo ya taifa.

Alisema vijana ndiyo taifa la baadaye, hivyo ni vyema kuyaenzi mapinduzi hayo kwa sababu kabla ya mapinduzi, wazanzibar waliishi kwa kubaguliwa.

Dk. Amani alisema mapinduzi siyo ugomvi, bali ni uhuru na hakuna mtu ambaye anamiliki mapinduzi hayo, hivyo kila mzanzibar yanamuhusu na anatakiwa atembee kifua mbele.

Aliwataka wazanzibar kuendeleza umoja na mshikamano uliopo, akiamini hatua hiyo itawezesha nchi yao kupata maendeleo kupitia mapinduzi yao waliyojikomboa mwaka 1964.

Akizungumzia tamasha hiyo, alisema ni mwendelezo wa kuenzi mazuri yaliyofanywa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Mzee Abeid Amani Karume baada ya mapinduzi ya mwaka 1964.

Dk. Amani aliunga mkono kaulimbiu ya tamasha hilo ya 'ushirikishwaji wa jinsia kwa maendeleo ya biashara' kuwa inakwenda sambamba na kauli za viongozi wakuu wa nchi.

Pia aliipongeza Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kufanikisha tamasha hilo ambalo limeshirikikisha wafanyabiashara na mashirika mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi na litasaidia kubadilishana ujuzi, maarifa na kuongeza mapato ya wananchi. Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Said Omar Shaaban alisema tamasha hilo linawakutanisha wafanyabiashara kutoka ndani na nje ya mipaka ya Tanzania kuonyesha bidhaa na huduma muhimu za biashara zinazozalishwa ndani ya nje ya nchi.

Alisema tamasha hilo ni sehemu ya utekelezaji wa mikakati ambayo serikali imejiwekea ya kuhamasisha na kuchochea shughuli za kiuchumi kwa wafanyabiashara na watoa huduma za aina zote nchini.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ali Khamis Juma alisema tamasha hilo limeanzishwa kwa ajili ya kuwaunganisha wafanyabiashara na wananchi wa Zanzibar kukutana na wenzao kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania na nje ya Tanzania.

Alisema tamasha hilo limekuwa na ufanisi tangu lilipoanzishwa mwaka 2014 ambapo kulikuwa na washiriki 109 na sasa tamasha hilo lina washiriki zaidi ya 400 wanaotoka ndani ya Zanzibar, Tanzania Bara, Uganda, Kenya, Misri, Ghana, Zambia na India.



Waziri wa Habari Vijana Utamaduni na Michezo Tabia Maulid Mwita akikata utepe kuashiria ufunguzi wa maegesho ya magari hafla iliyofanyika Michenzani Mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Bosi Tume ya Mipango apata dawa uhaba wa ajira nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mtendaji Tume ya Mipango Zanzibar, Dk. Rahma Salim Mahfoudh amesema sekta ya ubunifu ikiendelezwa na kuwekewa mikakati, ina mchango mkubwa katika utoaji wa ajira na kukuza uchumi wa nchi.

Alisema hayo jana wakati wa mashindano ya ubunifu yaliyofanyika kwenye viwanja vya Maisara katika Tamasha la Tisa la Biashara linaloendelea, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za kutimia miaka 59 ya Mapinduzi.

Alisema wabunifu hutumia mbinu na ujuzi wa kubuni vitu mbalimbali, zikiwamo mashine na mifumo ya TEHAMA, vitu ambavyo vina uwezo wa kutatua changamoto zinazotokana na uzalishaji na utoaji wa huduma.

Katibu Mtendaji huyo alisema ubunifu unachangia kukuza shughuli za uzalishaji, utoaji wa huduma, maendeleo ya viwanda, kuongeza ajira na kuleta ufanisi mpana katika biashara.

Dk. Rahma alisema kuwa licha ya kuwapo kasi kubwa ya vijana kubuni mambo mbalimbali, bado asilimia kubwa ya ubunifu wao unaishia njiani kutokana na kukosekana kwa mikakati ya kuendelezwa.

Akizungumzia mashindano hayo, Katibu Mtendaji huyo aliitaka wizara husika kuyaendeleza kwa kuwa yanasaidia kutanua wigo kwa vijana katika kubuni vitu vinavyorahisisha utoaji wa huduma.

Alitumia fursa hiyo kuzitaka taasisi zinazohusika na urasimishaji wa biashara, kuwasaidia wabunifu hao ili kuzirasimisha kazi zao zitumike kibiashara.

Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Ali Khamis Juma aliwataka wabunifu kutanua wigo na kuwa na uthubutu katika uzalishaji wa bidhaa zao ili kuleta faida.

Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA), Soud Said Ali alisema wameamua kufanya mashindano hayo kila mwaka ili kuwatambua wabunifu waliopo nchini na kuwaongeza ujuzi na uwezo wa kubuni vitu mbalimbali kwa ajili ya maendeleo.

Katika mashindano hayo, wabunifu 21 walishiriki. Kati yao, 17 walishinda wakiwamo 11 wa TEHAMA na wabunifu sita katika utengenezaji mashine.



## CHEGE

UKURASA 16





# WAMEJIACHIA KIMAHABA



YUKO WAPI ?

# MUHIDIN GURUMO-2

# Sauti ya radi inayounguruma, muasisi majina Msondo, Sikinde

**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita tulianza makala ya mwanamuziki nguli kabisa nchini Tanzania, aliyebuni mitindo ya bendi mbili zilizotokea kuwa hasimu nchini Tanzania, Msondo Ngoma Music na Mlimani Park Orchestra ambazo alizipitia, akazifanyia kazi na kuziongoza, leo tunaendelea kutiririka.

**Kuanza kwake rasmi muziki**

Mara nyingi anapozungumza Gurumo, historia yake inaanzia NUTA Jazz, lakini ukweli ni kwamba alianza muziki mwaka 1960 akiwa na miaka 20 tu kwenye bendi ya Kilimanjaro Chacha.

Mwenyewe alisema alirithi muziki kutoka kwa mama yake ambaye alikuwa akiimba kwenye vikundi vya ngoma za asili ya kizaramo.

"Mimi kuimba nilirithishwa na mama yangu, alikuwa anaimba kwenye vikundi vya ngoma ya asili ya kizaramo inaitwa 'Ndekule', wakati huo bado msichana," alisema mzee Gurumo wakati wa uhai wake.

Itakumbukwa kuwa alipoihama Sikinde mwaka 1985 na kwenda kujiunga na Orchestra Safari Sound ambayo ilikuwa imeondokewa na mwanamuziki Freddie Ndala Kasheba na mtindo wake wa 'Dukuduku', Gurumo aliuondoa mtindo huo na kuasisi mtindo wa 'Ndekule.' Kumbe ilikuwa ni jina la ngoma ya kikundi cha asili ambacho mama yake alikuwa akiimbia.

Hakukaa sana na bendi ya Kilimanjaro Chacha kwani miaka miwili baadaye 1962 akajiunga na Rufiji Jazz Band, nako pia ni kama alitia pua tu, mwaka mmoja baadaye akaenda bendi ya Kilwa Jazz.

Mwaka 1964 alikuwa mmoja kati ya waasisi wa bendi ya NUTA Jazz ambayo ilibuni mtindo wake wa 'Kiwelewele'.

Bendi hii ilikuwa inamilikiwa na Chama cha Wafanyakazi na ilikuwa inabadili majina yake kutokana na mabadiliko ya siasa na mfumo wa uendeshaji.



**Alivyoasisi jina la Msondo Ngoma**

Baada ya kutumia kwa muda mtindo wa 'Kiwelewele', Gurumo aliamua kuwaita wenzake na kuwaambia wabadilishe mtindo na yeye angetoa jina la mtindo wa bendi. Ndipo akawaambia kuanzia sasa bendi ya NUTA Jazz itatumia mtindo wa 'Msondo Ngoma', ikiwa ni ngoma ya asili ya kwao Uzaramuni.

Ngoma hiyo ni maarufu kwa kuwafunda watoto wa kike wanaingia ukubwani, maarufu kama wanawari.

Na kweli, walipoanza kutumia mtindo huo bendi ikaanza kupata umaarufu mkubwa, ikijipatia mashabiki kila kona si nchini tu, bali Ukanda wa Afrika Mashariki nzima.

Hiyo ilichagizwa pia kwa kutunga vibao vilivyozitetemesha bendi nyingi kama 'Nimechoka Kuwa Nawe', 'Nakwenda Kijiji Cha Ujamaa', TANU na AFRO Shirazi, 'Nakonda Kwa Mawazo', 'Nipeleke Kwa Baba', 'Mpenzi Nakukanya', 'Viva Frelimo', 'Magdalena', 'Nimuokoe Nani', 'Msondo wa NUTA', 'Pongezi kwa Wakulima', 'Kaka', 'Dada', 'Upekepeke Si Mwema','Asha Adabu Yako Mbaya', 'Amina', 'Dada Rehema' na nyingine nyingi.

Baada ya Vyama Vya Siasa TANU Tanzania Bara na AFRO Shirazi cha Visiwani kuungana na kuundwa kwa CCM wakati huo chama kikishika hatamu, bendi hiyo ilibadilisha jina na kuitwa JUWATA Jazz Band mwaka 1977. Hii ilitokana na bendi hiyo sasa kuwa mikononi mwa chama, chini ya moja ya jumuiya zake tano, yaani Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania. Na jina JUWATA lilitokana na kifupi cha maneno hayo.

Lakini mtindo wa bendi ukabaki pale pale 'Msondo Ngoma' kama ulivyoasisiwa na Gurumo mwenyewe.

Ni kipindi ambacho tayari bendi ilikuwa kwenye kilele cha mafanikio, ikiwa ni moja kati ya bendi kubwa na tishio nchini Tanzania.

Iliendelea kutoa vibao mbalimbali vilivyojizolea umaarufu kama 'Mpenzi Zarina', 'Nirudishe Kwetu', 'Mwana Acha Wizi', 'Josephina', 'Mwanaidi', 'Kaka Selemani', 'Dada Mariam' na nyingine nyingi.

**Inaendelea wiki ijayo....**

## UDAKU TU



# WAMEJIACHIA KIMAHABA

MWANZO ilikuwa kama mshtuko kwa mashabiki wa muziki nchini baada ya picha mbalimbali zenye utata kuwahusisha wanamuziki wa Bongo Fleva, Harmonize na mrembo Feza Kessy.

Hapo ndipo ukaibuka mjadala kwamba tayari Harmonize ameanzisha penzi zito na mrembo huyo baada ya kumbwaga Kajala Masanja hivi karibuni.

Wakati mjadala huo unashika kasi kwenye majukwaa mbalimbali ya kijamii, Harmonize aliachia video ngoma yake mpya inayoitwa 'Wote' ambayo ndani yake mrembo huyo amefanya kufuru kutokana na uigizaji wake.

Kama ni mara ya kwanza kuitazama video ya wimbo huo, itakupa hamu ya kuangalia tena na tena ili kudadisi ufundi uliofanyika katika uchukuaji picha.

Kimsingi Harmonize na Feza wamefanya mapinduzi mapya hasa kutokana na kila mmoja kuonekana yuko huru kufanya kile kinachotakiwa.

Hata hivyo, video hiyo inaongeza maswali zaidi kati ya wawili hao kama kile kinachoonekana kama kiliishia katika uchukuaji picha au kuna zaidi ya kazi hiyo.

Kinachoendelea kuwapa wasiwasi mashabiki wa muziki waliotazama kibao hicho ni pale Feza anapoonekana kuutawala vyema mwili wa Harmonize, kiasi ambacho isingewezekana kama hakuna kitu kingine nyuma ya pazia.

Mashabiki ni kama wameachwa njia panda na wanaendelea kusubiri kuona kama wawili hao wataishia katika kazi au kuonyesha mlango mwingine wa kimahaba.

## INSTA-TWITTER



@burudanitele





**@wahu**
Januari ikiwa mtu yeyote aliniambia kwamba ningemaliza 2022 kama mama wa watoto watatu ningesema huo ni utani wa kikatili. Waliniambia kuwa haiwezekani kupata ujauzito tena bila msaada wa matibabu. Nilikuwa najaribu kufanya amani na kuwa mama wa watoto wawili.

**Muhimu** kuchukua tahadhari Corona inaua. Mwenyezi Mungu atuepushie-**Yusuph Mlela.**





**@mauasama**
After Recording 8 bangers (baada ya kurekodi nyimbo kali nane).

**@zuchu**
Kama nisingekuwa mwanamuziki basi ningekuwa mwanasiasa, wakati nasoma chuo nilichagua kuwa mwanasiasa baada ya kuzunguka nchi mbalimbali duniani ikiwemo India.



BASI SAWA

## Chege atafuta jibu watu Watajisikiaje?



MSANII mkongwe wa Bongo Fleva, Chege amesema kundi la TNC limewashtua wengi baada ya ujio wake kuja na Albam.

Kundi hilo ambalo ni kifupi cha majina ya |Temba, Necha na Chege lipo chini ya mtayarishaji maarufu wa muziki P Funk majani.

Amesema Albam hiyo Utajisikiaje' ni kazi nzuri na tofauti itakayoleta changamoto kwa wanamuziki wengine.

"Albam Utajisikiaje ni kazi itakayoshtua wengi, hii ina maana kubwa sana kwetu kwani wale mahasimu sasa tumeungana na kufanya kitu pamoja, tunawauliza wale waliosema haitawezekana watajisikiaje," alihoji.

## Mc Pilipili kuwarudisha shule watoto walemavu

MCHEKESHAJI wa jukwaani, Emmanuel Mathias, maarufu kama Mc Pilipili, ameanzisha kampeni ya kuwarudisha shule watoto wanaoishi katika mazingira magumu.



Akizungumza na BT, Mc Pilipili, amesema ili kufanikisha mpango huo ameanzisha kampeni ya kuchangisha vifaa mbalimbali vya kuwawezesha kurudi shuleni watoto yatima wa Morogoro na Dodoma Vijijini.

"Nikiwa kama kijana mwenye nafasi nimeamua kuunga serikali mkono kwa kuhakikisha watoto yatima na walemavu wanarudi darasani, kuanzia sasa napokea chochote ulichonacho kama peni,penseli,daftari, mabegi, sare za shule na fedha taslimu," amesema Pilipili.



## MSIZWA AMKABILI DIAMOND

ALIYEKUWA shemeji wa Diamond Platnumz, ambaye alimuoa Asma, ameibuka na kudai kwamba Marioo ameanza kuwa tishio na ndio maana msanii huyo mkubwa ameanza kumsema vibaya.

Msizwa amesema kuwa sio kweli alichosema Diamond Platnumz kuwa Marioo ndio aliomba asainiwe WCB, bali wao ndio wanamuhitaji.

Amsema wakati Diamond Platnumz anaongea na Marioo kuhusu kumtaka ajiunge na lebo hiyo, yeye alikuwepo akiwamo Zembwela na Baba levo.

"Marioo amekuwa Mfalme na ndio maana anaongelewa. Diamond kumzungumzia alikuwa na lengo baya, kwanini aongee uongo? Amehoji Msizwa.



## Idris Sultan acha kumchokoza Harmonize

MCHEKESHAJI na mwigizaji wa Bongo Muvi, Idris Sultan, amempiga dongo Harmonize kuwa wanawake ambao ana uhusiano nao wa kimapenzi anawakuta gym wakifanya mazoezi.

Hivi karibuni kumeibuka minong'ono kwamba Harmonize anatoka kimapenzi na Feza Kessy ambaye amepamba video ya wimbo wake mpya 'Wote' siku chache baada ya kutengana na Kajala Masanja.

"Huwa anawakuta kwenye gym." Ameandika Sultan na kuibua mjadala kuhusu maana halisi ya kauli hiyo, huku watu wengi wakisema amempiga kijembe Harmonize kwamba wanawake wake anakutana nao kwenye nyumba za mazoezi.

FILAMU

## Wivu: Sumu ya mapenzi inayotembea

Na Adam Fungamwango

WAPO watu wanaodai wivu ni kinga ya mapenzi, lakini ukiingia kwa undani na kufanya uchunguzi mdogo tu utakutana na matokeo yatakwambia ni sumu ya mapenzi.

Wivu ni ubinafsi ambao maeneo mbalimbali, lakini kwenye mapenzi ni kwamba mtu anataka kummiliki mke, mume au mpenzi asishirikiane, kuongea na mtu wa jinsia nyingine, au kwenda sehemu yoyote ile mbali na mmiliki mwenyewe.

Ndoa au mapenzi ni maelewano na maridhiano, neno ambalo limetokana na neno ridhaa, au matakwa ya yeye mwenyewe.

Kama mapenzi yanatokana na neno hilo, basi wanandoa au wapenzi wanapaswa wawe na kitu kinaitwa uaminifu, kila mmoja akimuamini mwenzake na si kufuatana, kulindana kuoneana wivu unaosababisha hata kudhalilishana.

Mtunzi wa filamu ya 'Wivu' anaitahadharisha jamii kuwa mwisho wa wivu ni aibu na hasara. Akatengeneza dude moja lililochezwa na Fatuma Ahmad, Zubeda Simba, Abdallah Mbulahona, Sameer Seif, Peter Mtweve, Ramadhani Nassor.

Dullah anaishi na mkewe Dahuu. Lakini hawaishi vizuri. Dahuu hana raha kwenye ndoa yake. Mumewe ana wivu kupindukia. Unaweza kusema huyu ndiyo mwenyekiti wa wanaume wenye wivu nchini. Mkewe akienda dukani, sokoni sijui wapi, popote kule anafuata nyuma nyuma.

Ameshagombana na wauza mabucha, masoko na wauza maduka kwa kuongea na mkewe kwa dakika kadhaa. Ameshawapiga wengi hadi waendesha mkokoteni wa maji. Kisa ni wivu tu kwa mkewe. Hataki avae nguo nzuri. Akiitwa nyumbani kwao anapangiwa nguo ya kuvaa, hadi muda wa kurejea. Akirejea kitakachompata ni kipigo tu.

Tatizo pia ni kwamba Dullah, pamoja na wivu, lakini pia wivu wake umechanganyika na gubu na ubahili pia. Hamtunzi vema mkewe, akitaka kufanya biashara, jamaa anaona kama vile atachukuliwa mke. Kuna kipindi alifanya kazi ya saluni, akamsimamisha baada ya kwenda kumkuta anaongea na kijana ambaye alikuwa akimtuma amletee maji.

Yaani jamaa huyu anatumia muda mwingi kumfuatilia mkewe, kuchunguza nyendo zake na kumfuata nyuma nyuma kuliko kufanya kazi.

Kuchungwa kama mbuzi, kufuatwafuatwa, matunzo duni, kukamfanya Dahuu kushindwa kuishi naye na kuamua kurejea kwao.

Dullah anampenda sana mkewe, tatizo ni wivu. Anakwenda ukweni kumbembeleza. Kama alidhani wakwe zake hawajui tabia zake alikosea.




Mama mkwe akamzodoa na kumpasha, akimueleza kila kitu ambacho amekuwa akimfanyia binti yake. Dullah akaona aibu. Dahuu naye akakataa katakata kurejea nyumbani. Mama kwa hasira akamrudishia kiasi cha pesa za mahari ambazo ametoa.

Dullah akachukua pesa zake na kuondoka. Hakuwa na wakati mzuri tena. Alikuwa kama chizi. Siku chache baadaye akagongwa na bodaboda, akafariki dunia.

## WASANII NA MABODIGADI WAO BONGO

**Na Adam Fungamwango**

ZAMANI tulikuwa tunaona kwa wenzetu tu nje ya nchi, wasanii wakubwa wakitembea na walinzi. Nchini Tanzania miaka ya nyuma haikuwa hivyo. Lakini miaka inabadilika na maisha yanabadilika.

Kwa sasa nchini kuna baadhi ya wasanii wamekuwa wakilindwa mithili ya viongozi. Kuna baadhi ya wasanii wakishapata majina makubwa tu, utaona wanaanza kutembea na mabaunsa au walinzi wao binafsi.

Tabia hii kwa sasa imekuwa kubwa sana Bongo hasa kwa baadhi ya wasanii wanoona wamefika viwango fulani vya umaarufu, hivyo kuhitaji 'mabodigadi'.

Kwa baadhi ya watu imeonekana kuwa ni gumzo, vituko, vichekesho, majisifu, majigambo,usumbufu kwani wanaona hala hakuna umuhimu wa hilo. Wengine wanafanya kwa fasheni tu kwa sababu mtu fulani ana walinzi.

Ukweli ni kwamba kwa sasa nchini kuna baadhi ya wasanii ambao wamekuwa vipenzi vya mashabiki na umaarufu wao unawalazimisha kuwa na walinzi ili kumuepusha na hatari yoyote inayoweka kutokea kwenye safari zake za kibinafsi, kifamilia, misele yake ya kila siku, studio, kupiga picha za video au kutambulisha ngoma.

Kuna wakati mashabiki wanakuwa na furaha ya kupitiliza wanapowaona wasanii wanaowapenda, hivyo wanaweza kuwakumbatia kwa furaha, kuwang'ang'ania kiasi cha kusababisha usumbufu kwa msanii mwenyewe au kumdhuru.

Leo tutawaangalia wasanii wa Kibongo ambao kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali, ndiyo wanaoongoza kwa kulindwa au kwa ulinzi mkali kuliko wengine.

**5. Nandy**

Jina lake kamili ni Faustina Charles. Jina lake maarufu la kimuziki ni Nandy. Anatembea na 'mabodigadi' wawili ambao huambatana naye kila anakopita. Akienda kushuti video, kununua nguo au bidhaa, au kutambulisha ngoma ni lazima aambatane na mibaba hiyo iliyoshiba, yenye uwezo wa kufanya chochote inapoona bosi wao yupo kwenye hatari.

**4. Zuchu**

Kwa sasa hakuna mtu anayehoji uwezo wa msanii huyo wa kike ambaye ameibuka kwa kasi na kuwa staa kamili. Na hata umaarufu wake umekuwa wa juu sana kiasi sasa naye kuhitaji walinzi.


Anatembea na walinzi wawili waliotuna. Huwezi kumsogelea kwa karibu hadi upate ruhusa maalum.

**3.Rayvanny**

Huyu pia ni mmoja wa wasanii wanaoongoza kuwa na ulinzi mkali. Ila tofauti ni kwamba mabaunsa waomlinda Rayvanny wao hawavai suti. Kama kuanza waanze leo.

Wao wanavaa nguo za kawaida zozote zile wanazoona zinavaa kwa siku hizo au kwa sababu maalum.

**2. Harmonize**



Konde Boy yeye anatembea na 'mabodigadi' kama wanne hivi. Lakini mara nyingi sana wanakuwa watatu. Nadhani mmoja anakuwa amebaki kulinda nyumbani wakati mwingine. Mabaunsa wake mara zote wanaonekana kuwa makini mno. Huyu alianza kuwa na walinzi pale tu walipojiunga na WCB.

**1. Diamond Platinumz**

Huyu ndiye baba lao. Si kwenye muziki tu, bali hata kwenye ulinzi. Ana walinzi au 'mabodigadi' kila sehemu anapokanyaga. Analindwa kwa gharama kubwa kwa sababu kwa sasa ndiyo kioo kwa Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Mara nyingi anakuwa na walinzi wanne. Diamond ndiye msanii mwanzilishi wa kuwa na mabaunsa nchini.

BONGO FLEVA

# Black Market Records kutafuta wasanii Tanzania




SOKO la muziki wa Bongo Fleva, linazidi kukua kwa kasi na kuwavutia wamiliki wa lebo mbalimbali duniani.

Hivi karibuni kiongozi Mkuu wa lebo ya Black Market Records ya nchini Marekani, Cedric Singleton, amefanya ziara nchini kwa ajili ya kuangalia namna ya kuwekeza katika muziki.

Tayari lebo hiyo imefanya vyema katika nchi mbili za Afrika Mashariki na kusababisha baadhi ya wasanii kupata mafanikio makubwa.

Akiwa jijini Dar es Salaam, Singleton, amesema kwamba lengo la ziara yake ni kuimarisha uhusiano na wadau mbalimbali ambao wamekuwa wakifanya nae kazi na kuwainua wasanii wake.

"Nimekuja Dar es Salaam kuangalia namna ya kuwainua wasanii, pia nitapita kwenye nchi nyingine za Afrika Mashariki kama Kenya na Uganda ambako huko kuna wasanii wanaosimamiwa na Black Market Records," amesema Singleton.

Black Market Records, imejizolea umaarufu mkubwa baada ya kuwa nyuma ya mafanikio ya wasanii wengi nchini Kenya na Uganda na Tanzania inatarajia kuingia katika orodha hiyo mwaka huu.

Kwa upande wa meneja wa Black Market Records nchini Kenya, Paulah BMR, amesema wamefanikiwa kufanya kazi na wasanii wakubwa kama vile Exray

Mbuzi Gang, Boondocks Gang, Daddy Andre, Nina Roz na Vic West.

## BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**Orchestre Sikinde Original**

Bendi hii inajiandaa kuingia studio kurekodi nyimbo za albamu ya kwanza ambapo itafanya onyesho moja tu la kesho Jumapili katika ukumbi wa Nefaland Manzese Argentina.

**FM Academia**

Wiki hii watakuwa na onyesho moja tu litakalofanyika kesho katika ukumbi wa Target Mbezi Beach.

**Twanga Pepeta**

Leo Jumamosi wapo Kiduli Garden Magomeni, kesho Jumapili watakuwa ndani ya ukumbi wa Gwambina Lounge Chang'ombe.

**Kimokimo Band**

Kama kawaida yao wakiwa chini ya mwimbaji wa siku nyingi aliyepitia bendi mbalimbali, Khadija Kimobitel, kila Ijumaa huwa ndani ya ukumbi wa Mariot uliopo eneo la Extertanal jijini Dar es Salaam.

**Mjengoni Classic Band**

Ikiwa nyumbani kwake jijini Arusha, leo Jumamosi itafanya makamuzi ndani ya ukumbi wa Kokoriko Annex, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wake wa nyumbani wa Mjengoni Club Orasiti jijini humo.

**Town Classic Band**

Leo Jumamosi watafanya vitu vyao ndani ya ukumbi wa Mawasiliano Ubungo, kesho wapo ndani ya ukumbi wa Twist Lounge Tabata.

**Waluguru Original**

Bendi hii yenye maskani yake mjini Morogoro, leo Jumamosi itatoa burudani ndani ya ukumbi wa Terminal Pub Msamvu, kesho Jumapili itamalizia wikiendi katika ukumbi wa F2 Florida mjini humo.

Tukuyu Sound Band

Kama kawaida yao, kila Jumapili vijana wa bendi hii watamalizia wikiendi yao katika ukumbi wao wa nyumbani wa Mawasiliano Park, uliopo Ubungo kando ya Barabara ya Sam Nujoma.



# AMELEWA UMAARUFU

UMAARUFU umemlevya! Ndivyo mashabiki wa muziki nchini Nigeria wanavyosema katika maoni yao baada ya mwanamuziki maarufu Burna Boy, kufanya madudu katika tamasha lake.

Mwanamuziki huyo ambaye jina lake halisi Damini Ogulu, alifanya kwa mara kwanza tamasha lake la muziki jijini Logos, na kufanikiwa kujaza watu wengi kuliko siku za nyuma.

Hata hivyo, mashabiki wake hawakufurahishwa na jinsi alivyokuwa akifanya kabla na baada ya kupanda jukwaani.

Kwanza Burna Boy alichelewa kupanda jukwaani kwa zaidi ya saa saba, na alipopanda jukwaani alionekana kuwa na hasira kiasi ambacho alionekana akimpiga teke shabiki aliyekwenda kumshika.

Katika video iliyosambaa mtandaoni ameonekana Burna Boy akimpiga teke shabiki aliyejaribu kwenda kumgusa akiwa jukwaani.

Hata hivyo, Burna Boy mwenyewe alijitokeza na kuomba msamaha kwa kile kilichofanyika wakati wa tamasha hilo na kuahidi kutorudia tena katika matamasha yanayokuja.

Katika video hiyo shabiki huyo alionekana akianguka kutoka jukwaani baada ya kupigwa teke ambalo halikutarajiwa kutoka kwa msanii mkubwa kama yeye.

Burna Boy amekuwa msanii wa kwanza kujaza kumbi kubwa duniani kama Madison Square Garden ya Marekani, State Farm Arena ya Ufaransa.

Tamasha hilo lilianza kwa hasira za mashabiki baada ya kutakiwa kuanza saa 12.

Kulingana na vyanzo vingi, mwimbaji huyo anadai kuwa mashabiki wa Nigeria hawampendi kwa sababu walieneza uvumi wa uwongo kuhusu yeye si asili ya nchi hiyo.



# Yomi Gold avunja ndoa

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Yomi Alore, maarufu kama Yomi Gold, ametangaza kuachana na mke wake Meenah.

Katika chapisho lililoshirikiwa kupitia ukurasa wake wa Instagram, Gold amefichua kuwa waliamua kuachana kwa sababu mapenzi yalikuwa yamekufa katika uhusiano huo.

Kwa maneno yake aliandika, "mimi na Meenah tuliamua kwenda njia tofauti. Nataka familia zetu zote na marafiki, mashabiki waelewe. Huu sio wakati wa kumhukumu mtu mapenzi yanapokufa katika uhusiano,"



## Jeremy alazwa hospitali

JEREMY Renner, msanii wa muziki kutoka kundi la Marvel, yuko katika hali mbaya baada ya kufanyiwa upasuaji kutokana na ajali aliyoipata wakati akiondoa theluji nje ya nyumba yake.

Baada ya tukio hilo, msanii huyo alisafirishwa kwa ndege hadi hospitalini kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

Renner alipata jeraha eneo la kifuani na kupata ufa kwenye mifupa.

## Portable aibuka kituko kipya

MWANAMUZIKI mwenye utata kutoka Nigeria, safari hii amekuja na kituko cha aina yake, baada ya kuonekana akiwa peke yake ndani ya ndege wakati akisafiri kwenda nchini Benin.

Kupitia akaunti yake rasmi ya Instagram, mwimbaji huyo alirusha video mbalimbali akiwa ndani ya ndege ndogo huku viti vingine vikiwa vitupu.

Portable, ambaye alionekana kufurahishwa na hali hiyo alisikika akisema "Wahala Wahala Wahala, ndani ya ndege wanaona kiti tupu, lakini kwa watu wa nje mengi, hakuna pesa za kununua tiketi,"





## Shanty Town ndani ya Netflix

NETFLIX imetoa trela ya filamu mpya ya mapigano 'Shanty Town' ambayo inazungumzia magenge ya kihalifu nchini Nigeria.

Filamu hiyo ambayo imeandaliwa na waongozaji wawili Xavier Ighorodje na Chichi Nworah, itakuwa ni mwendelezo wa mradi wao wa sehemu sita.

Filamu hiyo ambayo inaelezea maisha ya waimbaji watatu wa Jimbo la Lagos, imechezwa na Ini Edo, Nse Ikpe-Etim na Nancy Isime.

Wasanii hao wanaungana kupigana vita dhidi ya kundi kubwa la uhalifu na katili katika jimbo hilo.

## Lala amtamani serengeti boy

MREMBO Lala Anthony wa Marekani, amerudia kusema kwamba anataka kumpata mwanaume mwenye miaka 22.

Lala mwenye umri unaopita miaka 40, amesema bado hajampata mwanaume mwenye umri huo na anaendelea kumtafuta.

Mwanamke huyo alikuwa kwenye uhusiano na Alex Cooper , lakini miezi michache iliyopita waliachana na kila mtu kuchukua njia yake.



MAKALA

# Wizara na mkakati kumaliza kero za ardhi

Na Munir Shemweta


Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula.

KWA muda mrefu kumekuwa na kilio cha migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini, iliyosababisha pia uvunjifu wa amani. Hatua hiyo ilisababisha serikali kuunda kamati ya mawaziri wa wizara za kisekta ili kupita na kuona namna ya kutatua migogoro hiyo.

Katika moja ya njia ambazo zimefanyika katika kumaliza migogoro hiyo ni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuridhia ardhi yenye ukubwa wa ekari 1,492,703 iliyokuwa sehemu ya maeneo ya hifadhi na maeneo ya umma, zikiwamo ranchi za serikali kumegwa na kurasimishwa kwa wananchi.

Aidha, mapori tengefu 12 yenye ukubwa ekari 707,962 na Hifadhi za Misitu 7 zenye ekari 46,715 nayo yamefutwa na ardhi hiyo kukabidhiwa kwa wananchi kupitia usimamizi wa serikali za mikoa katika kupanga na kuyapima maeneo hayo.

Hatua hiyo iliyofikiwa na Rais Samia, ilibainishwa wiki hii na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alipokuwa akizungumzia masuala mbalimbali ya sekta ya ardhi na mwelekeo wa utekelezaji wa wizara hiyo kwa kipindi cha kuanzia Januari, mwaka huu.

"Kamati ya Mawaziri wa Wizara za Kisekta imeielekeza mikoa kusimamia utekelezaji wa uamuzi wa Serikali kwenye maeneo yao yote yaliyoainishwa na kutolewa uamuzi," alisema Dk. Mabula.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, katika kuhakikisha masuala ya ardhi yanazingatiwa na kuepusha migogoro, miongoni mwa kazi zinazondelea kutekelezwa hivi sasa ni pamoja na uwekaji wa alama za mipaka baina ya maeneo ya hifadhi na maeneo ambayo serikali imeridhia yabaki kwa wananchi.

Hatua zingine ni upangaji na upimaji wa maeneo yaliyorejeshwa kwa wananchi, utambuzi, uhakiki na uthamini wa maeneo ambayo wananchi watatakiwa kupisha shughuli au maeneo yatakayotumika kwa matumizi ya umma na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

Waziri pia aliagiza kila mkoa kusimamia utekelezaji wa uamuzi wa serikali kuhusu masuala ya ardhi kama ilivyoelekezwa na kuhakikisha kazi zote zinakamilishwa ifikapo machi 30, mwaka huu.

**KODI YA PANGO**

Akizungumzia ulipaji kodi ya pango la ardhi hasa baada ya msamaha wa riba ya malimbikizo uliotolewa na Rais Samia kwa wananchi wenye malimbikizo kupewa nafuu ya kulipa deni la msingi ili wasamehewe riba ya malimbikizo, Waziri alisema kutokana na unafuu uliotolewa, wizara imekusanya Sh. 90,907,939,421 sawa na asilimia 75 ya lengo la nusu mwaka.

Hadi kufikia Novemba, 2022 wananchi 2,819 walinufaika na msamaha wa riba ya malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi yenye jumla ya Sh. 6,946,930,272. Idadi hiyo hajumuishi wananchi waliojitokeza ambao walihudumiwa kuanzia Desemba Mosi hadi 31, mwaka jana.

Kutokana na mafanikio hayo na mwitikio mkubwa, Waziri Mabula aliwashukuru na kuwapongeza wamiliki wa ardhi waliojitokeza kunufaika na msamaha uliotolewa. Katika mwezi Desemba, wizara ilishuhudia idadi kubwa ya wamiliki waliojitokeza kulipa na Sh. bilioni 22.6 zilizokusanywa katika kipindi hicho.

**KUKOMESHA MIGOGORO**

Akigeukia suala la utatuzi wa migogoro ya ardhi, Dk Mabula aliziitaka mamlaka za serikali za mitaa kusimamia kikamilifu mipango ya jumla, mipango kina na mipango ya matumizi ya ardhi vijijini kupitia kamati za ardhi za vijiji kudhibiti ujenzi uholela usiozingatia mipango iliyoandaliwa na kuidhinishwa kupitia kamati za mipangomiji.

"Wizara imekuwa ikipokea taarifa na malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu ukiukwaji wa taratibu mbalimbali zinazohusu usimamizi wa ardhi mijini na mijini. Miongoni mwa malalamiko ni baadhi ya viongozi wa vijiji na mitaa kuuza ardhi kinyume cha utaratibu.

"Pia malalamiko hayo yanatokana na kukosekana kwa udhibiti wa uendelezaji ardhi katika maeneo ya vijiji na miji. Hali hiyo imesababisha kuongezeka kwa migogoro ya ardhi na uendelezaji ardhi kinyume cha mipango iliyoandaliwa na kuidhinishwa,' alisema. Ili kupata mwafaka wa kudumu katika suala hilo, Dk.Mabula alisema wizara yake inaandaa programu maalum ya kufanya ukaguzi wa uzingatiaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa mamlaka za mpangaji.

"Taarifa hizi zitatolewa kwa umma kama sehemu ya uwajibikaji wa mamlaka zetu kwa wananchi," alisema.

**VITUO VYA MAFUTA**

Kumekuwa na taarifa ya ongezeko la ujenzi wa vituo vya mafuta jambo ambalo limesababisha kuibuka kwa wasiwasi wa usalama wa wananchi na mali zao katika maeneo ya jirani na vituo hivyo.

Kuhusu suala hilo, Dk. Mabula alisema hadi Desemba 31, mwaka jana, wizara ilipokea taarifa ya uendelezaji wa vituo vya mafuta kutoka halmashauri 129 kati ya 184 zilizoko nchini sawa na asilimia 70.1.

Alisema uchambuzi uliofanywa na wizara ulibaini kuwa katika halmashauri 129, kuna vituo 2,063 kati ya hivyo, vituo ni 1269 (asilimia 61.6) na vituo vidogo vya mafuta ni 794 (asimilia 38.5) huku vituo 1,868 vikiwa vimejengwa katika umbali wa zaidi ya mita 200 kutoka kituo kimoja na kingine sawa na asilimia 90.5 kama inavyoelekezwa na kanuni ya viwango vya umbali.

Pia alisema vituo 195 vimejengwa umbali wa chini ya mita 200 sawa na asilimia 9.5 na kwamba wizara inaendelea kufanya uchambuzi zaidi ili kubainisha vituo ambavyo vimejengwa kabla au baada ya kanuni za mwaka 2018 zinazoendelea kutumika ili hatua stahili zichukuliwe.

**URASMISHAJI MAKAZI**

Kuhusu programu ya miaka 10 ya urasimishaji makazi holela, alisema wizara inayo Programu ya Urasimishaji Makazi iliyoanza kutekelezwa mwaka 2013.

Programu hiyo mwisho wake ni mwaka huu na imekuwa ikitekelezwa katika mitaa 3,397 kwenye mikoa yote 26.

Katika utekelezaji wa programu hiyo, Dk. Mabula alisema mitaa 1,961 imerasimishwa sawa na asilimia 57.7 na mitaa 1,436 haijarasimishwa sawa na asilimia 42.3 na kubainisha kuwa programu hiyo imewezesha upangaji wa viwanja 2,338,926 na kati ya hivyo, viwanja 1,170,638 upimaji wake umekamilika. Aidha, jumla ya milki 177,330 zimeandaliwa na kutolewa kwa wananchi.

Hata hivyo, alisema katika kutekeleza programu hiyo, kumekuwapo na changamoto mbalimbali licha ya mafanikio yaliyopatikana na kuzitaja baadhi ya changamoto kuwa ni pamoja na uelewa mdogo wa wananchi juu ya umuhimu na namna urasimishaji unavyofanyika, baadhi ya wananchi kutokuwa tayari kuchangia ardhi inayohitajika kwa ajili ya miundombinu na matumizi ya umma.

Changamoto nyingine, kwa mujibu wa Waziri ni baadhi ya wananchi kutolipa gharama za urasimishaji kwa wakati hali inayosababisha baadhi ya kampuni kushindwa kumudu gharama za utekelezaji na baadhi ya kampuni za urasimishaji kutokamilisha kazi kwa wakati pamoja na kutumia wataalam wasiokuwa na sifa.

Hata hivyo, alisema kutokana na uwepo wa changamoto hizo, wizara imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha kazi za urasimishaji zinakamilika na hatua hizo ni pamoja na Wizara kwa kushirikiana na halmashauri, kukwamua baadhi ya kazi zilizokwama, kuchukua hatua kwa kampuni zilizoshindwa kutimiza wajibu wao ikiwa ni pamoja na kusimamisha au kufungia baadhi ya kampuni hizo, kuhusisha taasisi za kifedha katika miradi ya urasimishaji na kuandaa na kusambaza mwongozo wa urasimishaji ikiwemo kupunguza gharama za urasimishaji hadi kufikia Sh. 130,000 kwa kiwanja.

Pamoja na jitihada hizo, alisema wizara kwa kushirikiana na halmashauri na sekta binafsi inatekeleza programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi ili kuwa na miji nadhifu na iliyopangwa.

Kwa mujibu wa Waziri, matumizi ya programu hii, yatasaidia kupunguza mitaa isiyorasimishwa na kudhibiti kuendelea kukua kwa makazi yasiyopangwa. Pia baadhi ya mitaa ambayo haijarasimishwa, ipatayo 559, imeingizwa kwenye Mradi wa Uboreshaji Milki za Ardhi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na utekelezaji wake umeanza.

Sambamba na hilo, wizara imeandaa mkakati wa kushughulikia changamoto za urasimishaji baada ya kikao baina ya wataalam wa wizara na wadau wa urasimishaji kilichofanyika Desemba 22, mwaka jana.

MAKALA

# Makivuka chanzo kumaliza vita Ukraine?

## -Russia yashangaa, Marekani kicheko

**Na Mwandishi Wetu**

VITA kati ya Ukraine na Russia, imeingia katika sura mpya baada ya wanajeshi zaidi ya 89 kuawa kutokana na shambulio lililofanywa na Ukraine.

Pigo hilo ambalo halikutarajiwa, limeleta majuto kwa Warussia kiasi ambacho watu wameanza kulalamika kuhusu usalama wa watoto wao wanaopigana vita hiyo nchini Ukraine.

Wakati Russia imetoa orodha ya wanajeshi 89 waliouawa, jeshi la Ukraine linadai zaidi ya askari 400 wameuawa.



**NINI KILITOKEA?**

Kilichotokea Makivka bado kinawashangaza wengi na kujiuliza ilikuwaje lundo la askari wakauawa kwa mpigo?

Bado Russia haijapata jibu licha ya kuendelea kupata mshangao, huku ikizidi kutoa orodha mpya ya wanajeshi waliouawa kila wakati.

Nchi za Ulaya nazo zimepigwa butwaa kwa tukio hilo, huku Marekani ikionekana kufurahia kwa kile inachokiona msaada wake kwa Ukraine unafanya kazi kwa ufanisi.

Warusia wengi wanaona shambulio hilo ni kama uzembe wa wakuu wa kijeshi ambao walipewa jukumu la kusimamia kambi ya Makivka, iliyoko katika eneo la Donetsk, ambalo linakaliwa na Russia.

Inaelezwa wakati makombora yaliyorushwa na kikosi cha Ukraine, eneo hilo kulikuwa na idadi kubwa ya wanajeshi wa Russia.

Hata hivyo, Russia imeonekana kupuuza malalamiko ya uzembe wa baadhi ya majenerali wake, badala yake imesema shambulio lililotokea mwaka mpya lilitokana na matumizi mabaya ya simu janja ya mmoja wa askari.

Makombora hayo yaliteketeza kambi hiyo ambayo ni kama chuo cha kujiunga na jeshi majira ya saa sita usiku.

Matumizi ya simu zilizopigwa marufuku, na matumizi yake yaliruhusu adui kupata shabaha yake.

Ingawa idadi ya watu waliouawa haijathibitishwa, ni idadi kubwa zaidi ya vifo vinavyotambuliwa na Russia katika vita hivyo.

Ukraine inadai idadi hiyo ni kubwa zaidi, ikisema wanajeshi 400 waliuawa katika shambulio hilo na wengine 300 kujeruhiwa.

Russia inakiri kwamba katika siku ya mwaka mpya, roketi sita zilirushwa kutoka kwa mfumo wa roketi uliotengenezwa na Marekani aina ya Himars na kuharibu chuo cha ufundi, mbili kati yao zilidunguliwa.

Naibu kamanda wa kikosi hicho, Lt Kanali Bachurin, alikuwa miongoni mwa waliouawa.

Tume inachunguza hali iliyosababisha shambulio hilo, ilisema ni dhahiri tayari kwamba sababu kuu ya shambulio hilo ilikuwa uwepo wa matumizi makubwa ya simu janja kwa wanajeshi.

"Jambo hili liliruhusu adui kupata na kushambulia eneo la wanajeshi kwa shambulio la kombora." Ilisema taarifa moja.

Taarifa hiyo inaongeza kwamba maofisa watakaopatikana na hatia katika uchunguzi huo watafikishwa mahakamani ili hatua zichukuliwe kuzuia matukio kama hayo katika siku zijazo.

Russia pia iliongeza idadi ya wanajeshi wake waliouawa katika shambulio hilo hadi 89 kutoka 63 ya huko nyuma. Ni nadra sana kwa Russia kuthibitisha majeruhi wowote kwenye uwanja wa vita.

Chuo hicho cha ufundi kilijaa watu walioandikishwa upiginaji ambao walikuwa kati ya 300,000 walioitwa katika uhamasishaji wa watu kujiunga na vita uliofanywa na Rais Vladimir Putin mnamo Septemba.

Risasi pia zilikuwa zikihifadhiwa karibu na eneo hilo, ambalo lilikuwa limeharibiwa na kuwa kifusi.

Baadhi ya wachambuzi na wanasiasa wa Russia wamelishutumu jeshi kwa kutokuwa na uwezo, wakisema kuwa wanajeshi hao hawakupaswa kamwe kupewa makao hayo katika sehemu moja .

Pavel Gubarev, ofisa mkuu wa zamani katika mamlaka ya uwakilishi ya Russia huko Donetsk, anasema uamuzi wa kuweka idadi kubwa ya wanajeshi katika jengo moja ni uzembe na uhalifu.

"Ikiwa hakuna mtu atakayeadhibiwa kwa hili, basi itakuwa mbaya zaidi," alionya.

Naibu Spika wa bunge la Moscow, Andrei Medvedev, anasema ilitabirika kwamba wanajeshi hao wangelaumiwa badala ya kamanda aliyefanya uamuzi wa awali wa kuwaweka wanajeshi wengi katika sehemu moja.

Rais Putin alitia saini amri siku ya Jumanne kwa familia za wanajeshi waliouawa wakiwa kazini kulipwa rubles milioni 5.



MAKALA

Na Mwandishi Wetu

# HEKALU LA KIFALME LATIKISIKA

## -Kitabu cha Prince Harry chafichua mazito
## -Wengi wasubiri kuzinduliwa Januari 10



MTIKISIKO umelikumba kasri la Kifalme la Uingereza, baada ya kufichuka baadhi ya mambo yaliyokuwa yakiendelea ndani ya jumba hilo.

Katika kitabu kilichoandikwa na Prince Harry, kinachoitwa ‘Spare’ na taarifa zake zimevuja kinaelezea namna ndugu wawili wana wa mfalme Harry na William, walivyoishi kama paka na panya.

Kitabu hicho kinaelezea malalamiko na maumivu katika Familia ya Kifalme, mfano kuna madai kwamba Prince Harry na Prince William walimsihi baba yao asimuoe Camilla.

Lakini moja ya madai yanayojulikana kutoka kwa Harry, yaliyoripotiwa kwanza na gazeti la Guardian, ni jinsi alivyogombana na kaka yake.

Kasri ya Kensington na Buckingham, zote zimesema hazitatoa maoni kuhusu kitabu hicho.

Gazeti la The Guardian lilipata nakala ya kitabu hicho na kuchapisha dondoo mapema Alhamisi.

Gazeti la The Sun na mengine pia yalipata toleo la Kihispania baada ya kuchapishwa nchini Uhispania kabla ya tarehe yake rasmi ya kutolewa ambayo ni Januari 10.

Ndani ya kitabu hicho kinaelezea jinsi Prince Harry anavyoelezea kaka yake William na Catherine, ambaye sasa ni Mwana Mfalme na Binti wa Mfalme wa Wales, walimcheka baada ya kumuona akiwa amevaa sare za Nazi kwenye sherehe.

Pia kuna tuhuma za Harry kutumia dawa za kulevya na uzoefu wake wa urubani wa helikopta ya Jeshi katika mgogoro wa Afghanistan.

Hata hivyo, katika dondoo zilizovuja hakuna kitu maridhiano na maelewano kwa ndugu hao, bali kunaonekana kuwepo kwa sauti ya huzuni isiyotatuliwa, malalamiko na shutuma za madai ya Harry.

Kitabu hicho kinaelezea kuhusu familia yake ya karibu, kaka, mama wa kambo, dada na baba yake.

Kuna wingu la hasira juu ya madai hayo na haitawezekana kwa hilo kupuuzwa kwa wakati ujao pale Harry atakapoonekana na Familia ya Kifalme.

Sherehe za kumvika taji Mfalme baba yake zimebaki miezi michache tu na hazitaangalia simulizi kuhusu Harry.

**BABA ASIMUOE CAMILLA**

Harry anaandika kwamba yeye na William walimsihi baba yao asioane na Camilla, ambaye sasa ni Malkia wa Consort, kwa kuhofia angekuwa mama yao wa kambo mbaya, The Sun limeripoti.

The Sun, ambalo lilipata nakala ya Kihispania ya kitabu hicho baada ya kuchapishwa kwa bahati mbaya kabla ya tarehe rasmi ya kutolewa, linaripoti kwamba Harry anadai yeye na kaka yake walikuwa na mikutano tofauti na Camilla kabla ya kujiunga rasmi na familia.

Harry anadai kwamba alitafakari ikiwa siku moja angekuwa mama yake wa kambo mwenye roho mbaya, lakini yeye na kaka yake walikuwa tayari kumsamehe ikiwa angeweza kumfurahisha baba yao Mfalme Charles.

Hakuna maelezo yaliyotolewa kuhusu wakati ambao mkutano huo ulipofanyika au Harry alikuwa na umri gani wakati huo.

**UJUMBE KWA DIANA**

Harry anaelezea huzuni yake juu ya kifo cha mama yake, Diana, Princess wa Wales, ilisababisha kutafuta msaada kutoka kwa mwanamke ambaye alidai kuwa na nguvu.

“Mama yako anasema unaishi maisha ambayo hangeweza kuishi,” Harry anasema mwanamke huyo alimwambia.

Diana aliuawa katika ajali ya gari huko Paris mnamo 1997 wakati Harry alipokuwa na umri wa miaka 12.

Maelezo ya Harry kuhusu mazungumzo ambayo anasema alikuwa nayo na marehemu mama yake ni mafupi, gazeti la The Guardian linasema.

Pia hakuna maelezo juu ya wapi au lini mkutano na mwanamke huyo ulifanyika.

**ALIPIGWA NA WILLIAM**

Harry anadai kaka yake alishika kola yake, akararua mkufu wake na kumwangusha sakafuni kwenye jumba lake la kifahari la mjini London.



Kitabu hicho kinaweka mabishano kati ya ndugu hao.

Harry anadai yalichochewa na maoni yaliyotolewa na William kuhusu mke wake Meghan.

Harry anaandika kwamba kaka yake alikuwa akimkosoa Meghan na William akimtaja kama mtu mgumu na mkali.

Anasema kwamba kaka yake alikuwa akiongea na waandishi wa habari wakati mzozo ulipokuwa ukiongezeka, hayo kulingana na Guardian.

Harry anasemekana kuelezea kile kilichofuata, ikiwa ni pamoja na madai ya kupigana.

“Aliweka chini glasi ya maji, akaniita jina lingine, kisha akaja kwangu. Yote yalitokea haraka sana. Kwa haraka sana.

“Alinishika kwenye shingo, akararua mkufu wangu na kuniangusha chini”.

“Niliangukia kwenye bakuli la mbwa, ambalo lilipasuka chini ya mgongo wangu, vipande vipande ndani yangu. “Nilijilaza hapo kwa muda, nikiwa nimepigwa na butwaa, kisha nikasimama na kumwambia atoke nje.” Alinukuliwa Harry.

**WILLIAM NA CATHERINE**

Maelezo hayo pia yanadai Prince William na mkewe Catherine wakati Harry aliporudi nyumbani akiwa amevaa mavazi ya Nazi, kabla ya sherehe ya mavazi ya kifahari mnamo 2005.

Harry anasema alikuwa akijadili mavazi kwa ajili ya tukio hilo na kuwataka wawili hao kutoa maoni yao, kati ya sare ya marubani na vazi la Nazi ili aweze kuchagua.

“Nilimpigia simu Will na Kate na kuwauliza wanafikiria nini,sare ya Nazi.Niliikodisha, pamoja na sharubu za kubandika, na kurudi nyumbani”

“Willy na Kate walikuwa wakicheka. Ilikuwa mbaya zaidi kuwa vazi la chuichui la Willy. Ni baya zaidi.” Alisisitiza kwenye kitabu hicho.

**KUTUMIA COCAINE**

Harry anasema alipewa cocaine kwenye nyumba ya mtu alipokuwa na umri wa miaka 17 na anakiri kutumia dawa za kulevya mara kadhaa, ingawa hakuifurahia.

“Haikuwa ya kufurahisha sana na haikunifanya nijisikie mwenye furaha hasa kama ilivyoonekana kuwafanya watu wengine wote, lakini ilinifanya nijisikie tofauti, na hilo ndilo lilikuwa lengo langu kuu.

Anaongeza “Nilikuwa mvulana wa umri wa miaka 17 tayari kujaribu chochote ambacho kilibadilisha agizo lililowekwa hapo awali.”

Pia anasimulia jinsi alivyovuta bangi bafuni katika Chuo cha Eton wakati akiwa mwanafunzi, huku maafisa wa Polisi wa Thames Valley wakihudumu kama walinzi wake waliokuwa wanalinda nje ya jengo hilo.

**WILLIAM NA MEGHAN**

Harry anadai kuwa familia ya kifalme ilitaka kupanga tarehe na mahali pa kufanyika harusi yake na Meghan.

Anasema aliposhauriana na kaka yake kuhusu uwezekano wa kufunga ndoa katika kanisa la Westminster Abbey au Kanisa Kuu la St Paul, William alimwambia haiwezekani kwa sababu palikuwa sehemu waliyofunga ndoa Charles na Diana na yeye William na Catherine.

William badala yake alipendekeza kanisa la kijiji karibu na nyumba ya baba yao ya Highgrove House huko Cotswolds.

Harry na Meghan walifunga ndoa katika St George’s Chapel, Windsor Castle, Mei 2018.

Harry anafichua kwamba mwishoni mwa majira ya joto ya mwaka 2013, alikuwa akipitia wakati mbaya kiasi cha kudhoofika.

Hali hiyo ilimsababishia mashambulizi ya kutisha na hofu.

Akielezea majukumu yake wakati huo, kutoka katika kutoa hotuba hadi kufanya mahojiano, Harry anasema alijikuta hawezi kufanya kazi hizo za msingi.

“Nilipovaa koti na kufunga viatu, jasho lilikuwa likinitoka mashavuni na mgongoni”. anasema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Enzi za ndoo za chuma, bati kila kona

## -Ikitoboka inazibwa na saruji, ikichakaa chooni

Na Adam Fungamwango

HUWA nikiwaona baadhi ya kinadada , wakichota maji ndoo mbili au tatu tena kwa ndoo za plastiki na kusema wamechoka, na bomba liko jirani tu huwa nacheka peke yangu.

Afadhali waseme hivyo kipindi cha uhaba wa maji, au pale yanapo katika kwa sababu wanakwenda umbali mrefu kutafuta maji.

Nikiangalia zile ndoo za plastini ambazo siku hizi akinadada na akinamama wanabeba, halafu nikikumbuka zile ndoo za zamani ambazo walikuwa wanabeba wale wa zamani, najikuta nasema peke yangu kuwa ni kweli zama hazifanani na kila zama na kitabu chake.

Nakumbuka jinsi kinamama, kinadada na hata watoto wa zamani walivyokuwa wakipata tabu kuchota maji wakiwa na aina ya ndoo ambazo kwa sasa sidhani kama hawa wa sasa wanaweza kukubali kubeba.

Na cha kujiuliza ni kwamba hata hizo nguvu zenyewe za kubeba wanaweza kuwa nazo?

Watoto, akinadada na akinamama wa zamani walikuwa wakakamavu na nguvu kweli, labda kutokana na aina ya vyakula walivyokuwa wakila miaka hiyo ambavyo vingi ni vya asili, visivyokuwa na mafuta mengi na vingi si vya kusindikwa viwandani.

Zamani kulikuwa na ndoo za chuma. Hizi zilikuwa nzito kabla hata mtu hajakwenda kuchota maji.

Halafu kulikuwa na ndoo za bati. Uzito wake ulikuwa na fadhali kidogo, lakini ndoo zote hizi kwa hali ya kawaida tu zilikuwa nzito, lakini kinamama walikuwa wakizikusanya na kwenda nazo bombani kupanga nazo foleni.



Ikijaa anaomba kutwishwa huku kichwani akiwa ameweka nguo yoyote au tambara lililokunjwa mduara maarufu kama ngata ili kichwa kisiumie.

Mara nyingi zamani mabomba yalikuwa mbali na nyumbani, hivyo ataanza safari ya kupeleka na kurudia kuchukua nyingine hadi hapo zitakapoisha.

Wapo wale wa vijijini. Hawa ndiyo walipata tabu sana kwa sababu walisafiri umbali wa kilometa kadhaa hivi kwenda kusaka maji. Mbali na kutembea kwa muda mrefu, lakini ndoo pia ilikaa kichwani kwa muda mrefu na safari ya kutembea kwa miguu nayo haikumuacha salama.

Kwa jinsi ilivyo, nilitamani hizi ndoo nyepesi za plastiki ndizo wangezitumia akinamama wa zamani na zile ngumu za chuma na bati wangezitumia hawa wa sasa.

Ni kwa sababu hawa wa sasa hawaendi umbali mrefu sana kama wale wa zamani. Lakini kila kitu kina sababu yake.

Pamoja na uzito wa ndoo ya chuma na bati, lakini pia kinamama na watoto wa zamani walikuwa wanapata changamoto nyingi kila ndoo hizo zinapoanza kuwa kuukuu.

Kwanza kabisa usiombe ianguke hasa ikuangukie mguuni kwa sababu sehemu ya kuweka ndoo chini inakuwa na upinde ambao ukifanya masihara ikakuangukia vizuri mguuni, inaweza kukukata ukaomba po.

Kuna upinde pembeni ambao hutumika kuifanya ndoo iwekwe chini bila matatizo, lakini unakuwa na makali yaliyozunguka ambayo yakikupiga popote pale kama ndoo itaanguka, yanaweza kukujeruhi.

"Hapo kwenye upinde wa kwenye kitako ukikuangukia mguu unaweza kukatika, halafu mama yako anakwambia bamiza tu mwanangu hiyo ndoo hamna shida baba yako si fundi vyuma?" Huo ulikuwa ni ujumbe wa mchangiaji mmoja mada hiyo ilipowekwa kwenye mtandao wa kijamii.

Changamoto nyingine ndoo inapotoboka. Kwa sababu akinamama wa zamani walikuwa wabunifu, kwani ikitoboka na hasa kule chini wanaziba au kusiliba na simenti ili maji yasivuje. Sasa hapo uzito ndiyo unaongezeka kabisa.

Usiombe mtoto utumwe ukachote maji halafu upewe ndoo ambayo imesilibwa na simenti. Maana sasa inakuwa nzito kuliko uzito wa maji ambayo unaambiwa ukachote.

Faida pekee waliyokuwa wakipata akinamama na watoto wa zamani kwa ndoo hizo nzito ni kuwa walikuwa na uwezo wa kuzitumia kwa kuinjikia maji ya kuoga.

Bila kutumua sufuria, karani au kitu chochote kile, ndoo yenyewe kwa sababu ni ya chuma au bati ilikuwa ikijazwa maji inawekwa juu ya jiko la mkaa au kuni, hapo maji hadi yanachemka, yanapoozwa na ya baridi, watu wakwenda kuoga.

Kwenye hizi ndoo za kisasa za plastiki thubutu.

Na cha kuwakumbusha vijana wa sasa kuwa ndoo ikiendelea kuwa kukuu sana mpaka ikashika kutu sasa hiyo inabadilishiwa matumizi, badala ya kutupwa inahamishiwa bafuni au msalani. Ilimradi tu isiwe inavunjwa na mara nyingi mpaka inafika huko, imeshasilibwa simenti na kuongezeka uzito maradufu kiasi kwamba sasa hata kuibeba tu yenyewe tabu.





## China yataka haki Covid-19

**BEIJING,** CHINA

WIZARA ya Mambo ya Nje ya China, imesema Umoja wa Ulaya unapaswa kuzingatia haki katika hali ya janga la UVIKO-19.

Msemaji wa wizara hiyo, Mao Ning, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini Beijing. Mao alikuwa akijibu swali kuhusu mapendekezo ya Umoja wa Ulaya kutaka abiria kutoka China wapimwe virusi vya corona kabla ya kuondoka nchini humo.

Maofisa wa serikali za Ulaya wamependekeza kwamba wasafiri wote wanaoingia kutoka China wanatakiwa kuthibitisha kwamba hawana maambukizi ya UVIKO-19 kabla ya kuanza safari.

Ujerumani, Ubelgiji, Sweden na Ugiriki juzi zilitangaza kuwa zinaanzisha upimaji wa lazima wa UVIKO-19 kwa abiria kutoka China.

Nchi hizo nne zimefuata nyayo za Uingereza, Ufaransa, Italia, Korea Kusini na Marekani. **DW**

## Umoja wa Mataifa wabaini M23 bado wanashikilia maeneo DRC

**NEWYORK,** MAREKANI

WATAALAM wa masuala ya kijasusi wa Umoja wa Mataifa, wamesema wamebaini operesheni zinazoshukiwa kuwa za waasi wa M23 kwenye maeneo ya mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Nyaraka za ndani za Umoja huo zilionesha jana kuwa M23 wamedhibiti maeneo mengine, wakati ambapo walitakiwa kuondoka huko.

Kitengo cha Ujasusi cha Umoja wa Mataifa, kilisema katika ripoti yake ya siri kwamba waasi hao hawajaondoka kabisa katika jimbo la Kivu Kaskazini na mji wa Kibumba. Ripoti hiyo ilieleza kuwa mapigano kadhaa yanayowahusisha M23 yameripotiwa wiki hii na kusababisha waasi hao kudhibiti maeneo zaidi ikiwemo Kitchanga na Nyamilima na kusababisha wasiwasi kwa raia.

M23 walipaswa kuondoka pia kwenye mji wa kimkakati wa Rumangabo hadi kufikia jana, lakini siku ya Jumatano Kikosi cha Jumuia ya Afrika Mashariki kiliahirisha hafla iliyopangwa ya makabidhiano, kikisema bado kinatathmini hali ya usalama **DW**

# Republican washindwa kumchagua Spika

**WASHINGTON,** MAREKANI

KIONGOZI wa chama cha Republican katika Baraza la Wawakilishi nchini Marekani, Kevin McCarthy, ameshindwa kwa mara nyingine katika jaribio la kuchaguliwa Spika wa bunge hilo.

Imeelezwa mkwamo wa kumpata spika haujaonekana tangu enzi ya kabla ya vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini humo.

Kundi la wafuasi wa mrengo wa kulia katika chama chake walizuia jaribio la 11 la kumchagua katika siku ya tatu ya upigaji kura.

Wanachama wa Republican walichukua udhibiti wa Bunge hilo katika uchaguzi wa katikati ya muhula wa Novemba, lakini mzozo huo umesababisha baraza hilo kushindwa kuwaapisha wanachama au kupitisha miswada.

Tangu 1860, wakati muungano wa Marekani ulipokuwa ukivutana juu ya suala la utumwa, baraza la chini la Congress lilipiga kura mara nyingi kuchagua Spika. Wakati huo ilichukua raundi 44 za kura.

Kundi la wabunge 20 wenye msimamo mkali wa chama cha Republican, wanakataa kumpa McCarthy kura 218 zinazohitajika.

Waasi hao wana mashaka na imani ya kihafidhina ya mbunge huyo wa California, licha ya kuidhinishwa na Rais wa zamani Donald Trump.

Mmoja wa wapinzani, Ralph Norman wa South Carolina, aliiambia BBC kuwa hana imani na McCarthy.

Mbunge huyo alisema timu ya McCarthy ilitishia kulipiza kisasi kisiasa dhidi yao ikiwa hawangetii msimamo wa chama, katika wiki chache kabla ya mkwamo huo.

"Tulikuwa tunaenda kutupwa nje ya kamati," alisema Norman na aliendelea "Tutapoteza kila fursa tuliyokuwa nayo"

**BBC**



Wanajeshi wa Ukraine wakifyatua makombora aina ya A65 Msta-B kuelekea vikosi vya Russia katika mstari wa mbele katika mkoa wa Zaporizhzhia, jana. **PICHA: REUTERS**

## Putin aomba kusitishwa vita, Ukraine yajibu kwa kukataa

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia Vladimir Putin amemuamuru waziri wake wa ulinzi kusitisha vita kwa saa 36 kwenye mstari wa mbele wa vita huko Ukraine, kuanzia jana.

Usitishaji mapigano, uliopangwa kuanza saa 12:00 saa za Russia, kwa sababu ya kuwapa nafasi watu kusherehekea Sikukuu ya Krismasi ya kanisa la Orthodox la nchini humo.

Putin aliiomba Ukraine ijibu, lakini nchi hiyo ilikataa ombi hilo kwa haraka.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alisema mapatano hayo ni jaribio la kusitisha hatua za kijeshi za nchi yake.

Taarifa ya Ikulu ya Kremlin ilionekana kusisitiza kwamba Rais Putin, aliamuru wanajeshi wake kuacha mapigano sio kwa sababu alikuwa anazidisha kasi.

Alisema Putin hapunguzi kasi yake kamwe katika kila jambo, lakini kwa sababu alisikiliza ombi kutoka kwa mkuu wa Kanisa la Orthodox la Russia.

Patriaki Kirill alitoa wito wa kusitishwa kwa mapigano ili kutoa fursa kwa sherehe za Krismasi na kuwaruhusu waumini kuhudhuria ibada za kanisa kwa ajili ya Krismasi ya Orthodox.

Kanisa la Orthodox la Russia huadhimisha siku ya Krismasi Januari 7, kila mwaka kulingana na kalenda ya Julian.

"Kwa kuzingatia ombi la Kirill, rais anamwagiza waziri wa ulinzi wa Shirikisho la Russia kuweka utaratibu wa kusitisha mapigano katika mstari wote wa mapambano nchini Ukraine, kwa muda wa saa 36," ilisema taarifa hiyo ya Ikulu.

Agizo la Putin liliitaka Ukraine kufanya hivyo pia ili idadi kubwa ya waumini wa Orthodox ambao wanaishi katika maeneo ambayo uhasama unaendelea waweze kusherehekea Mkesha wa Krismasi kuanzia jana na leo.

Katika siku chache zilizopita, nchi za Magharibi zimekuwa zikizungumza juu ya nia yao kutoa magari ya kivita kwenda Ukraine, ambayo vikosi vya wanajeshi vya Ukraine vinahitaji kufanya mashambulizi.

Kabla ya hatua hiyo, Ukraine mara kwa mara ilielezea kutoridhika na kusita kwa nchi za Magharibi kuwapa zana zenye uwezo wa kupambana vilivyo na Russia.

Siku ya Jumatano, Rais Biden alijibu kwa uthibitisho swali kuhusu kama Marekani ilikuwa inafikiria kuhamisha magari ya kivita ya Bradley hadi Ukraine.

Maofisa katika utawala wake walisema magari ya APC yanaweza kujumuishwa katika kifurushi cha silaha kitakachotangazwa wiki hii.

Kulingana na Associated Press , magari ya Bradley yangetangazwa jana kuyapekeka Ukraine dazeni kadhaa.

Kutakuwa na takriban Bradleys 50 katika kifurushi kipya cha msaada wa kijeshi, vyanzo viliiambia Reuters, kwa gharama ya jumla ya dola bilioni 2.8.

Siku hiyo hiyo, Ufaransa ilitangaza kwamba ingeipatia Ukraine mizinga ya magurudumu mepesi ya AMX-10RC na Magari ya kijeshi aina ya Bastion.

Kwa mujibu wa ofisi ya Rais Macron, hatua hiyo itakuwa ya kwanza kwa vifaru vya kisasa vinavyotengenezwa na nchi za Magharibi kufikishwa Ukraine.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**CIVIL CASE 3/2022**
**HEKI BUSINESS CO. ..............PLANTIFF**
**VERSUS**
**TANZATHAI I.R CO.LTD............DEFFENDANT**
**TO: TANZATHAI I.R CO. LTD**

## NOTICE OF DATE OF MENTION

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing/mention on **17 day of 1, 2023 at 9:00 am** Before **Hon KATEMANA RM/SRM**

**YOUR ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail and you may bring with you all required documents in support of your case.

Given under my hand and the seal of the court this 2 day of 12, 2022

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**
**Usimamizi wa mirathi na 02|2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HALIMA WAZIRI OMARI**
**KATIKA SAHURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIOLETWA NA RAMADHANI RASHIDI ABDALLAH**

## TANGAZO

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama zamwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa
Hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 01 Mwezi 01 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehem anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetotewa leo tarehe 05 Mwezi 01 mwaka 2023**

---

## KUPOTELEWA NA CHETI



**UPENDO JOFREY LAIZER** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S5202-0129** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **TINGATINGA SEKONDARY** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MAG/RB/9424/2023.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## HATI YA KIAPO

**MIMI CLETUS CHRISTOPHER OLOMY** wa Kange, Tanga, nikiwa mtu mzima na akili zangu timamu naapa mbele ya Wakili kama ifuatavyo:

- Kwamba ni mmiliki wa kiwanja **Na. 247, Kitalu 'A' Kange,** Tanga.
- Kwamba hati ya toleo (offer) ya kiwanja kilichotajwa katika aya Na. 1 hapo juu imepotea na nimefanya juhudi mbalimbali za kuitafuta lakini nimeshindwa kuipata.
- Kwamba kutokana na maelezo niliyoeleza katika ya Na. 1 na 2 hapo juu naomba ifahamike kwa mamlaka zozote zile ya kwamba hati hiyo ya toleo (offer) imepotea na siwezi kuipata tene.

Ninathibitisha kwamba hayo niliyoyatamka hapo juu katika aya ya 1-3 ni kweli tupu kwa kadri nijuavyo na kwa kadri ya sharia za viapo.

Imethibitishwa hapa Tanga
Na CLETUS CHRISTOPHER OLOMY
Leo tarehe 06 mwezi wa 01, 2023
CLETUS CHRISTOPHER OLOMY

MBELE YANGU: M. B. Maiga
CHEO: WAKILI
ANUANI: TANGA
SAHIHI:

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TANZANIA NATIONAL PARKS** inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **SU35584 – LANDROVER. ENGINE NO. 16194002B. CHASIS NO. SALLDHMF72A635065.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/9723/2023.**

---

## NOTISI/ TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART & GENERAL BROKERS kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya EQUITY BANK (TANZANIA) LIMITED,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya mnada wa hadhara kuuza dhamana uliyoweka kama ratiba inavyoonyesha.

| s/No. | Jina la Mdaiwa | Jina la mdhamini | Dhamana | Mahali ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | PAUL JOHN MUSHI | JANEROSE MAGOTI LANGALANGA | Nyumba | MTAA WA KWAZOMBOKO,MBAGALA CHARAMBE-TEMEKE. "LAND PARCEL TMK/CHB/ZBK18/174" | 25/01/2023 Kuanzia saa 4:30 asubuhi na kuendelea. |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0788411524 /0714939933.**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi bila gharama yeyote.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **Aly Mohemed Seleman** wa Bariadi Simiyu anatangaza kupotewa kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **T 555 AWC** aina ya sunlg rangi nyekundu. Taarifa imetolewa katika kituo cha polisi Bariadi na kupewa namba **MS/MAS/RB/8035/2023.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au awasiliane naye kwa namba ya simiyu, **0682710 202.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI ZA MAGARI

**OLIVIA HILARY ANASTAZI** anatangaza kupoteza kadi za magari matatu ya shule zilizosajiliwa kwa jina la Muleba Sekondari yenye namba za usajili **T365 CFY, T861 AQC na T195 BEJ.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/MUL/RB/7342/2023.** Kwa yeyote atakayeziona atoe taarifa polisi au apige simu **namba 0763916092.**

---

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF LANDS, HOUSING AND HUMAN SETTLEMENT DEVELOPMENT**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, (CAP 117)**

## DEED POLL



The documents presented for registration on the **30-12-2022** at **1:00PM** herewith the original of the above mentioned documents registration having under folio/s **2033** and serial/s **18/2023** knowledge receipt of the enclosures here to.
**URES:**

**SIGNED AND DELIVERED BY SAID TEREZA NYANGARYA MAGOMA**
Who is known to me personally
Identified to me by....the letter being known to me personally.
This **28** day of **12 / 2022.**

DEPONENT

**BEFOR ME:**

BEFORE ME
Name:
Signature:
Postal Address:
Date:
Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AZIZA HASSANI MUSSA** anatangaza kupoteza kadi ya gari aina ya **Toyota Hiace,** rangi **nyeupe** yenye usajili wa **T 106 BES,** Chasis **No.L111291008599.** Taarifa ya polisi namba **DSM/PHQ/RB/5469/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu **namba 0682494345**

---

**LEGENDS AUCTION MART AND GENERAL BROKER LIMITED**

## TAARIFA YA MNADA WA HADHARA

KWA MAMLAKA TULIYOPEWA NA **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MAGARI YAFUATAYO KUANZIA **TAREHE 16 JANUARY 2023 NA TAREHE 19 JANUARY 2023 KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI.**

ORODHA YA MALI ZITAKAZOUZWA NI KAMA IFUATAVYO HAPA CHINI

| S/N | JINA LA MTEJA | MODEL | USAJILI | MAHALI LILIPO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SAMWEL KISAKA MZAVA | LPK 2519 | T598DMK | MWANZA |
| 2. | JULIUS GAMBA MUGETA | LPT709 | T548DXP | MWANZA |
| 3. | SASN AUTO GARAGE COMPANY LIMITED | NOVUS 340HP | T275DVM | DAR ES SALAAM |
| 4. | ISAYA LWIDIKO SANGA | LP909Bus | T424DNM | DAR ES SALAAM |
| 5. | YAMIN MOHAMED SULEIMAN | UTRA BUS | T728DVN | DAR ES SALAAM |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14 na ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa
3. Gharama ya kukagua na kuona magari ni ya mnunuzi pamoja na kuhamisha umiliki ni ya mnunuzi.
4. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote akatayejaribu kuharibu mnada huu
5. Kwa mawasiliano zaidi piga namba **0714939933 AU 0788411524**

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, ni mmoja wa wasichana warembo kijijini hapo ni mmoja waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# MTAKE MSITAKE-13

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Nasema kila siku wewe ni mwanamke mwenye akili sana, na kweli, mimi nitagharamia kila kitu. Tufanye sherehe kubwa ya kumuaga Adel ndugu yetu anaondoka, halafu tunaondoka naye kumpeleka kwenye Hospitali ya Muhimbili kumtelekeza kama mpango wetu tulivyopanga."

"Na baada ya hapo na sisi tunatokomea. tunakwenda kuishi Arusha si ndiyo mpenzi?"

"Haswa na mimi huku tena, nitakuwa natuma tu mwakilishi, sina mpango wa kurudi tena huku, mambo yote yatakuwa yanasimamiwa na watu wangu."

"Urudi kufanya nini, Henock atakuacha kweli?" Alipomaliza kusema hivyo, wakaangua kicheko.

"Yaani imebaki wiki mbili naona kama mwaka mtoto we, nilikuwa na hamu na wewe." Usonzo akafunguka.


"Anza kufanya mazoezi kabisa, wiki mbili tu zimebaki na mimi kumaliza dozi yako ya dawa ya tumbo niliyokwambia, kila kitu kimekwenda kama kilivyopangwa."

Siku mbili baadaye Mary na Adel walikwenda tena ofisini kwa Usonzo kumshukuru kwa kutoa kitita cha pesa ambacho kitafanikisha matibabu yake na nauli pia.

Wakati akiongea maneno matamu ya kumuaga mfadhili, Mary na Usonzo walitazamana na kukonyezana kwani wanajua hakukuwa na mpango wowote ule, bali wanachotaka kufanya ni kwenda kumtelekeza hospitali ili wapate nafasi ya kwenda kula raha. Kwenda Arusha kula nchi. Kula kuku hadi bata waone wivu. Kula kuku na mifupa yake. Kula kuku kwa mrija.

*****************************

"Jamani wananchi ya kijiji chetu hiki, tumesanyika hapa, leo siyo mkutano kama ilivyo siku zote, ila leo ni tafrija. Ni pati ya kumuaga rafiki yetu, kipenzi chetu Adel Adam. Yeye ndiye aliyeomba tufanye pati hii kwa ajili ya kuwashukuru wakazi wote kwa kipindi chote ambacho alikuwa nasi hapa. Kuna mazuri ambayo yamefanyika, ingawa yapo ambayo yamemsababishia matatizo, lakini yeye mwenyewe amesamehe kwa sababu anasema ni mipango ya Mwenyezi Mungu.Alikuja kwenye kijiji hiki kumchukua bibi yake kumpeleka jijini Dar es Salaam kwa matibabu, lakini yalitokea kila mtu anajua, haikuwezekana, akaingia kwenye matatizo, na hayo mimi sitokuwa mzungumzaji, yatazungumzwa na wengine. Leo hapa ni kula na kunywa. Yeye mwenyewe yupo meza kuu hapa akiwa na mwekezaji wetu Usonzo pamoja na rafiki yake naweza nikasema, anaitwa Mary." Alikuwa ni Mzee Chale Mwenyekiti wa kijiji, ambaye ni kama vile alikuwa anafungua rasmi hafla hiyo.




**Pamoja na kwamba kulikuwa na disco linapigwa, lakini bado muungurumo ulikuwa mkubwa zaidi kila muda unavyozidi.**

Tangu saa nne asubuhi watu sherehe ilianza kwa ngoma na disco, mchana watu wakala na kunywa na kila kitu kiliendelea hadi saa 10:00 jioni baadhi ya watu wako hoi kwa kilevi, lakini ni kama vile ndiyo ilikuwa inaanza, kwani wakubwa ndiyo walikuwa wanaingia.

Kwa jinsi itifaki ilivyopangwa ni kwamba baada ya Mzee Chale kumaliza, Mary alitakiwa kupanda ili na yeye akatoe machache yake.

Aliongea mengi jinsi alivyokutana na Adel kwa mara ya kwanza na akawa ni shujaa wake alipomuokoa kwenye ajali ya bodaboda, na hadi alivyohusika na kumtia mtoto wa watu upofu.

"Jamani mimi nimechukuliwa kama mtu mbaya hapa kijijini na baadhi ya watu, lakini nilikuwa nalinda uchumba wangu, nimefanya hivi kwa hasira maana alikuwa ananisumbua sana, alikuwa ananitaka kimapenzi. Lakini yote yamepita, nimemuomba msahama amekubali kwa masharti kuwa mimi niwe ndiye namuongoza kila anakokwenda na kukaa kwangu hadi atakapondoka. Ndiyo maana mnaona hakwenda kumshtaki polisi, lakini ahadi nyingine imekuwa ni siri yangu mimi mchumba wangu Enock na yeye mwenyewe Adel, kwa hiyo nimtakie kila la kheri, asikose kuja kututembelea, hapa sasa ni kama kwake," alisema Mary, lakini hakupigiwa sana makofi na kushangiliwa kama mzee Chale. Wengi walimuona ni mnafiki tu.

Kuna walevi wachache walizomea.

Mzee Chale anamsimamisha Mosha Usonzo ili aje kuongea na wananchi wa kijiji hicho. Alianza mbali sana kuwapozapoza na kuahidi kuwachimbia kisima, achana na kile ambacho alichimba kwa ajili ya mashamba yake na hakitumiwi na wanakijiji. Wananchi walinyamaza kimya wakimsikiliza. Hakuna aliyepiga makofi, wala kumshangilia. Wengine waliendelea kunywa.

"Ni kijana mzuri tumeishi naye hapa, ana nidhamu, pamoja na matatizo ambayo yametokea kwake, kupata ulemavu wa kudumu, lakini bado amemsamehe Mary na maisha yameendelea, namsifu pia mchumba wa Mary, bwana Enock kwa kuwa mvumilivu kwa kipindi chote hiki. Kwa haya yote namkaribisha bwana Adel mwenyewe asimame na kutoa mawili matatu." Akamaliza Usonzo.

Hakuna yoyote kati ya Usonzo au Mary aliyeeleza mbele ya wanakijiji kuwa mpango wao pale ni kumuondoa, kumpeleka kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kumtelekeza huko.

"Kila mtu anajua nini kimetokea kwenye kijiji hiki, mimi nimemuachia Mungu, na leo hii nawaaga, naondoka. Lakini kabla ya kupata madhila haya nilikuwa kwenye wakati mzuri. Na hata sasa naondoka nimekuwa na marafiki wengi hapa. Hata aliyefanya hivi pia mpaka sasa ni rafiki yangu. Imetokea tu, ajali siku zote haina kinga..."

Wakati anaongea huku baadhi ya watu waliokuwa wanamkubali na kumpenda Adel kutokana na tabia yake njema tangu alivyoingia hadi alipopofuliwa macho kwa kumwagiwa tindikali wakiwa wanamshangilia, kulisikika muungurumo wa gari kwa mbali.

Pamoja na kwamba kulikuwa na disco linapigwa, lakini bado muungurumo ulikuwa mkubwa zaidi kila muda unavyozidi.

Na kweli, yalionekana magari matatu, Land Cruiser VX moja, V8 moja na Land Rover moja aina ya Defender nyeupe, zote zilikuwa zikiwa kasi zikielekea sehemu ambayo kuna sherehe.

Baadhi waliogopa, lakini kwa sababu wengi walio walikuwa wamelewa, waliona ni jambo la kawaida. Jinsi yalivyokuwa yakikaribia vumbi lilitimka isivyo kawaida. Hakuna aliyejua ni kitu gani kimetokea.

Yalifika na kusimama pale pale kwenye uwanja wa shule ya msingi ambapo hafla hiyo ilikuwa inafanyika. Kwa namna ambayo haikutegemewa, walishuka watu wawili tu kwenye gari VX, waliokuwa wamevaa suti zenye rangi ya bluu. Na hata hivyo bado kuna watu wengine waliokuwa wamebaki kwenye gari hilo. Hakuna yeyote aliyeshuka kwenye magari mawili yaliyobaki licha ya kwamba ndani kulikuwa na watu. Hawakuonekana ni watu wa kawaida. Ilionekana kabisa kuna jambo wamelifuata. Kuna kitu kimetokea au kinataka kutokea.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# AZAM FC YAUOTA UBINGWA KOMBE LA MAPINDUZI 2023

**Na Saada Akida,**
ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Kally Ongala, amewapongeza wachezaji wake kwa kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi na kuongeza mwaka huu michuano hiyo imekuwa na ushindani mkubwa.

**Azam FC ilitinga hatua ya nusu fainali baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Jamhuri kutoka Pemba katika mechi iliyoche zwa juzi jioni.**

Kwa matokeo hayo, Azam FC imeongoza Kundi A ikiwa na pointi nne sawa na Malindi lakini wao wakiwa na mabao manne kibindoni huku Malindi ikiiaga michuano hiyo kwa sababu imemaliza kundi hilo ikiwa katika nafasi ya pili.

Kally alisema anawashukuru wachezaji wake kwa kupambana na kuinusuru timu yao kuondolewa katika hatua ya makundi kama ilivyotolea kwa waliokuwa mabingwa watetezi, Simba kutoka Dar es Salaam.

Kocha huyo alisema maandalizi mazuri waliyofanya ndio siri pekee ya kikosi chake kusonga mbele na ubora wa wachezaji wake pia umewafanya wastahili kuendelea katika michuano hiyo.

Aliongeza katika mechi ya juzi wachezaji wake walionyesha kiwango kizuri na anaamini wataendelea kufanya hivyo kwenye mechi ya hatua ya nusu fainali ili watimize malengo ya kurejea na ubingwa wa kombe hilo.

"Msimu huu hii michuano imekuwa migumu, tumekutana na ushindani mkubwa katika michezo yetu miwili, bado kidogo tuondolewe katika mashindano lakini wachezaji wamepambana na kupata matokeo mazuri na kutufanya tusonge mbele," alisema Kally.

Aliongeza mbali na kutaka kushinda kikombe, bado wanatumia michuano hiyo kujenga muunganiko na kutafuta kikosi cha kwanza kwa sababu kila mchezaji anatafuta namba hali iliyowalazimu kusafiri na wachezaji wote waliosajiliwa.

"Bado tunajifunza na kila mechi kwetu tunapata kitu, na kwa sababu tunahitaji kujenga kikosi imara, tumekuja na wachezaji wetu wote ili kuhakikisha kila mmoja anapata nafasi ya kucheza katika kikosi cha kwanza lakini pia kurejea nyumbani tukiwa na kombe hili," alisema kocha huyo.

Mbali na Azam, timu nyingine iliyofanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ni Mlandege wakati wapinzani wao walitarajiwa kujulikana baada ya mechi za jana kumalizika.



Kocha wa Ilala Queens inayojiandaa na Ligi ya Wanawake ya Mkoa wa Dar es Salaam, Allen Haule (kushoto), akitoa maelekezo kwa wachezaji wake wakati wa mazoezi yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Karume, jijini jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Makocha Z'bar wafurahia ubora

**Na Saada Akida,**
ZANZIBAR

WAKATI Simba ikivuliwa ubingwa na kutolewa katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea visiwani hapa, makocha wanaofundisha timu za Zanzibar wameridhishwa na viwango wa nyota wao huku pia wakijipanga kuvuka maji kufuata wachezaji wapya kutoka Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Malindi, Omary Ally, alisema mwaka huu Wazanzibari wameonyesha ukomavu tofauti na miaka ya nyuma kwa kuwashangaza vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga.

Omary alisema kiwango walichokionyesha kilikuwa cha juu ingawa bado wana tatizo la washambuliaji, hivyo timu yake imejipanga kuanza mchakato wa haraka kusajili mastraika wapya ili kuongeza nguvu kabla ya Ligi Kuu Zanzibar haijarejea.

"Mashindano haya yametusaidia sana kuona mapungufu yetu,timu yetu imekuwa imara kila sehemu isipokuwa tumeangushwa na washambuliaji, tayari tumeanza mchakato huo wa kuangalia washambuliaji kutoka Bara ili kuja kuimarisha vikosi vya timu zetu," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema timu yake imeonyesha kiwango kizuri lakini anahitaji kuboresha safu ya ushambuliaji ambayo haikuwa makini katika kutumia nafasi walizopata.

"Tulikuwa vizuri katika idara ya ulinzi na viungo, lakini tumeangushwa na safu ya ushambuliaji, hili ni tatizo kubwa, tunahitaji kuangalia zaidi katika nafasi hii ili kuimarisha kikosi cha timu yetu wakati huu wa usajili wa dirisha dogo," Msimu alisema.

## Oppa macho yote kiatu cha dhahabu

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Simba Queens, Oppa Clement, amesema malengo yake msimu huu ni kutwaa Tuzo ya Ufungaji Bora katika Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ambayo inaendelea kwenye viwanja mbalimbali hapa nchini.

Akizungumza na gazeti hili jijini, Dar es Salaam jana, Oppa alisema ataendelea kucheza katika kiwango cha juu na chenye ushindani kwenye michezo yote ili atimize ndoto yake.

"Malengo yangu ni kuwa mfungaji bora wa msimu huu, naamini hakuna linaloshindikana, nikishirikiana na wachezaji wenzangu kuhakikisha tunaipa mafanikio timu yetu," alisema Oppa.

Straika huyo alisema kila mchezo kwa upande wao wanaufananisha na fainali hivyo kuzitaka timu nyingine zikae sawa kuwakabili pale watakapokutana nao.

"Ligi ya msimu huu ina ushindani tofauti na msimu uliopita, nimefurahi tumepata pointi tatu baada ya kuifunga Fountain Gate Princess ambayo ilikuwa haijafungwa tangu tulipoanza msimu, tunaomba mashabiki wetu waendelee kutuamini,"alisema nyota huyo.

Simba Queens ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 10 kutoka mikoa mbalimbali.

## Tenisi Tanzania yapania makubwa

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha timu ya vijana ya tenisi ya umri chini ya miaka 14 na 16 kiko kamili kwenda kupeperusha bendera ya nchi katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika kuanzia Jumatatu nchini Burundi, imeelezwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Tenesi Tanzania (TTTA), Dennis Nkoi, alisema lengo la mashindano hayo ni kupata wachezaji bora Afrika ambao watakwenda kushiriki michuano ya Kombe la Dunia itakayofanyika baadaye mwaka huu.

"Maandalizi kuelekea katika mashindano hayo yatakatoshirikisha wachezaji wasichana na wavulana yanaendelea vizuri, wachezaji wote wanajifua ili kujiimarisha na kwenda kuiwakilisha vyema Tanzania,"alisema Nkoi.

Alitaja nchi nyingine zitakazoshiriki katika mashindano hayo ni pamoja na Eritrea, Djibouti, Somalia, Ethiopia, Sudan Kusini, Kenya, Uganda, Rwanda, Comoro, Shelisheli na wenyeji Burundi.

"Mchezo wa tenisi kwa sasa unazidi kukua tofauti na miaka iliyopita, kila siku vipaji vipya vinaibuka, tunaamini ndani ya miaka miwili ijayo nchi yetu itafika mbali kwa sababu tayar tuna wachezaji wengi wazuri na mikakati yetu ni kuwekeza kwa vijana," Nkoi aliongeza.

## ZISIKUPITE

### KOLO ANUKIA UNITED



KLABU ya Manchester United inavutiwa na mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt mwenye umri wa miaka 24, Randal Kolo Muani. (***Sky Germany***)

### JUDE AKARIBIA MADRID

REAL Madrid ina matumaini ya uwezekano wa kuishinda Liverpool katika usajili wa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19 kutoka Borussia Dortmund. (***Marca***)

### LAPORTA: JONG HAUZWI



KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 25 ni mmoja wa wachezaji wanne wa Barcelona ambao hawatauzwa mwezi huu, kwa mujibu wa Rais wa klabu hiyo, Joan Laporta. (***Mirror***)

### KUDUS AWEKWA SOKONI

AJAX wameweka bei ya pauni milioni 40 kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ghana, Mohammed Kudus, mwenye umri wa miaka 22, ambaye anasakwa na Manchester United. (***Star***)

### DISASI ATAJWA UNITED

MANCHESTER United imefanya mazungumzo ya awali kuhusu kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Axel Disasi kutoka Monaco, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 akifuatiliwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England. (***Mail***)

### SOUTHAMPTON ANUKIA KEANE

KLABU ya Southampton inaangalia uwezekano wa kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya England, Michael Keane mwenye umri wa miaka 29 kutoka Everton. (***Athletic***)

### ORSIC KUTUA DINAMO

SOUTHAMPTON imekubali mkataba wa pauni milioni sita na Dinamo Zagreb kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Croatia, Mislav Orsic. (Fabrizio Romano)

### JUVENTUS, DORTMUND VITANI

JUVENTUS na Borussia Dortmund zinamfuatilia kiungo wa kati wa Aston Villa, Tim Iroegbunam mwenye umri wa miaka 19 ambaye yuko kwa mkopo Queens Park Rangers. (***Teamtalk***)

### MUDRYK AITAKA ARSENAL

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 22 amefahamisha Shakhtar Donetsk kwamba anataka kujiunga na Arsenal Januari hii. (***90min***)

### PATERSON ANUKIA CITY

KLABU ya Coventry City inaweza kumnunua kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jamie Paterson, ambaye ana umri wa miaka 31. (***Coventry Live***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# SANCHO AENDELEA KUIVURUGA UNITED

## Kocha wake asema nyota huyo bado hayuko fiti kuingia uwanjani kwa...

**MANCHESTER,** England

JADON Sancho anahitaji kuwa fiti "kimwili na kiakili" kabla ya kurejea katika timu ya Manchester United, kwa mujibu wa Kocha, Erik ten Hag.

Sancho hajacheza tangu Oktoba, mwaka jana na alikosa kambi ya United nchini Hispania wakati wa Kombe la Dunia, badala yake alisafiri hadi Uholanzi kushiriki katika programu ya mazoezi ya mtu binafsi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 sasa amerejea Manchester lakini Ten Hag amesema winga huyo wa Timu ya Taifa ya England hayuko fiti vya kutosha kurejea uwanjani.

"Kwa wakati huu hayuko sawa vya kutosha," alisema Ten Hag akiwaambia wanahabari.

**"Ni kimwili na akili bado hayuko sawa. Lakini nadhani sasa anaendelea vizuri katika sehemu ya kimwili na hiyo itamsaidia. Natumaini anaweza kurudi haraka lakini siwezi kusema ni muda gani."**

Kukosekana kwa Sancho kumepunguza zaidi chaguzi zake mbele lakini Ten Hag amesisitiza hatamharakisha mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City na Borussia Dortmund licha ya kukabiliwa na mfululizo wa mechi nyingi katika mashindano manne katika kipindi cha pili cha msimu.

"Ningependa kumrejesha Jadon haraka iwezekanavyo," alisema Ten Hag. "Lakini pia katika hili, siwezi kulazimisha utaratibu huu na hivyo nitafanya kila lililo katika uwezo wangu, lakini michakato mingine huwezi kuilazimisha na hii ni moja wapo.

"Kwa hiyo lazima nionyeshe uvumilivu, ingawa sina uvumilivu kwa sababu ndio, uko sawa, tunakosa nafasi kwenye safu ya mbele, wachezaji ambao wanapatikana na wenye uwezo wa kuchangia katika Ligi Kuu England.

"Jadon ni mmoja, anapokuwa fiti, atachangia kisha tuna chaguo la ziada na hivyo tutakuwa na nafasi zaidi ya kushinda michezo mingi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,063,6

MECHI KALI

VILLARREAL
VERSUS
REAL MADRID

1 | 3.21
X | 3.66
2 | 2.06

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# GREALISH: MAISHA YA CITY MAGUMU

**MANCHESTER,** England

JACK Grealish amesema kuzoea mtindo wa uchezaji wa Manchester City imekuwa "ngumu zaidi" kuliko alivyofikiria.

Mchezaji huyo wa England alinunuliwa kwa pauni milioni 100 kutoka Aston Villa na bado hajawa kwenye kiwango bora kama ilivyotarajiwa.

"Nilipokuja hapa, nitakuwa mkweli ilikuwa ngumu zaidi kuliko nilivyofikiria," alisema Grealish mwenye umri wa miaka 27 akiiambia Sky Sports baada ya ushindi wa bao 1-0 wa City dhidi ya Chelsea.

"Kichwani mwangu nilidhani naenda kwenye timu iliyoketi kileleni mwa ligi na ningepata mabao mengi na pasi za mabao, ni wazi sivyo.

"Kocha wa zamani wa Aston Villa, Dean Smith angeniambia niende kutafuta kiungo dhaifu kwenye safu ya ulinzi, iwe ni upande wa kulia au kati.

"Nilikuja City, nikiwa Villa maisha yangu yote, na sijawahi kubadilika. Nimekuwa nikizoea hilo kila mara. Sikutambua jinsi ilivyo ngumu kuzoea timu na kocha tofauti."

# *Potter alalamikia majeruhi Chelsea*



**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Graham Potter, amesema "sijawahi kukumbana na jambo kama hili" baada ya hali ya majeraha kuwa mbaya katika klabu hiyo huku Raheem Sterling na Christian Pulisic wakitolewa uwanjani wakati wa kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Manchester City hapo juzi.

Sterling alilazimika kutolewa nje baada ya dakika tano na Pulisic alimfuata dakika ya 17 baadaye kutokana na tatizo la goti huku mchezaji wa akiba wa City, Riyad Mahrez akifunga bao la ushindi kipindi cha pili na kuwafanya vijana wa Pep Guardiola kubakisha pengo la pointi tano nyuma ya vinara wa Ligi Kuu ya England, Arsenal.

Mason Mount pia hakuwapo baada ya kuumia mazoezini na watatu hao wakaungana na Wesley Fofana, Armando Broja, Reece James, Ben Chilwell na N'Golo Kante kuwa nje ya uwanja.

The Blues watamenyana na City tena katika mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la FA itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Etihad na Potter alisema: "Haifanyi iwe rahisi lakini ni wazi mapema sana kujua jinsi majeraha yalivyo mabaya."

"Halafu Christian naye atakuwa nje pamoja na Mason. Sijawahi kupata kitu kama hiki."

"Matarajio ni pale yalipo hivyo unataka kuwa hapa na kuwa na wachezaji wako wote na kuwa na kikosi fiti na kuweza kushindana."

## HABARI MICHEZO

605,974/-

# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/01/23 | 18:00 | KAS Eupen vs Royal Charleroi SC | 2.65 | 3.55 | 2.44 |
| 02. 07/01/23 | 18:00 | Millwall FC vs Sheffield United | 2.90 | 3.20 | 2.43 |
| 03. 07/01/23 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Burnley FC | 2.32 | 3.40 | 2.90 |
| 04. 07/01/23 | 18:00 | Cambridge United vs Bristol Rovers | 2.85 | 3.30 | 2.41 |
| 05. 07/01/23 | 18:00 | Morecambe FC vs Cheltenham Town | 2.50 | 3.25 | 2.75 |
| 06. 07/01/23 | 18:30 | RKC Waalwijk vs SC Heerenveen | 2.43 | 3.50 | 2.70 |
| 07. 07/01/23 | 20:30 | Brentford FC vs West Ham United | 2.65 | 3.25 | 2.65 |
| 08. 07/01/23 | 22:00 | Fortuna Sittard vs Go Ahead Eagles | 2.60 | 3.30 | 2.65 |
| 09. 07/01/23 | 22:45 | Royal Antwerp FC vs KAA Gent | 2.44 | 3.40 | 2.70 |
| 10. 07/01/23 | 23:00 | Espanyol Barcelona vs Girona FC | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 11. 08/01/23 | 14:30 | US Salernitana vs Torino FC | 3.20 | 3.20 | 2.25 |
| 12. 08/01/23 | 15:30 | Bristol City vs Swansea City | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 13. 08/01/23 | 17:00 | Spezia Calcio vs US Lecce | 2.55 | 3.10 | 2.85 |
| 14. 08/01/23 | 18:00 | SV Zulte Waregem vs Yellow-Red KV Mechelen | 2.70 | 3.70 | 2.32 |
| 15. 08/01/23 | 18:30 | FC Pacos Ferreira vs GD Chaves | 2.85 | 3.25 | 2.46 |
| 16. 08/01/23 | 18:45 | Excelsior Rotterdam vs FC Groningen | 2.65 | 3.55 | 2.45 |
| 17. 08/01/23 | 19:00 | Fenerbahce Istanbul vs Galatasaray Istanbul | 2.39 | 3.50 | 2.75 |

# MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 07/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 3394 | Reading vs Watford | 2.31 | 3.25 | 2.90 |
| 15:30 | 4867 | Tottenham vs Portsmouth | 1.11 | 7.88 | 16.75 |
| 15:30 | 4926 | Crystal Palace vs Southampton | 1.88 | 3.50 | 3.75 |
| 15:30 | 5414 | Gillingham vs Leicester | 12.86 | 6.33 | 1.18 |
| 15:30 | 5440 | Malaysia vs Thailand | 3.02 | 3.16 | 2.21 |
| 15:45 | 4444 | Pyramids vs Ghazl EL Mahallah | 1.35 | 4.59 | 8.77 |
| 16:30 | 3038 | Marumo Gallants FC vs Maritzburg Utd | 2.27 | 2.73 | 3.67 |
| 16:30 | 5306 | Golden Arrows vs SuperSport Utd | 2.92 | 3.02 | 2.46 |
| 17:00 | 3441 | Fiorentina vs Sassuolo | 1.67 | 3.81 | 4.55 |
| 17:30 | 1430 | Hyeres FC vs Marseille | 25.95 | 10.98 | 1.06 |
| 17:30 | 3106 | Lyon vs Metz | 1.27 | 5.55 | 9.32 |
| 18:00 | 1317 | Bournemouth vs Burnley | 2.38 | 3.31 | 2.76 |
| 18:00 | 1617 | Fleetwood Town vs QPR | 3.85 | 3.56 | 1.84 |
| 18:00 | 1942 | Bolton vs Plymouth | 2.06 | 3.42 | 3.32 |
| 18:00 | 2087 | Blackpool vs Nottingham | 4.04 | 3.70 | 1.76 |
| 18:00 | 2395 | Middlesbrough vs Brighton | 5.11 | 3.83 | 1.59 |
| 18:00 | 2506 | Rochdale vs Newport | 3.07 | 3.16 | 2.28 |
| 18:00 | 2572 | Hull City vs Fulham | 5.13 | 4.15 | 1.54 |
| 18:00 | 2909 | Celtic vs Kilmarnock | 1.08 | 9.55 | 20.89 |
| 18:00 | 3030 | Chesterfield vs West Bromwich | 4.93 | 4.04 | 1.58 |
| 18:00 | 4416 | St Mirren vs Hearts | 2.78 | 3.33 | 2.41 |
| 18:00 | 4558 | Ipswich vs Rotherham | 1.60 | 3.94 | 4.82 |
| 18:00 | 4981 | Shrewsbury vs Sunderland | 3.46 | 3.36 | 2.01 |
| 18:00 | 5810 | Ross County vs Livingston | 2.64 | 3.14 | 2.64 |
| 18:15 | 1432 | FC Andorra vs Real Oviedo | 2.13 | 2.97 | 3.66 |
| 18:15 | 2768 | Villarreal vs Real Madrid | 3.21 | 3.66 | 2.06 |
| 18:30 | 1641 | Cape Town City vs Orlando Pirates | 2.63 | 2.83 | 2.88 |
| 18:30 | 2032 | Levadiakos vs PAS Giannina | 2.40 | 2.99 | 3.09 |
| 18:30 | 3742 | Maccabi Tel Aviv vs FC Ashdod | 1.22 | 5.63 | 9.52 |
| 18:30 | 4873 | Waalwick vs Heerenveen | 2.40 | 3.46 | 2.67 |
| 19:00 | 1678 | Besiktas vs Kasimpasa | 1.54 | 4.49 | 4.98 |
| 19:00 | 3785 | Hapoel Haifa vs Hapoel Hadera | 1.94 | 3.31 | 3.55 |
| 20:00 | 1400 | AF Virois vs Nantes | 15.88 | 7.35 | 1.14 |
| 20:00 | 2203 | Ceramica Cleopatra vs Coca Cola | 3.09 | 2.79 | 2.54 |
| 20:00 | 2399 | Monaco vs Rodez Aveyron | 1.15 | 7.36 | 13.92 |
| 20:00 | 2584 | Juventus vs Udinese | 1.80 | 3.52 | 4.18 |
| 20:00 | 4850 | Al Masry Club vs El Ittihad Alexandria | 2.18 | 2.89 | 3.69 |
| 20:00 | 5601 | Le Puy vs Nice | 10.94 | 5.57 | 1.24 |
| 20:30 | 1027 | Malaga vs Tenerife | 2.68 | 2.88 | 2.78 |
| 20:30 | 1544 | Brentford vs West Ham | 2.44 | 3.26 | 2.72 |
| 20:30 | 2741 | Hapoel Katamon vs Beitar Jerusalem | 2.26 | 3.25 | 2.86 |
| 20:30 | 3740 | Mallorca vs Valladolid | 1.95 | 3.26 | 4.01 |
| 20:45 | 1358 | AZ Alkmaar vs Vitesse Arnhem | 1.51 | 4.36 | 5.35 |
| 21:00 | 2992 | Kaizer Chiefs vs Sekhukhune United | 1.90 | 3.12 | 4.26 |
| 21:00 | 5978 | Sheffield Wed vs Newcastle | 6.30 | 4.43 | 1.43 |
| 22:00 | 3286 | Fortuna Sittard vs GO Ahead Eagles | 2.49 | 3.34 | 2.64 |
| 22:45 | 1840 | Monza vs Inter | 5.36 | 4.17 | 1.53 |
| 23:00 | 1505 | PSV Eindhoven vs Sparta Rotterdam | 1.21 | 6.15 | 10.92 |
| 23:00 | 4945 | Espanyol vs Girona | 2.26 | 3.35 | 3.05 |
| 23:00 | 5444 | Liverpool vs Wolverhampton | 1.29 | 5.31 | 8.27 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# KOCHA MPYA KUTUA AZAM IKIJIPANGA KUSAJILI WANNE

**Hadija Mngwai na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC imesema iko katika hatua za mwisho za kutangaza kocha mpya ambaye atakiongoza kikosi hicho kilichoko kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara huku pia ikijiandaa kusajili wachezaji wapya wanne, imeelezwa.

Azam imekuwa chini ya Kally Ongala na Agrey Morris baada ya klabu hiyo kuachana na aliyekuwa kocha mkuu Mfaransa, Denis Lavagne, ambaye alidumu kwa muda wa mwezi mmoja.

Zaidi ya makocha 100 kutoka mataifa mbalimbali duniani yalituma maombi kutaka nafasi hiyo iliyoachwa wazi na Lavagne.

Kaimu Ofisa Habari wa Azam FC, Hasheem Ibwe, alisema licha ya kusimamisha mchakato wa kuteua kocha huyo kwa sasa, kuna majina sita yamewekwa kiporo na mmoja wao atatangazwa rasmi kukabidhiwa majukumu.

"Timu inacheza vizuri, matokeo mazuri inapata, hivyo kumleta kocha mpya ambaye atakuja na mfumo mpya na timu itatoka katika uhalisia uliokuwapo," alisema Ibwe.

Ofisa huyo aliongeza klabu yao inajipanga kufanya usajili mkubwa ambao unaweza kuwashtua wadau wa soka wa hapa nchini.

Kiongozi huyo alibainisha katika kipindi hiki cha usajili wataingiza wachezaji wanne wapya na kati ya hao, watatu watakuwa ni Watanzania na mmoja kutoka nje ya nchi.

"Kuna watu kama vile wanatukatia tamaa, lakini tarehe zenyewe za maumivu ni zile za mwisho za usajili, kuanzia terehe 13, 14 na 15, ndani ya siku hizi mbili tatu, tutatangaza mchezaji wa kwanza tuliyemsajili kwenye dirisha dogo na hiki chuma kitatoka nje ya nchi," alisema Ibwe.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema Azam imemshusha golikipa mwingine kutoka nje ya nchi kutokana na kutoridhishwa na kiwango Mcomoro, Ali Ahmada lakini pia Beno Kakolanya wa Simba naye akitajwa kuwindwa.



Hashim Ibwe

# *Simba yaenda Dubai kujiwinda*

INATOKA UK 32

"Mimi ni muumini mzuri wa vijana, nafurahi kuona kijana wangu huyo ameonyesha kiwango kizuri katika mechi hizi mbili za Kombe la Mapinduzi, lakini bado anahitaji nafasi ya kucheza ili kuendelea kupata ukomavu. Kama tunahitaji awe vizuri na tegemeo kwa hapo baadaye basi ninaimani viongozi watalifanyia kazi suala lake la kubakia KVZ kwa ajili ya kupata uzoefu," aliongeza.

Alisema kinda huyo anatakiwa kupata miezi sita mingine ya kucheza ligi kama ilivyo awali na msimu ujao kurejea katika kikosi kikubwa cha timu A ili awe tegemeo.

Wekundu hao wa Msimbazi katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iko katika Kundi C pamoja na Raja Casablanca ya Morocco, Horoya FC (Guinea) na Vipers ya Uganda, na itaanzia kampeni zake ugenini kwa kuwafuata Horoya kati ya Febuari 10 na 11, mwaka huu.

Ikirejea kutoka Dubai, Simba itawaalika Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Januari 17, mwaka huu.

# Yanga- Usajili wetu utasimamisha nchi

INATOKA UK 32

elekeza tufanye usajili wa aina gani kulingana na maeneo aliyoyaelekeza. Muda wowote ndani ya hizi siku 10 tutatangaza majina ya wachezaji hao na kufunga usajili wetu," alisema bosi huyo.

Aliongeza kila usajili unaofanywa unalenga kuziba makosa na madhaifu yaliyoko na wanaamini utaimarisha zaidi ubora wa kikosi chao hasa katika safu ya ushambuliaji ambayo kwa sasa inaongozwa na kinara wa mabao, Fiston Mayele.

"Kurejea kwa wachezaji wetu wawili, Yacouba Songne na Lazarous Kambole, ambao tunawaona katika mashindano haya ya Mapinduzi wakicheza, hii ni faraja, itawasaidia kurejea katika ubora wao," aliongeza Haji.

Yanga jana usiku ilikuwa inakutana na Singida Big Stars na timu itakayopata matokeo mazuri zaidi ndio itatinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo ya Kombe la Mapinduzi mwaka huu inatimiza miaka 17 tangu ilipoanzishwa.

Simba ndio walikuwa mabingwa watetezi wa michuano hiyo lakini wameondolewa mapema baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Kundi C, nyuma ya vinara Mlandege ambao wamesonga mbele.

Michezo
Nipashe Jumamosi Januari 7, 2023



Sancho aendelea kuivuruga Utd UKURASA 29



Kiungo, Feisal Salum maarufu Feitoto (katikati), akiwa ameambatana na watu wake wa karibu akiingia katika ofisi za Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) jijini, Dar es Salaam jana ili kusikiliza wito kuhusu malalamiko yaliyowasilishwa na Yanga. Hivi karibuni nyota huyo alitangaza kuvunja mkataba wake na klabu hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga- Usajili wetu utasimamisha nchi

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

WAKATI mshambuliaji wa zamani wa TP Mazembe ya DRC na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Thomas Ulimwengu, akitajwa anakaribia kutua Jangwani, mabosi wa Yanga wamesema usajili wao utakaofuata 'utatingisha' kwa sababu wanahitaji kutetea ubingwa wa Bara na kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Tayari Yanga imeshamtambulisha kiungo, Mudathiri Yahya kutoka KMKM ya visiwani hapa huku ikiweka wazi inahitaji kupata mshambuliaji mpya.

Makamu wa Rais wa Yanga, Arafat Haji, aliliambia gazeti hili kabla ya dirisha dogo la usajili halijafungwa, klabu hiyo itatangaza usajili mkubwa na kuongeza kwa sasa wako katika hatua za mwisho za mazungumzo na nyota hao.

Haji alisema baada ya kufanikiwa kuwaongeza mikataba baadhi ya wachezaji wao akiwamo kipa, Djigui Diarra, Khalid Aucho na Dickson Job sasa nguvu wanazielekeza kwa nyota wapya ambao ujio wao utasaidia kuimarisha kikosi chao.

"Kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili tutashusha majina mawili mapya mazito, usajili tunaoufanya ni mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha wetu, Nesreddine Nabi, kwa kutu-

INAENDELEA UK 31

# Simba yaenda Dubai kujiwinda

## ●●● Lengo kurejesha makali yake Bara na katika Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo...

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

KIKOSI cha Simba kinatarajia kuondoka nchini leo na kuelekea Dubai kwa ajili ya kuweka kambi ya muda ili kujiandaa na mechi za lala salama za Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na michezo ya hatua ya makundi ya michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imefahamika.

**Taarifa zilizopatikana jijini, Dar es Salaam zinasema lengo la kambi hiyo ni kumpa nafasi nzuri kocha mpya, Roberto Oliveira 'Robertinho' kukifahamu vyema kikosi chake na kukamilisha programu ya mazoezi aliyoiandaa na hatimaye kufikia malengo ya klabu.**

Chanzo chetu kilisema safari hiyo itawahusisha wachezaji wote waliosajiliwa na timu hiyo wakiwamo nyota wapya waliojiunga katika kikosi cha Wekundu wa Msimbazi wakati huu wa dirisha dogo.

"Timu imesharejea Dar na kesho (leo), tunatarajia kwenda Dubai, ni kambi ya muda mfupi lakini kocha mpya anaamini itamsaidia kukamilisha vitu muhimu na kurejea nchini tukiwa imara," kilisema chanzo chetu.

Chanzo hicho kiliongeza maandalizi ya safari hiyo yamekamilika na kutolewa mapema katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi kumekuwa ni nafuu kwa benchi la ufundi kurekebisha mapungufu waliyoyabaini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, alisema wameamua kurudi haraka katika uwanja wa mazoezi kwa ajili ya kukifanya kikosi chao kirejee kwenye ubora wake na kuwa tayari kupambana katika kila mechi watakayocheza.

Mgunda alisema wanafahamu Ligi Kuu Tanzania Bara imeingia katika hatua yenye ushindani na wao wanahitaji kupambana kusaka matokeo mazuri lakini pia wakihitaji kuona wanafika hatua ya nusu fainali au fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

"Tunatarajia kuingia kambini haraka, hatuna muda wa kupoteza, tunahitaji kuiandaa timu vizuri kwa sababu mbele kuna michuano ya kimataifa, huko kazi ni ngumu zaidi," alisema Mgunda.

Aliongeza kila mchezaji wa Simba anajua kiu ambayo wanayo na wanachohitaji ni kurejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa imara zaidi.

"Tulijiandaa kushindana na kutafuta matokeo mazuri katika hii michuano (Kombe la Mapinduzi), lakini bahati haikuwa kwetu, tunarudi nyumbani kwa ajili ya kujiandaa na kilichokuwapo mbele yetu hasa ni michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, na kumpa muda kocha mpya kuona kikosi chake," Mgunda alisema.

Aliongeza licha ya kuondolewa mapema, ameitaja michuano ya Kombe la Mapinduzi imewasaidia kupata mwanga wa kuwaona baadhi ya wachezaji ambao walikuwa hawapati nafasi ya kucheza mara kwa mara na kubaini ubora na madhaifu yao.

"Sasa tunaenda kufanyia kazi hayo mapungufu kuhakikisha tunayaondoa kabisa na ikishindikana kuyapunguza, ubora wetu kuuongeza kuwa bora zaidi," alisema kocha na mchezaji huyo wa zamani wa Coastal Union.

Kuhusu mchezaji wake chipukizi, Michael Joseph, kutoka Simba B, ambaye alikuwa kwa mkopo katika kikosi cha KVZ FC ya Zanzibar, Mgunda alisema anafurahi kuona kinda huyo ameonyesha kiwango kizurI na anaimani anahitaji kupewa nafasi ya kujiamini na kupewa muda zaidi wa kucheza.

INAENDELEA UK 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >